# Nipashe

Jumanne Februari 4, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580145

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710





UKURASA 13



## Magufuli ataja kilichowabeba viongozi wateule aliowaapisha

UKURASA 3



# Nabii Mwamposa ashukiwa kila kona

**VIONGOZI** wa dini wakemea mafundisho potofu, wataka manabii 'vizuka' wachunguzwe, DC Sabaya, Mwenyekiti CCM watema nyongo...*Endelea uk. 2*



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, akiongoza mamia ya waombolezaji kuaga miili ya waumini 20, waliofariki katika maombezi ya Mtume Boniface Mwamposa, katika Manispaa ya Moshi jana. **PICHA: MARY MOSHA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




## Mbowe amwandikia barua JPM

UKURASA 2

## WAWEKEZAJI KUANZISHA VIWANDA VYA BANGI

UKURASA 3


**MICHEZO** SIMBA YATAKA UBINGWA NA REKODI YA POINTI 100 UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Mwamposa ashukiwa kila kona

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI miili ya watu 20 waliofariki dunia kwa kukanyagana ikiagwa katika viwanja vya Majengo, Moshi, mkoani Kilimanjaro, viongozi wa dini na wanasiasa wamshukia kiongozi wa dini, Boniface Mwamposa, kutokana na vifo hivyo.

Pamoja na viongozi hao kunena mazito, serikali imesema haitafunga shughuli za dini na badala yake itashughulikia upungufu uliojitokeza na kusababisha vifo hivyo.

Baadhi ya viongozi wa dini walionyesha kuudhiwa na aina ya mafundisho yanayotolewa na baadhi ya madhehebu kwa sasa ikiwamo kuwaaminisha watu katika kutumia vitu, huku baadhi ya watu wanaojiita mitume na manabii wakitumika ulaghai wa kujipatia mali na kuwaahidi kupata mali.

Shughuli ya kuaga miili hiyo ilifanyika katika viwanja vya Mashujaa mjini Moshi na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, dini, chama na siasa, pamoja na mamia ya waombolezaji na wananchi wengine.

Mwakilishi wa Kanisa Katoliki, Padri Colman Siriwa, alisema Mungu amewapa wanadamu akili na utashi wa kutambua mambo fulani yakuwasaidia katika maisha.

"Siku hizi watu wanatafuta majibu rahisi kwa maswali magumu ya maisha na viongozi wengi wanatoa majibu rahisi kwa mambo magumu hata tukitumia njia ovu kiasi gani ili mradi tumepeleka jawabu bila kujali litamwathiri kiasi gani. Ni wakati wa kujiuliza nipo katika njia sahihi ya kutafuta majibu rahisi? Na kiongozi ninatoa majibu rahisi kwa ninaowaongoza?" Alisema.

Alisema umefika wakati kwa viongozi wa dini kujitafakari kwamba kondoo waliokabidhiwa kama wanawapeleka sehemu sahihi na kama sivyo wachukue hatua kwa kusaidia na viongozi pamoja na utashi waliopewa.

"Ni kweli tunasikitika kwa kilichotokea ni kosa moja linaleta simanzi kiasi hiki. Tunapaswa kulitubu na tutubu kweli kama viongozi wa dini," alisema na kuongeza:

"Tunaomba ukomavu wa waumini wetu, wafuate njia sahihi waliyoelekezwa kwenye madhabahu yao bila kuyumbishwa na vizuka vizuka vinavyojitokeza. Vizuka hivyo kabla havijachekiwa vizuri vitatupeleka mahali pabaya sana. Tukio hili ni shule inayoumiza mioyo yetu lakini ndiyo funzo."

Naye Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mlima Kilimanjaro, Dk. Stanley Hotay, alisema vifo hivyo vimesababishwa na ulaghai, uzembe na udanganyifu na kwamba viongozi wa dini wana jambo la kutubu kwa familia na taifa kwa ujumla.

"Tusitumie uhitaji wa watu kuwa mtaji wetu. Waliokufa wote ni wahitaji...sisi tunao-

INAENDELEA UK 8



Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mbowe amwandikia barua Magufuli

**Na Enock Charles**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, amemwandikia barua Rais John Magufuli kumwomba kuanzisha mchakato wa kubadilisha baadhi vifungu katika katiba na sheria ili kuwezesha uwapo wa tume huru ya uchaguzi itakayosimamia uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Akiisoma barua hiyo aliyosema tayari imeshafikishwa kwa Rais mbele ya waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mbowe alisema lengo la kuandika barua hiyo kwa Rais ni kuepusha kile alichodai machafuko yanayoweza kutokea wakati, kabla na baada ya uchaguzi huo ili kudumisha amani na utulivu nchini. "Chadema tunaleta kwako mapendekezo yetu ya awali ya kulikwamua taifa katika sintofahamu hii inayolinyemelea taifa. Chadema tunaamini 'prevention is better than cure' (kinga ni bora kuliko tiba)," Mbowe alisoma sehemu ya barua hiyo.

Sheria na vifungu vya katiba ambavyo Kiongozi huyo wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni alisema vinahitaji kumulikwa ni pamoja na Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ya Mwaka 2015 na Sheria ya Gharama za Uchaguzi.

Sambamba na kurekebishwa kwa sheria hizo, Mbowe pia alisema katika barua yao hiyo, wamemwomba Rais kuunda tume ya maridhiano ya kitaifa na kurudiwa kwa uchaguzi wa serikali za mitaa, uliofanyika Novemba 24 mwaka jana kwa kile wanachodai haukuwa huru na haki.

Alidai taratibu za uchaguzi huo zilikiukwa na kukiwezesha Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupita bila kupingwa.

Mbowe aliwaambia waandishi wa habari kuwa masuala ambayo chama hicho kingependa yajadiliwe katika tume ya maridhiano ni; kupotea kwa watu katika mazingira yenye utata, kufanya uchunguzi na kufuta kesi alizodai zina sura ya kisiasa, kufuta makatazo yote ya kufanya mikutano ya hadhara, kutafuta mwafaka kati ya baadhi ya wakuu wa mikoa na wilaya na wananchi, na kuondoa mfumo wa kodi usio rafiki kwa wawekezaji.

Juhudi za Nipashe kupata taarifa za ama kupokewa au kutopokewa kwa barua ya Chadema Ikulu hazikuzaa matunda baada ya simu ya Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Gerson Msigwa, kuita bila kupokewa alipotafutwa na hata alipotumiwa ujumbe mfupi wa maandishi hakujibu.

## ... Sakata lake latua bungeni

**Na Godfrey Mushi, DODOMA**

SAKATA la watu 20 kupoteza maisha na wengine 16 kujeruhiwa wakati wakigombea kukanyaga mafuta yanayodaiwa kuwa na upako katika Uwanja wa Majengo, Moshi, Kilimanjaro limetua Bungeni jijini hapa.

Februari Mosi, mwaka huu, watu hao walipoteza maisha baada ya Mtume na Nabii Boniface Mwamposa, maarufu kama 'Buldoza' wa Kanisa la Calvary Assemblies of God, kudaiwa kuwaelekeza waumini wake wapite katika sehemu ambayo ilikuwa na turubai lililomwagwa mafuta ili wapate nafuu ya matatizo au shida zao.

Hoja ya dharura ya kulitaka Bunge lijadili tukio hilo na kutoa maelekezo kwa serikali iliwasilishwa jana kwa nyakati tofauti na Mbunge wa Geita Vijijini (CCM), Joseph Musukuma na Mbunge wa Vunjo (NCCR Mageuzi), James Mbatia.

Aliyeanza kulishawishi Bunge kujadili mkasa huo, alikuwa Musukuma ambaye alisimama na kusema: "Nasimama kwa kanuni ya 47(1) na naisoma na kifungu cha 3. Kwanza nianze kwa kutoa pole kwa ndugu zetu waliopoteza ndugu zao kule Kilimanjaro, Jumamosi ya Februari 1, 2020 na yaliyotokea yote wabunge tunafahamu mpaka kusababisha ndugu zetu 20 kupoteza uhai.

"Naomba kutoa hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge, kwa sababu suala hili ni zito na ili tuone namna ya kulijadili na kulitolea uamuzi. Kumekuwa na maneno tofauti tofauti, tunaona mitandaoni wabunge wenzetu wanaongea, wanatoa kauli za kulaumu serikali wakati sheria za usimamizi wa vikundi hivi, tumevitunga sisi wenyewe Bungeni," alisema.

Musukuma alisema anaona kuna umuhimu wa kukaa kama Bunge wakajadili na kuona namna ya kuliweka jambo hilo likae vizuri, kwa sababu wenzao wamepoteza maisha.

"Lakini sidhani kama kuna umuhimu sana na kulaumu wachungaji kwa sababu haya mambo yapo na ni masuala ya kiimani. Kwa hiyo nilikuwa naomba tujadili kwa sababu kila mtu humu ndani ana imani yake. Sasa hatuwezi tu kuzuia kwamba kulikuwa makosa, basi kwa idhini yako naomba tujadili, naomba kutoa hoja," alisisitiza Musukuma.

Baada ya kutoa hoja hiyo, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisimama na kulieleza Bunge kuwa hoja ya Musukuma haikuungwa mkono.

Dakika chache baada ya kauli ya Spika Ndugai, Mbatia alisimama tena na kuijenga upya hoja hiyo akitumia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

INAENDELEA UK 26


bgtl BEST GROUP (T) LIMITED
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADAWA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **First National Bank t (FNB),** tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya wadaiwa wao, ambazo ni Nyumba kama zilivyoorodheshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea.

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | **Josia Kinabo Bihemo** | Nyumba ya makazi yenye Hati na.59739LR, Kiwanja na.1264, Kitalu B, iliyopo eneo la Kiseke, katika Jiji la Mwanza kwa jina la **JOSIA KINABO BIHEMO.** | 21/02/2020 |
| 2 | **Mansoor Karama Saleh Investment** | Nyumba ya makazi yenye Hati na.7369, Kiwanja na.77, Kitalu "H", iliyopo eneo la Nyamanoro jijijni Mwanza kwa jina la **KARAMA SALEH MANSOOR.** | 22/02/2020 |
| 3 | **Mansoor Karama Sarehe Investment** | Nyumba ya makazi yenye Hati na.31570, Kiwanja na.643, Kitalu "M" iliyopo eneo la Pasiansi jijini Mwanza kwa jina la **HERBERT MOSES BUHANGWA.** | 22/02/2020 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa Au kuchukua mshindi wa pili.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**Contact: +255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**First National Bank Tanzania Limited (FNB)**
**Ohio street**
**P.O.BOX 72290,**
**DAR ES SALAAM**
**Contact I:+255 713963596**
**0758502628**
**Email: info@fnb.co.tz**

HABARI KITAIFA

# Magufuli ataja kilichowabeba wateule wapya aliowaapisha

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli ametaja vigezo alivyotumia kuwateua viongozi mbalimbali aliowaapisha jana Ikulu jijini Dar es Salaam, kikubwa kikiwa ni uchapakazi uliosababisha baadhi yao kuchukiwa.

Akizungumza baada ya kuwaapisha viongozi hao aliowateuwa siku ya mwezi uliopita, Rais Magufuli aliwataka wakafanye kazi kwa ushirikiano na wale watakaokuwa wanawaongoza.

Katika hafla hiyo, Rais Magufuli alimtaja kila mmoja kwa jina, nafasi aliyokuwa nayo awali na mpya aliyompatia na sababu iliyomsukuma amteue na anachotakiwa kwenda kukifanya.

Akimwelezea Kamishna Jenerali mpya wa Magereza, Brigedia Jenerali Suleiman Mzee, aliyechukua nafasi ya Phaustine Kasike aliyeteuliwa kuwa balozi, Rais Magufuli alisema:

"Ni miongoni mwa ma-brigedia wanaochapa kazi sana. Alikuwa mkuu mpya wa Komandi ya Pangau, aliikuta ipo chini, akaisimamia vizuri, akajenga nyumba, akanunua magari kwa kutumia 'force account'.

"Hakai ofisini, nilipokuwa napata shida Magereza namna ya kutafuta apatikane mwingine, nikasema wote siyo wanafundishwa mafunzo ya aina moja ya mguu pande, mguu sawa, mwili legeza, nyuma geuka, nikaona bora nimpeleke huyu.

"Niliona nikiteua wa chini yake wale wa juu watamdharau na wa juu zaidi anafanya kazi nzuri, lakini amebakiza miezi minne astaafu, anayefuatia naye anafanya kazi nzuri, lakini nikaona kwenye kazi hii ya Kamishna Jenerali, hatatusaidia sana, lakini ni mama mmoja injinia mzuri sana, nazungumza ukweli kutoka moyoni, sitaki kuwa mnafiki."

Rais Magufuli alisema aliamua apeleke Brigedia Jenerali Magereza kwa sababu 'haiwezekani nyumba zikitaka kujengwa, watumie Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) wakati wafungwa wapo'.

"Hicho kilikuwa kinaniumiza kweli, wakapewa mradi wa Sh. bilioni tisa wa kiwanda cha karanga, bado jengo lilikuwa halijaisha na mashine nafikiri zitakuwa zimekuja.

"Ninasikia baada ya kuzungumza juzi, wanafanya kazi usiku na mchana. Hicho ndiyo kisa kilichonifanya nichague Brigedia Jenerali Mzee," alisema.

Kuhusu Kamishna Jenerali mpya wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (DCP), John Masunga, aliyechukua nafasi ya Thobias Andengenye, ambaye uteuzi wake umetenguliwa, Rais Magufuli alisema alikuwa anafanya kazi nzuri Magereza.

Rais Magufuli alisema Kamishna Jenerali Masunga ambaye awali alikuwa Naibu Kamishna wa Magereza (DCP), angemteua palepale Magereza lakini watu watatu au wanne wamemtangulia, hivyo angepata shida.

"Nilijua atapata shida kama yule aliyeondoka kwa sababu walimwachia tu anazunguka, anafanya mikutano hadi saa nane wengine wamelala, hakupata ushirikiano na yeye hakutaka kutumia intelijensia kujua kama anasafiri na watu au peke yake.

"Nikaona katika kufanya mabadiliko, nimpeleke Zimamoto, ni matumaini yangu yaliyofanywa na waliotangulia hutayafanya, yakiwamo ya aliyekuwa Mkuu wa Utawala ambaye naye alitoka Magereza, ndugu Simwanza.

"Kafanye kazi, na utakuwa na faida umetoka magereza wakati mwingine unaweza kutokea moto kwenye mashamba, wapeleke wafungwa kwa sababu unawajua," alisema.

Rais Magufuli akimwelezea Nathaniel Nhonge ambaye ni Kamishna mpya wa Ardhi, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, alisema Mkoa wa Dar es Salaam una matatizo mengi ya ardhi na anaamini atayatatua.

Kuhusu Jaji Gerald Ndika, Rais Magufuli alisema alikuwa Jaji wa Mahakama Kuu na alifanya vizuri na kupandishwa kuwa Jaji wa

INAENDELEA UK 8



Rais John Magufuli akimwapisha Dk. Hassan Abbas kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Wawekezaji waomba kuja kuchakata bangi

**Na Godfrey Mushi, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Anjela Kairuki, amesema ofisi yake imepata wawekezaji wakubwa wawili ambao wameonyesha nia ya kuwekeza katika kilimo ikiwamo kuchakata mafuta ya bangi kwa ajili ya matibabu.

Kairuki alikuwa akimpa taarifa mchangiaji aliyekuwa akichangia mjadala wa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mbunge wa Kahama Mjini (CCM), Jumanne Kishimba, aliyetaka serikali ipitishe jambo hilo mapema kabla bei ya bangi haijaporomoka.

Kishimba wakati anachangia mjadala huo alisema bei ya bangi duniani imepanda maradufu na nchi zote alizozizunguka wamesharuhusu kilimo cha zao hilo, hivyo anamwomba Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, atoe ufafanuzi kwamba watu wanaotaka kulima wamuone nani.

"Waliopiga marufuku bangi ni Wazungu miaka ya 40, lakini Wazungu walewale waligundua ndani ya bangi kuna dawa, na sisi wenyewe tunaenda kwenye viwanda vya dawa. Je, sisi tuki- import dawa zenye material ya bangi (tukiagiza dawa zenye malighafi itokanayo na bangi) tutakuwa tumeagiza kutoka wapi na tuta declare (kutangaza maslahi) namna gani. Kwa kuwa bei ya masoko duniani ni bei ya ushindani... ni vizuri serikali ifanye uamuzi huo mapema zaidi.

Kishimba aliongeza: "Tanzania kwa Afrika ni nchi ya tatu kwa kulima bangi kwa magendo na kama wataruhusu na sheria kama ilivyo inaweza sana ikatusaidia kutupeleka mahali. Lakini kwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi (George Simbachawene) yuko hapa anaweza akatoa msamaha hata kwa bangi iliyokamatwa kwa muda wa miezi sita, kama msamaha anavyoutoa wa silaha."

Kwa mujibu wa Kishimba, msamaha huo kama utatolewa na wananchi wakawasilisha bangi hizo Polisi, watu wakauziana bangi hiyo Polisi na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) watapata mapato na wanunuzi wakaja kununua hapa, linaweza kusaidia wenzetu wakapata pesa na kwa hali hiyo, lazima tuende haraka sana.

"Uganda wamepewa na Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), zaidi ya Dola milioni 500 kwa ajili ya kilimo cha bangi, na kwamba kwa kuwa tulianza kulima bangi muda

INAENDELEA UK 8

# Daktari afichua nyama ng'ombe inavyotoa mimba

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

DAKTARI wa Mifugo, Meljory Mariki, kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, amesema ulaji wa nyama ya ng'ombe ambayo haijapimwa na wataalamu wa mifugo, umekuwa ukisababisha tatizo la utokaji wa mimba (Brucelosis).

Amesema nyama isiyopimwa pia husababisha ugonjwa kifua kikuu (TB), kimeta na kueneo wa home ya bonde la ufa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Dk. Mariki alisema asilimia 75 ya magonjwa ya binadamu yanasababishwa na wanyama ambao wanachinjwa kinyemela bila kufuata taratibu na sheria za uchinjaji.

Dk. Mariki alisema jamii inashindwa kutambua umuhimu wa kupima wanyama kabla ya kuchinjwa, inasaidia kupunguza maambukizo ya magonjwa hayo ambayo dalili zake hutokea baada ya mwezi mmoja au miwili. "Hakuna sababu ya wafanyabiashara kuchinjia nyama vichochoroni kukwepa kodi ya uchinjaji, lakini ukumbuke unapofanya hivyo unaiumiza jamii inayokwenda kutumia kitoweo hicho kwa sababu kitawasababishia madhara endapo ng'ombe atakuwa na magonjwa," alifafanua.

Alisema ni vema watu wakatumia machinjio ambayo yaliyohalalishwa na ina vigezo vyote vikiwamo vya vifaa maalum vya utambuzi wa afya ya mnyama.

"Jana (juzi) tuliteketeza kilo 200 za nyama, baada ya kupima tulizibaini zina ugonjwa," alisema.

Mtaalamu huyo alisema machinjio yanapaswa kuwa na vifaa maalum kwa ajili ya kutambua kama ng'ombe ana magonjwa au la, hivyo akatoa wito kwa wananchi kutumia machinjio ya kisasa ya Dodoma, ambayo imeyaboresha kwa kiasi kikubwa.

Kaimu Meneja Mkuu wa Machinjio ya Dodoma, Victor Mwita, aliwataka wafanyabiashara ya nyama kupeleka ng'ombe kwa ajili ya kuchinja katika machinjio hayo kwa kuwa ni salama na yana vigezo vyote badala ya kwenda kuchinja vichochoroni.

Ofisa Usajili wa Bodi ya Nyama, Godfrey Kakuru, alisema bodi hiyo imekuwa ikifanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha machinjio ya nyama yanafikia vigezo vinavyowekwa kisheria.

"Badaa ya ukaguzi tulifanikiwa kuwabaini wafanyabiashara zaidi ya 25 ambao wamekutwa na makosa mbalimbali yakiwamo ya uuzaji nyama isiyokaguliwa na daktari, usafirishaji nyama katika viroba, kusafirisha nyama kwa kutumia vifaa visivyosajiliwa kama pikipiki na magari binafsi. Pia tulibaini usafirishaji wa mifugo kama mbuzi, kuku kwenye magari ya abiria-daladala, uuzaji nyama kwenye maeneo ya wazi na uchinjaji wa mifugo katika maeneo yasiyokidhi ubora," alisema.

# Mhagama ataka miradi ya maendeleo kibiashara

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, amewataka watendaji katika ngazi ya halmashauri na serikali za mitaa kusimamia kikamilifu miradi inayofadhiliwa na wadau wa maendeleo katika maeneo yao ili iwe endelevu kwa kujiendeleza kibiashara.

Akizungumza katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo iliyofadhiliwa na Ubalozi wa Denmark kupitia Mradi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (LIC) ambayo umelenga kuwakwamua kiuchumi wananchi wa mkoa wa Dodoma hususan vijana na wanawake mwishoni mwa wiki, alisema miradi hiyo lazima iwe endelevu.

"Serikali inataka kuona miradi iliyoanzishwa na wafadhili mkoani Dodoma inakuwa endelevu kwa kuwafanya wananchi kushiriki kwenye miradi hii hali itakayoleta hamasa kubwa kwa wafadhili kuendelea kujitoa kuchangia miradi ya maendeleo," alisema Waziri Mhagama.

Alisema gharama kubwa imetumika katika miradi ya mnada wa kuku Mbande katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, mradi wa kuwezesha vijana kujiajiri kupitia ufundi - Hombolo na mradi wa kiwanda cha kuchakata mazao ya zabibu iliyopo Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

"Miradi hii inakwenda kutatua changamoto zilizopo katika usindikaji wa zabibu kwani asilia kubwa ya zao hili lilikuwa inaharibika kwa kukosa kiwanda cha kuchakata, tatizo la ajira kwa vijana litakwenda kupungua baada ya kupata ujuzi kupitia mradi wa ufundi Hombolo," alisema.

Waziri alisema miradi yote ilitokana na majadiliano kati ya sekta za umma na sekta binafsi iliyokuwa na lengo la kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ambayo ilifadhiliwa na LIC kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Biashara (TNBC).

Alisema mradi unakwenda umefikia ukingoni hivyo halmashauri zinatakiwa kuja na mbinu ambazo zitasaidia kufanya miradi hii kuwa endelevu kwa kuwapatia wananchi kipato ili kuondokana na umaskini katika jamii.

"Haitakuwa na maana kama wafadhili watamaliza muda wao na miradi isimame, tunapaswa kuifanya miradi hii iendelee ili faida ya kuanzishwa kwake iweze kuonekana hasa katika kumwinua mwananchi kiuchumi," alisema. Waziri Mhagama alisema miradi hii inachangia katika utekelezaji wa azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025, hivyo miradi ikiendelezwa kibiashara wananchi watafaidika na nchi kwa ujumla kupita makusanyo ya kodi.

Katika hatua nyingine Waziri Mhagama alipongeza TNBC na LIC kwa namna walivyoshirikiana kukamilisha miradi hiyo kwa wakati na katika viwango vinavyotakiwa, hivyo ni jukumu la wananchi kuchangamkia fursa zilizopo katika miradi hii.

Katibu Mtendaji wa TNBC, Dk. Godwill Wanga, alisema baraza lake litaendelea kushirikiana na halmashauri kuhakikisha miradi iliyopo katika maeneo yao inakuwa endelevu ili thamani ya fedha iliyotumika kukamilisha miradi iendane na shughuli za kibashara katika miradi hiyo.

"Kama baraza tutaendelea kushirikiana na halmashauri na pia sekta binafsi kupitia mikutano ya majadiliano ambapo changamoto mbalimbali zinajadiliwa na kupatiwa majibu ambayo yatasaidia kufanya miradi hii kuwa endelevu," alisema Dk. Wanga.

Naye Meneja wa Mfuko wa Uwezeshaji miradi midogo kutoka LIC, Goodluck Mghonu, alisema miradi mitatu ilifadhiliwa katika Jiji la Dodoma na Mkoa wa Kigoma zaidi ya miradi mitano ambayo jumla yake iligharimu zaidi ya Sh. bilioni 16 ambayo ililenga kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji nchini.




Meneja wa Benki ya DTB tawi la Nyerere, Zainab Rashid (kushoto), akipongezwa na Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Viju Cherian, baada ya tawi lake kuwa bora zaidi kwa mwaka 2019, katika sherehe za mwisho wa mwaka jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni tuhuma usafirishaji madini

**Na Julieth Mkireri, CHALINZE**

JESHI la Polisi mkoani Pwani, linawashikilia watu sita kwa tuhuma tofauti ikiwamo ya wanaodaiwa kuhusika na usafirishaji madini yanayodhaniwa kuwa ni sunstone, yanayotumika kutengeneza vito na urembo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema jana kuwa watuhumiwa wa usafirishaji wa madini walikamatwa wakiwa na mifuko mitano ya viroba.

Alisema mifuko waliyokamatwa nayo ilikuwa na uzito wa kilo 234.5 ikiwa na madini hayo yenye thamani ya Sh. 703,500 wakiyasafirisha kutoka Mpwapwa mkoani Dodoma kuelekea Dar es Salaam.

Aliwataja watuhumiwa hao ni Emmanuel, mkazi wa Mbezi; Ally Amour, mkazi wa Kawe na Joseph Ngauka, mkazi wa Chanika mkoani Dar es Salaam.

Aidha, jeshi hilo linamshikilia mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Mkombozi wilayani Same Mkoa wa Kilimanjaro kwa tuhuma za kukutwa na vifurushi 74 vya mirungi.

Inadaiwa mwanafunzi huyo alikamatwa katika eneo la Msata Februari mosi, majira ya asubuhi, akiwa anaisafirisha kutoka Same kwenda Dar es Salam.

Kamanda Wankyo alisema mwanafunzi huyo anashikiliwa katika Kituo cha Polisi Chalinze.

Katika hatua nyingine, Kamanda Wankyo alisema, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na kikosi cha kudhibiti ujangili wamewakamata watuhumiwa wawili maeneo ya Mdaula, wakiwa na vipande 10 vya meno ya tembo na vipande 23 vya magego ya tembo.

Alisema tukio hilo likitokea Januari 31, mwaka huu, na kwamba watuhumiwa hao walikutwa katika nyumba ya kulala wageni eneo la Mdaula na vipande hivyo ambavyo walikuwa katika mpango wa kuviuza.

## Wabunge washauri TIC kupewa nguvu

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WAJUMBE wa kamati mbalimbali za Bunge wameridhishwa utendaji wa Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC) na kusema kuwa marekebisho ya sheria ya uwekezaji yatasaidia kuondoa upungufu uliyopo na kuchochea kasi ya ukuaji wa uwekezaji.

Mbali ya kukipongeza kituo hicho kwa kazi kubwa inayofanya kuhamasisha vivutio vya uwekezaji nchini, wajumbe walisema kituo kimekuwa kikikwamishwa na mwingiliano wa majukumu yake na taasisi nyingine wezeshi za serikali.

Akichangia katika semina iliyoandaliwa na TIC kwa kamati 12 za Bunge ili kujifunza kazi mbalimbali za kituo jijini hapa mwishoni mwa wiki, Lucy Mayenga alisema kituo kinafanya kazi nzuri isipokuwa kinakwamishwa na mwingiliano wa kazi zake na taasisi nyingine.

"Ni matumaini ya walio wengi kuwa marekebisho yanayofanywa kwa sheria ya uwekezaji yatakuwa chachu na kuchochea ukuaji na ustawi wa uwekezaji Tanzania," alisema Mayenga na kuongeza kuwa

Tanzania inaweza kufanya vizuri katika nyanja za uwekezaji. Godbless Lema alisema sheria mpya ya uwekezaji itakuwa mwarobani kwani kumekuwa na mkanganyiko mkubwa katika suala la kuhamasisha na kuvutia uwekezaji badala ya kazi hiyo kufanywa na TIC kwa umakini mkubwa.

"Natambua kazi nzuri inayofanywa na TIC, lakini kuna kipindi kazi zinaingiliwa sana taasisi zingine za serikali, hivyo inaleta ugumu mkubwa katika utendaji kazi wake," alisema Lema na kuongeza kuwa TIC inabidi iungwe mkono wakati wote.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mashimba Ndaki, alishauri serikali kufanyia kazi sheria za uwekezaji ili kwenda sambamba na kasi ya Serikali ya Rais John Magufuli.

"Tunaridhishwa na kazi za TIC pamoja na upungufu uliyopo kwenye sheria iliyopo sasa, lakini marekebisho yatakayofanywa kwenye sheria hiyo yatachochea ukuaji wa sekta ya uwekezaji hapa nchini," alisema.

Akiwasilisha mada kwa kamati za Bunge, Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Geoffrey Mwambe, alisema kituo kimepewa jukumu na serikali la kusimamia na kuhamasisha uwekezaji hasa katika viwanda ya uzalishaji na kuongeza thamani katika sekta zote.

Alizitaja nchi kumi zinazoongoza kwa uwekezaji chini kati ya mwaka 1990 mpaka 2018 ni China, Uingereza, Marekani, Mauritius, India, Australia, Kenya, Uholanzi, Ubelgiji na Misri.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, aliwashukuru wajumbe wote wa kamati kwa michango yao mizuri na iliyolenga kuboresha marekebisho ya sheria ya uwekezaji.

# RC aona shida ubora wa taulo za kike

**Na John Mapepele, SINGIDA**

MKUU wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, amewataka wawekezaji na wafanyabiashara wa taulo za kike kuacha mara moja tabia ya kutengeneza na kuuza taulo zisizo na ubora.

Amesema mkoa wake umeanza msako wa kiintelijensia kuzinasa taulo zisizo na ubora na atakayebainika, sheria itachukua mkondo wake mara moja.

Dk. Nchimbi aliyasema hayo jana wilayani Ikungi wakati wa uzinduzi wa kampeni maalum ya uchangishaji wa taulo za kike katika Mkoa wa Singida iliopewa jina la "Mjali mtoto wa kike kwa maendeleo yake na taifa lake'.

Alisema kutokana na mageuzi makubwa ya kiuchumi yanayofanywa na serikali, nchi imekuwa kwenye mashindano ya kiuchumi duniani, hivyo mikakati madhubuti ya kudhibiti ubora inahitajika katika kipindi hiki kuliko kipindi kingine chochote.

Akizindua kampeni hiyo, Dk. Nchimbi alisema vyombo vya dola, viongozi wa dini na wazazi wana mchango mkubwa katika kumlinda mtoto wa kike kwa ustawi wa taifa.

"Ndiyo maana tunasema na tunamaanisha kuwa tunataka kujua mipango ya udhibiti wa ubora kwa watengenezaji hawa kwa kuwa majuto ni mjukuu, tusisubiri kufika huko," alisisitiza.

Aliongeza kuwa ubora wa taulo za kike ni ubora wa maisha yao, hivyo ni muhimu kuchukua hatua za kuangalia na kudhibiti mnyororo mzima wa uzalishaji na usambazaji wa taulo sizizo kuwa na ubora.

Kiongozi huyo wa mkoa alitoa wito wa wajasiriamali kuja na andiko zuri la utengenezaji wa taulo bora za kisasa zitakazotengenezwa kwa kutumia malighafi za nchini, akiahidi kuwa mshindi atapata zawadi ya Sh. milioni moja.

Aliwataka watoto wa kike kote nchini kujiamini kwa kuumbwa wanawake na kwamba hedhi ni kitu cha thamani kwa kuwa ni uhai, akisisitiza elimu ya jinsia na mtoto wa kike kutambua mabadiliko ya miili yao iendelee kutolewa ili kuwajenga watoto wa kike kujua thamani ambayo Mungu amewajalia.

Aliwataka wadau wote kuendelea kuchangia kwa kutambua thamani ya mtoto wa kike, lengo la kampeni hiyo ikiwa ni kuchangia paketi 8,000 za taulo za kike, lakini zilipatikana paketi 9,089 kulingana na fedha zilizotolewa.

Alibainisha kuwa malengo kwa mwaka huu katika Wilaya ya Ikungi ni kuchangia taulo 192,000 kwa watoto wote wa kike kwenye shule 36 za sekondari na shule 131 za msingi zenye watoto wa kike 16,000.

Alisema serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika huduma za afya zenye ubora na zinazowafikia wananchi wote ili kuboresha afya zao.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi, akifafanua jambo kwenye mkutano wa Bajeti wa Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo, mkoani Singida jana. **PICHA: ELISANTE JOHN**

# Mapinduzi ya kahawa yanukia Mara

**Na Mwandishi Wetu**

MKAKATI wa kuongeza zao la kahawa mkoani Mara umeanza kwa lengo la kufikisha tani 15,000 kutoka tani za sasa 1,500, hivyo kufikisha uzalishaji wa Sh. bilioni 10.

Katika kufikia lengo hilo, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imefanya mapinduzi makubwa ya zao la kahawa aina ya Arabica mkoani humo.

Zao hili limekuwa likizalishwa kwa kiwango kidogo mkoani humo licha ya kuwa Arabica bora Africa inatoka Wilaya ya Tarime.

Benki hiyo kwa kushirikiana na mkoa wa Mara pamoja na wadau mbalimbali ikiwamo Bodi ya Kahawa (TCB) na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa (TACRI) wameanza kutekeleza kwa vitendo.

Kwa kuanza na mkakati huu, TADB imeshiriki katika uzinduzi wa upandaji wa miche bora ya kahawa katika vitalu mbalimbali kwenye wilaya zote nne za mkoa wa Mara ikiwamo Butiama, Rorya, Tarime na Serengeti.

Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima ambaye aliongoza uzinduzi huu, alieleza kuwa mpaka sasa nchi inazalisha kahawa tani 48,000 (Robusta na Arabica) na lengo ni tani 200,000 kwa mwaka.

Alisema Mkoa wa Mara ni kati ya mikoa inayozalisha kahawa bora na safi nchini, na umenuia kutimiza lengo kwa kushirikiana na wadau muhimu ikiwamo TADB ambao wamekuwa kinara nchini kwa kuwawezesha wakulima, wafugaji na wavuvi nchini.

"Kwa sasa mche wa kahawa unazalisha gramu 250 kwa mwaka kwa msimu mmoja, ila kwa kutumia mche mpya uliofanyiwa utafiti na uliozalishwa na TACRI utakuwa unatoa gramu 3,000 ambayo ni mara 12 zaidi ya miche ya zamani," alisema na kuongeza:

"Vilevile na miche hii inayozalishwa haina gharama kubwa za ukuzaji na kutokuwa na mashambulio ya magonjwa kama chule buni. Na kwa wastani mkoa mzima unazalisha tani 1,500 na miche hii mipya itazalisha tani takribani 15,000."

Malima alisema kwa kushirikiana na TADB na TACRI, wakulima na AMCOS watajengewa uwezo wa kuendesha kilimo na uwekezaji pamoja na kuelimishwa mbinu za kilimo sanifu na bora kuanzia upandaji, ukuzaji na mpaka uvunaji.

Kwa sasa kilo moja ya kahawa inauzwa kwa wastani wa Sh. 900 hadi Sh. 1000 ambapo, kwa kutumia miche hii bora, bei ya soko ni shilingi 3,500 hadi Sh. 4,000 kwa kilo na uzalishaji ni mwingi kwa kupitia miche hii mipya hivyo kuongeza kipato kwa mkulima. Na hii imethibitika kutoka kwa wakulima wachache mkoani hapo ambao wamefuata kanuni za kilimo bora na miche na

Benki ya Maendeleo ya Kilimo inaendelea kutoa huduma mbalimbali kwa wakulima kwa lengo la kuchagiza maendeleo katika sekta ya kilimo nchini. Huduma hizo ni kukuza upatikanaji mitaji na uwekezaji katika kilimo na mnyororo wa thamani ya mazao ya kilimo.

# Bilioni 1.5/- kujenga chuo

**Na Mwandishi Wetu, UYUI**

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Tabora (Uyui), limeishukuru serikali kwa kuwapatia Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (Veta) katika eneo la Isikizya.

Fedha hizo zitasaidia katika ujenzi wa majengo ya fani mbalimbali ikiwamo ushonaji, ufundi umeme, uhazili, kompyuta na uchomeleaji vyuma.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Said Ntahondi, alitoa pongezi hizo wakati wa mkutano wa pili wa Baraza la Madiwani kupitia taarifa za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema kukamilika kwa chuo hicho kutasaidia vijana ambao wamemaliza elimu ya msingi na sekondari, kusomea kozi mbalimbali ambazo zitawawezesha kujiajiri wenye na kuondokana na umaskini.

"Kwa kweli, tunampongeza Rais John Pombe Magufuli kwa kutupatia fedha hizo zitakazotuwezesha kujenga chuo cha kiasasa katika eneo la Isikizya, hii inaonyesha kuwa anatupenda sana watu wa Uyui," alisifu.

Pia alisema Hospitali ya Wilaya imeanza kufanya kazi kwa kutoa huduma za matibabu ya wagonjwa wa nje.

Alisema hatua hiyo imefikiwa baada ya agizo la Mkuu wa Mkoa wa Tabora la kumtaka Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo kuanza utoaji wa huduma za awali katika majengo ambayo yamekamilika ili kuwapunguzia adha wananchi kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za matibabu.

Alisema kwamba kuanza utoaji wa huduma kwa wagonjwa wa nje(OPD) kumesaidia kupunguza usumbufu kwa wananchi wa wilaya hiyo kwa kupata huduma za matibabu.

Ntahondi alisema halmashauri imetenga Sh. milioni 60 kwa ajili ya ujenzi wa majengo katika shule saba za sekondari ili kupunguza mrundikano wa wanafunzi wa kidato cha kwanza.

Alisema sanjari na hilo, wanaomba Ofisi ya Kanda ya Udhibiti Ubora kuwasaidia ili Shule ya Sekondari ya Idete ipokee wanafunzi wa kidato cha tano mwaka huu.

Ntahondi alisema wanaendelea na maandalizi kwa ajili ya uanzishwaji kwa kidato cha tano kama watakubaliwa ili wilaya hiyo iwe na shule mbili za sekondari kwa ajili ya kidato cha tano na sita mbili. Kwa sasa wilaya hiyo ina shule moja ya Ndono.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Makubaliano ya TRA, ZRA yaondoe kero hizi

**BAADA** ya kero za muda mrefu za foleni ya malori na rushwa katika eneo la mpaka wa Tanzania na Zambia, hatimaye sasa zimeanza kuchukuliwa kama ufumbuzi wake.

Hatua zilizoanza kuchukuliwa ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Mamlaka ya Mapato Zambia (ZRA) kusaini makubaliano ya kubadilishana taarifa kwa njia ya mtandao lengo kuu ikiwa ni kuondoa kero ya foleni ya malori, kudhibiti biashara ya magendo ili kukusanya mapato stahiki na kukuza uchumi wa nchi hizo.

Makubaliano hayo yalisainiwa mwishoni mwa wiki na Kamishna Mkuu wa TRA, Dk. Edwin Mhede na Kamishna Mkuu wa ZRA, Kingsley Chanda.

Kusainiwa kwa mkataba huo ni utekelezaji wa maelekezo aliyoyatoa Rais John Magufuli Oktoba 5, mwaka jana wakati akiwa na Rais wa Zambia, Edgar Lungu, walipofungua kituo cha huduma za pamoja mpakani Tunduma.

Dk. Mhede alisema kuwa Desemba 13, mwaka jana walikutana na Kamishna Mkuu wa ZRA na kukubaliana kuwa kuna umuhimu wa kuboresha huduma, kutatua changamoto za kiforodha na kuimarisha uhusiano wa kibiashara katika nchi hizo mbili ili kuongeza ufanisi.

Alisema walichokubaliana ni pamoja na kurahisisha kuweka mfumo wa kubadilishana taarifa kwa njia ya mtandao, njia ambayo itawezesha nchi zote mbili kupata taarifa sahihi za mzigo inayosafirishwa na kuziwezesha kukusanya kodi kwa urahisi na ufanisi.

Alisema maboresho mengine ni kutatua changamoto ya mizigo kukaa muda mrefu mpakani na kukwamisha shughuli za biashara kurahisisha taratibu za kiforodha kwa kubadilishana taarifa ya mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam hadi inapovuka mpaka Nakonde kwa upande wa Zambia.

Naye Kamishna Chanda alisema malengo waliopanga yametimia, na kusema ushirikiano mkubwa ndio umesababisha kufanikiwa katika kuboresha mpaka huo ambao ni lango kubwa la nchi za kusini mwa Afrika ambazo ni wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Alisema Zambia itaendelea kuboresha na kutatua changamoto ambazo zilikuwa zikikwamisha magari kuchelewa kuvuka kwa kuboresha miundombinu ya barabara na kujenga sehemu kwa ajili ya kuegesha magari yatakayoondoa msongamano.

Kusainiwa kwa makubaliano haya bila shaka kutawezesha kuondoa kero hizo za muda mrefu. Kwa mfano, foleni ya mabari imekuwa ni ya muda mrefu katika eneo la mpaka wa nchi hizi mbili.

Lakini biashara ya magendo imekuwa na athari kubwa kwa kuwa pamoja na mambo mengine, imekuwa ikisababisha serikali za mataifa hayo kukosa kodi stahiki kwa maendeleo.

Ili kuhakikisha wkamba malengo haya yanafikiwa, itakuwa vyema kama watumishi wa kituo cha huduma za pamoja mpakani Tunduma wa nchi zote kufanyakazi kwa pamoja ikiwamo uadilifu, uzalendo na kuaminiana kwa maslahi ya nchi zote mbili.

Tunalisema na kulisisitiza hili kwa kuwa mchakato wa kupeana taarifa, unahitaji pande zote kuaminiana pamoja na watumishi kuwa waadilifu, vinginevyo foleni ya malori na vitendo vya magendo vitaendelea.

Huu ni wakati pia wa wafanyabiashara katika mpaka huo kurejea kwenye mstari kwa kuachana na maslahi binafsi na kuhakikisha wanaheshimu na kufuata sheria za nchi zao.

Tunasema hivyo kutokana na biashara ya magendo kuwa na mtandao unaowahusisha wafanyabiashara wa nchi zote mbili, hivyo kama wataviacha, bila shaka vitakoma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Walimu sayansi ni muhimu kwa Tanzania ya Viwanda

**UHABA** wa walimu wa masomo ya sayansi, ni moja ya changamoto, ambayo inaendelea kuzikabili shule za umma na kusababisha wanafunzi kutojifunza vya kutosha masomo hayo.

Hali hiyo inasababisha wanafunzi kutojifunza masomo hayo kwa uhakika na kujikuta wakiyakimbia, kutokana na kutokupata msingi mzuri wa masomo hayo kutokana na uhaba wa walimu.

Kutokana na hali hiyo, upo uwezekano kwa siku za baadaye kuwapo shida kwa kuwa ni kipindi ambacho nchi inaelekea kwenye uchumi wa kati kupitia viwanda, hivyo inaweza kukosa wataalamu wa kusimamia viwanda.

Elimu ikiboreshwa kupitia kuwaandaa walimu wa kutosha wa masomo ya sayansi, ina maana kwamba mchango wao ni mkubwa kufikia uchumi wa viwanda 2025, kwani watakuwapo wanataaluma walioandaliwa kwa ajili hiyo. Hivyo wakati umefika kwa Tanzania kuwa na walimu wa kutosha wa masomo hayo na ikiwezekana, wawe na mshahara mkubwa au posho za kutosha kutokana na ugumu wa masomo yenyewe.

Kwa vile serikali imeshasema kuwa imejipanga kuhakikisha inamaliza tatizo la upungufu wa walimu wa sayansi nchini kufikia mwaka 2020/2021, basi hilo lipewe kipaumbele ili kuhakikisha linatimia.

Nakumbuka aliyewahi kuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Joseph Kakunda, alisema kuna upungufu wa walimu 19,000 nchini.

Lakini akaweka wazi kuwa, ili kukabiliana na upungufu huo, serikali inaandaa utaratibu wa kuajiri walimu wa sayansi ili kuhakikisha tatizo hilo linaisha na kuwafanya wanafunzi wasome masomo yote.

Serikali imeshatangaza mwongozo mpya kuwa kuanzia masomo ya sayansi ni lazima kusomwa na wanafunzi wote wanaosoma elimu ya sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne.

Hiyo ni kwa mujibu wa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, katika moja ya hotuba zake kwa walimu wa elimu ya msingi.

Kwamba Sera ya Elimu iliyopo, wanafunzi wanaosoma elimu ya sekondari wanaweza kuchagua aina ya masomo watakayo wafikapo kidato cha tatu na kuacha mengine.

Lakini hivi sasa nchi imedhamiria kuingia kwenye uchumi wa kati kupitia ujenzi wa viwanda, hivyo suala la sayansi haliwezi kuepukwa kwa sababu ni wakati sasa wa kuwa na wataalamu wengi wa fani za sayansi watakaoweza kutosheleza mahitaji ya sekta ya viwanda.

Hatua hiyo itamlazimisha mwanafunzi kusoma kwa bidii, ili kuhakikisha anafaulu masomo hayo ingawa tatizo kubwa lililopo ni uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi, hali ambayo ni kikwazo. Katika mazingira hayo, baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakidai kwamba masomo hayo ni magumu na kusababisha wachague mengine na kumbe tatizo ni kukosa msingi tangu mwanzo.

Wana haki ya kudai hivyo, kwa sababu kinachochangia kuwapo kwa hali hiyo ni uhaba wa walimu, na wakati mwingine mwalimu, wanaweza kufundishwa topiki chache na tena bila vitendo.

Baadhi ya shule hazina maabara, hivyo kwa mazingira kama hayo, wanafunzi wanaweza kuendelea kuyakimbia masomo hayo kutokana na kutosoma kwa vitendo, hivyo lengo la serikali kukwama.

Ni uamuzi mzuri wa serikali kwamba kuanzia sasa wanafunzi wote wa elimu ya sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne, wasome masomo ya sayansi na kufanya mtihani wa masomo hayo, kisha baada ya matokeo ndipo wafanye uamuzi ama wa kuendelea nayo au la.

Hata hivyo, kwa hali ya sasa inawezekana wakaendelea kuyakimbia, kutokana na ukweli kwamba yana topiki nyingine halafu wakati mwingine wanasoma chache tu, hivyo kujikuta hawana uelewa na mambo mengi.

Hivyo juhudi za makusudi ziendelee kufanyika ili kuhakikisha shule zote za umma zinakuwa na walimu wa kutosha wa masomo hayo, lakini walimu wake wapewe kipaumbele katika maslahi ili wawe na moyo wa kufundisha.

Ili kwenda tunapotaka kuelekea, serikali hainabudi kuwekeza zaidi katika masomo ya sayansi kwa njia mbili. Kwanza kuwaandaa vizuri walimu wa sayansi ili wapatikane walio bora, ambao watakuwa na uwezo wa kutosha kuwafundisha wanafunzi na kuzalisha wenye uelewa.

Pili iandaliwe programu maalum ya kuwaandaa wanafunzi kusoma sayansi, kwa maana ya kuwaandalia mazingira bora ya kuyapenda masomo hayo.

Hayo yakifanyika, kwa kiasi fulani hali inaweza kubadilika na kupata wanafunzi wengi wanaopenda sayansi na kuandaliwa vyema kwa ajili ya kuwa wataalamu wa baadaye wa Tanzania ya viwanda.

## Bilioni 8/- kutumika kujenga soko Kibaha

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

HALMASHAURI ya Mji wa Kibaha, inatarajia kukamilisha ujenzi wa soko la kisasa unaotarajiwa kugharimu Sh. bilioni nane.

Hayo yalibainishwa juzi mjini Kibaha na Ofisa Uhusiano wa Halmashauri hiyo, Innocent Byarugaba, alipoongea na Nipashe ofisini kwake kuhusiana na miradi ya maendeleo inayotekelezwa.

Byarugaba alisema fedha za mradi huo kutoka serikali kuu zilitengwa katika mwaka wa fedha 2018/2019, akibainisha kuwa soko hilo linajengwa katika eneo la Kitovu cha Mji.

Alisema katika mradi huo, washirika wa maendeleo (UNCDF) wamechangia kiasi cha Sh. milioni 249.5 na hadi kufikia Desemba mwaka jana, Sh. bilioni mbili kutoka serikali kuu zilikuwa zimepokewa.

"Ujenzi wa soko hili kubwa la kisasa umekuja baada ya kuwa na soko la wakulima eneo la Loliondo ambalo bidhaa kubwa zinazopatikana huko zinatokana na kilimo na halitoshelezi mahitaji mengine ya wakazi zaidi ya 147,000 kwa sasa ukilinganisha na wakazi zaidi ya 128,000 liliposanifiwa," alisema.

Aliongeza kuwa kazi ya ujenzi huo ilianza Machi mwaka jana na ulitarajiwa kukamilika Desemba 30 mwaka jana, lakini kutokana na mvua, mkandarasi aliongezewa muda wa siku 59 zitakazofika ukomo Februari 27 mwaka huu.

Alisema kuwa baada ya kukamilika kwa mradi huo wa soko, watakuwa na chanzo kipya cha mapato kwa kuwa kunatarajiwa kuwapo maduka 43, ATM 12, migahawa, maegesho ya magari 165 na soko la jioni kwa wajasiriamali.

Inaelezwa kuwa mradi huo pia utasaidia uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo na vya kati na kutoa nafasi kwa wanawake kumiliki na kufanya biashara katika mazingira safi na salama.

Byarugaba alisema solo hilo litakapokamilika litatoa huduma kwa watu 834,956, sawa na kaya 196,422 za wakazi wa Mkoa wa Pwani na kwamba wananchi wengine 258,812 kutoka kata jirani za Wilaya ya Ubungo wanaotarajiwa kutumia soko hilo.

# Askari Polisi watatu wafa ajalini

**Na Erasto Mgeni, NJOMBE**

ASKARI watatu wa Jeshi la Polisi mkoani Njombe wamefariki dunia baada ya kutokea ajali iliyohusisha basi la kampuni ya Sharoon linalofanya safari zake Njombe - Arusha.

Basi hulo liligongana na gari la Polisi lililokuwa mbele yake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamis Issa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, majira ya jana alfajiri, na kusema basi hilo lenye namba namba T349 CXD liligonga gari la polisi lililokuwa mbele yake lenye namba PT 3734 Toyota Land Cruser na kusababisha vifo vitatu na majeruhi tisa.

Kamanda Issa aliwataja askari waliofariki ni namba H 4401 Mariharus Said Hamis, mkazi wa Lindi, H 6802 PC Michael Muhando mkazi wa Geita na H7486 PC Henry Athmani Soka, mkazi wa Arusha na Kilimanjaro.

Kamanda Issa alisema majeruhi wanaendelea na matibabu katika Hospitali ya Kibena na askari watatu wamefariki wakati wakipelekwa kwenye matibabu.

"Katika ajali hiyo majeruhi ambao walikuwa wamezidiwa zaidi ni watano, mmoja anayetambulika kwa jina la kijeshi namba H 1839 PC Dickson huyu amepata maumivu ya shingo na maumivu mengine mwilini, na amepewa rufani ya kwenda Muhimbili na hawezi kupanda gari labda usafiri wa ndege, hivyo mpaka sasa hivi tunafanya utaratibu askari huyu kusafirishwa kwa matibabu na taratibu zote za kumpeleka zimeshakamilika," alisema Kamanda Issa.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mji wa Njombe, Dk. Alto Damas Mtega, alisema walipokea majeruhi tisa na miili mitatu jana asubuhi.

"Tumepata majeruhi ambao wametokana na ajali na wote walikuwa ni askari polisi. Walikuwa wanatoka kituoni wanaelekea kazini, wawili hali zao sio nzuri sana watahitaji kupewa rufani," alisema Mtega.

Majeruhi wa ajali hiyo, Mustapha Said, alisema,

"Tuliona tu gari imepigwa kwa nyuma na watu wote walikuwa wamesharuka, kwa hiyo sikuweza kutambua kitu chochote."



Mkazi wa jijini Dar es Salaam, akisafirisha vipande vya magodoro vilivyosheheni kwenye guta lake, eneo la Ubungo Mataa jana, na kusababisha asione nyuma, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Bunge laona ukakasi 'force account'

**Na Godfrey Mushi, DODOMA**

BUNGE limeitaka serikali kutathmini upya uamuzi wake wa kutumia nguvu kazi ya mafundi jamii katika kutekeleza miradi mingi kwa gharama nafuu, huku likitoa tahadhari kusahauliwa umuhimu wa kukuza uwezo wa kitaalamu na kiutawala kwa kampuni za kizalendo.

Limesema umuhimu huo upo kwa sababu ya kampuni hizo hutoa ajira kwa vijana na kulipa kodi mbalimbali za serikali.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mahamoud Mgimwa, aliwasilisha hoja hiyo jana bungeni jijini Dodoma, aliposoma taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na kamati yake kwa kipindi cha kuanzia Januari 2019 hadi Januari mwaka huu.

Akizungumzia zaidi suala hilo, Mgimwa alisema utaratibu wa kutumia nguvu kazi hiyo ya mafundi jamii kwenye miradi ya maji, umeonyesha mafanikio makubwa kwa kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma na kuharakisha kukamilika kwa miradi ya maji iliyokuwa inatekelezwa kwa muda mrefu bila kukamilika.

"Kamati inaliomba Bunge liitake serikali kutathmini upya uamuzi wake wa kutumia 'force account' (nguvu kazi ya mafundi jamii) ili kutekeleza miradi mingi kwa gharama nafuu, bila kusahau umuhimu wa kukuza uwezo wa kitaalamu na kiutawala kwa kampuni za kizalendo ambazo hutoa ajira kwa vijana na kodi mbalimbali za serikali," alisema.

Pamoja na mambo mengine, kamati hiyo imetaka katika mpango wa maendeleo wa taifa wa miaka mitano, serikali ijielekeze kwanza kufungamanisha shughuli za kilimo na ukuaji wa uchumi hususani kwenye uchumi wa viwanda.

Alisema wanapendekeza Bunge liazimie kuanzia mwaka wa fedha 2020/21 na katika mpango wa maendeleo wa taifa wa miaka mitano wa mwaka 2021/22- 2026/27, sekta ya kilimo iwe kipaumbele cha kwanza serikali.

Alisema kilimo ndiyo kila kitu kwa maendeleo ya nchi kutokana na ukweli kwamba kinategemewa na asilimia 80 ya Watanzania.

Katika taarifa yake, Mgimwa alisema kilimo kinachangia asilimia 30 ya pato la taifa, kinachangia asilimia 95 ya chakula kinachotumika nchini na kinachangia zaidi ya asilimia 30 ya mauzo ya nje ya nchi na asilimia 70 ya malighafi ya viwanda.

"Na kwa kuwa ni takribani miaka 60 sasa, serikali inapanga, kutekeleza na kusimamia sera, mikakati, mipango na mbinu mbalimbali za kukwamua kilimo, mchango wa sekta ya kilimo kwenye uchumi bado ni mdogo kutokana na vikwazo vingi ikiwa ni pamoja na bajeti ndogo," alisema.

Katika sekta ya mifugo, Mgimwa alisema serikali imefanikiwa kutoa elimu, kupunguza migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi na kuhamasisha wafugaji kufuga kibiashara.

"Juhudi hizi zimesababisha kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya mifugo, ambapo maziwa yameongezeka toka lita bilioni 1.6 mwaka 2009 hadi bilioni 2.06 mwaka 2015, uzalishaji wa nyama umeongezeka toka tani 452,230 mwaka 2009 hadi tani 597,757 mwaka 2015 na uzalishaji wa ngozi umeongezeka toka ngozi milioni 5.6 mwaka 2009 hadi ngozi milioni 6.45 mwaka 2014," alisema.

# Mwamposa ashukiwa kila kona

INATOKA UK 2

tumia vitabu vitakatifu tafadhali tusivitumie tunavyotaka. Zamani kulikuwa na utaratibu wa kusajili dini au dhehebu, naomba utaratibu huo urudi ili mafundisho yao yakaguliwe na yaangaliwe," alisema.

Aidha, alitoa wito kwa viongozi wa dini kukutana ikiwamo serikali kushirikiana na kwamba wako wanamwagia watu soda kichwani na kwamba si matumizi sahihi ya neno la Mungu.

Aidha, alilitaka Jeshi la Polisi kuwachukulia hatua viongozi wa dini wanaofanya mambo ambayo ni ya kilaghai na kwamba watu 20 hawawezi kupotea kwa uzembe.

"Wananchi msome majira na nyakati tunazoishi. Kule Zambia walinyeshwa jiki kwa jina la upako, Afrika Kusini mtu alikufa akiwa ameshika simu, Uganda Kibwetere aliangamiza watu kwa mafundisho yasiyo na msingi wa neno la Mungu. Mungu hajatuahidi utajiri pasipo kufanya kazi.

"Tangu alivyotuumba alimwambia Adam akalime bustani, angeliweza kumwambia wewe kula, kulala, kuamka na kuimba lakini alimwambia akalime na alimwambia atakula kwa jasho. Kuja kwa Yesu hakujabatilisha hayo.

"Yesu hajaleta magari kwa watu wasiteseke, hao wanaolekeza watu kuwa magari yao yamezuiliwa baharini, gari haifiki baharini kabla haijalipiwa Japan, tusitumie ujinga wa watu kuwa mtaji wetu," alisisitiza.

Sambamba na hilo, alisema: "Wanaotumia vitu kama maji, soda, mafuta, chumvi na jiki, naomba wakaguliwe upya na kama ni maduka wakafungue lakini wasichezee maisha ya watu wasio na akili na ufahamu wa kutosha," alisema. Naye Kiongozi wa Bazara la Waislamu Mkoa wa Kilimanjaro, Abdullah Mfaume, alisema wampokea kwa masikitiko makubwa na kwamba ni tukio linalotoa fundisho kwa kuwa mwanadamu ana utaratibu wa kumtafuta Mungu.

"Jamii haina budi kuwa makini na mafundisho ya dini yasiyo sahihi na yanayotolewa na watu wasio sahihi. Tukio hili liwe fundisho kwetu," alisema.

**DC AGEUGA MHUBIRI**

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Ole Sabaya, akizungumza kwa niaba ya wakuu wa wilaya, alisema maandiko ya Mungu hayajabadilika na Mungu alisema watu watafute ufalme ya Mungu na si maghorofa wala magari.



"Hakuwahi kusema tafuteni maghorofa, nyumba, magari, utajiri. Injili hiyo ndiyo imesababisha Kibwetere akachomea waumini wetu ndani ya majumba. Neno pia linasema nanyi mtaijua kweli nayo kweli itawaweka huru," alisma.

Aidha, alisema itafika mahali serikali itasema imetosha na kwamba haijafikia sehemu kuondoa maisha ya watu kwa jina la Mungu.

"Mimi nakwenda kwa mganga ananiambia njoo na kuku mweupe halafu nakwenda kwa mchungaji ananiambia njoo na fruto. Hapa utajua nani mganga na mchungaji? Maandiko yanasema mtawatambua kwa matendo yao, hakuna matendo yatakayofanya tuwatambue watu zaidi ya kufa kabla ya muda wao," alibainisha.

"Ni kweli wachungaji wananchi wetu wanateska sana, wana mizigo mizito, matatizo ya ndoa, vikoba, madeni lakini tusigeuze tabu zao kama mtaji wa kuwasaidia tendeni kama mnavyopaswa kutendewa yakitokea hutakuwa na haja ya kukimbia bali utashiriki kuwakomboa," alisema.

**MWENYEKITI CCM**

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, alisema kuwa waamini vitu vitakatifu vya Mungu havimwagwi na kwamba waliokufa walikwenda kukanyaga mafuta yaliyosadikiwa kuwa ni matakatifu na kwamba yangekuwa matakatifu wasingekufa.

"Mahangaiko yetu yasituingize kwenye mambo yasiyotusaidia. Makanisa yaliyopo ni vizuri tukarudi katika historia na kwamba mkoani hapa hapakuwa na makanisa kama hayo," alisema.

"Ni vizuri yakaanza kufuatiliwa, uhalali, mafundisho na kweli ndiyo mafundisho yanayowapeleka kwa Mungu, sote tunataka kwenda mbinguni kwa kuomba na kujiombea, kuna mtu kawaaminisha watapata magari na hawajapata badala yake wamekufa, hakuna utajiri bila kufanyakazi, tufanye kazi kwa bidii na tusali kwa imani uliyorithi na unayoona inafaa," alisema Boisafi.

Aidha, aliomba serikali kufanya uchunguzi wa kina wa makanisa hayo juu ya uhalali wao, na kwamba ni vyma kutojiingiza kwenye mitego.

**VIONGOZI WA SERIKALI**

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alizungumza na majeruhi ambaye alitokea Kibosho kwa ajili ya kuwaombea watoto wakapatane na kuwaomba kokote waliko wapatane.

"Bado tupo tuna nguvu na bado tunampenda Mungu, tunamwamini na kumpenda Mungu, bado tunamtumainia Mungu kwamba nguvu yake inatosha na amani yake tukiishika kikamilifu inatosha," alisema.

Aidha, alisema Rais John Magufuli, alimwagiza washughuliki upungufu uliojitokeza na si kufunga shughuli za imani na kwamba kwa ujumbe huo hazitafungwa.

**JPM ATUMA SALAMU**

RAIS John Magufuli ametaka watu waendelee kuliombea taifa ili shetani aliepushe na mabalaa yakiwamo ajali.

Akizungumza jana Ikulu jijini Dar es Salaam wakati akiwaapisha viongozi mbalimbali aliowateua hivi karibuni, Rais Magufuli aliwataka watu waendelee kumuomba Mungu.

"Tuendelee kumwomba Mungu shetani atuepushe na balaa hili na tuwaombee majeruhi watano wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) wapone haraka, wapo wanajeshi 10 walikuwa kwenye mazoezi ya jeshi wamefariki. Vifo vilivyotokea Moshi na mkoani Lindi.

"Mungu ni mwema analipenda taifa nawashukuru viongozi wa dini kwa kuweka taifa mikononi mwa Mungu," alisema.

***Imeandikwa na Salome Kitomari, Romana Mallya (Dar) na Mary Mosha (Moshi) Salome Kitomari***

## Wawekezaji waomba kuja kuchakata bangi

INATOKA UK 3

mrefu, lakini basi namuomba waziri wakati wowote kama watapitisha iwe mapema kabla bei haijaporomoka," alisema.

Wakati Kishimba anachangia mjadala huo, Mbunge wa Geita Vijijini (CCM), Joseph Musukuma alisimama na kumpa taarifa akisema: "Kikawaida Bunge linapotunga sheria kinachofuata ni kanuni tu, sasa nilikuwa nafikiria Mheshimiwa Waziri angetuambia kanuni ziko tayari ili tuanze kulima kwa sababu bangi itaporomoka bei."

Baada ya michango hiyo ya wabunge, Spika wa Bunge, Job Ndugai alisema: "Niwa assue this is not a joke (niwahakikishie kwamba hili sio jambo la utani), anachochangia (Kishimba)... nilikuwa Canada majuzi hapa kwenye mkutano wa ma Spika wa Common Wealth (Jumuiya ya Madola) duniani. Ni big business in Canada (Ni biashara kubwa). Kwa hiyo anazungumza kitu cha msingi sana wala sio utani.

"Tena linaweza kuwa ni zao kubwa la biashara linaoweza kundoka kuliko mazao mengi tu kabisa, likafanya mapinduzi makubwa sana ya kipato. Kwa hiyo anachokizungumza Mheshimiwa Kishimba hazungumzi bangi itumike vile ambavyo tunavyofahamu inatumika hapa nchini.

"Tunazungumzia habari ya kilimo, moderated, monitored na taratibu zote halafu wanapelekewa wote wanaohitaji kwa ajili ya kutengeneza dawa za wanyama na binadamu."

# Magufuli ataja kilichowabeba wateule wapya aliowaapisha

INATOKA UK 3

Mahakama ya Rufani, hivyo anaamini katika nafasi mpya ya Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, atasaidia kwa sababu ni mtenda haki na msomi.

"Wakili Julius Bundala (Kamishna mpya wa Tume ya Utumishi wa Mahakama) amefanya kazi vizuri akiwa wakili, atatusaidia na Jenoveva Kato (Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Mahakama), ana umri mkubwa, amekuwa hakimu, akawa wakili na alisimamia kitu... ana busara atatusaidia, tumemchukua ili tuwe na jinsia zote," alisema.

Rais Magufuli akimwelezea Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Christopher Kadio, alisema aliwahi kufanya kazi Oryx na aliteuliwa kuwa Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza na ilipotokea ajali ya Nansio, fedha zilizochangwa, alisimamia ikajengwa hospitali ya wilaya na sasa alikuwa anajenga kituo cha kupokea abiria.

"Tumefikiri tumpeleke Wizara ya Mambo ya Ndani ambayo ina mapepo akayaombee, wakashirikiane na George Simbachawene (Waziri wa wizara hiyo), lazima tupeleke pale watu ambao wanajitoa," alisema.

Akimwelezea Katibu Mkuu wa Wizara wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas (alikuwa Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo), Rais Magufuli alisema amefanya kazi vizuri kama Msemaji wa Serikali.

"Hakuchoka, ameisemea vizuri serikali, alifuata miongozo vizuri ya Dk. Harrison Mwakyembe (Waziri wa Habari) na viongozi wengine, tungependa aendee kuwa msemaji wa serikali, lakini ikifika mahali mtu akitakiwa kupandishwa cheo, usimnyime.

"Tumemteua awe Katibu Mkuu na kwa sasa ataendelea kuwa msemaji wa serikali mpaka tutakapopata mwingine, atakuwa anasema akiwa mkubwa zaidi," alisema.

Rais Magufuli alisema Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Zena Said, akiwa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) aliwabana makandarasi na walimchukia.

Kuhusu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Riziki Shemdoe, Rais Magufuli alisema alipokuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafinga, aliongeza ukusanyaji wa mapato.

Akimwelezea Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Mary Makondo, (alikuwa Kamishna wa Ardhi wizarani hapo), Rais Magufuli alisema alikuwa hapendwi kwa sababu ya msimamo yake.

"Kwa sababu hiyo, tukasema huyu huyu ambaye hawampendi, abaki palepale ili wale ambao hawampendi waumie vizuri, nilikuwa nakuja wakati mwingine naambiwa hafai, ukienda kuchungulia unakuta ndiye anayefaa zaidi.

"Wamejitahidi kumwandikia kwenye ujumbe mfupi wa maelezo kumchafua lakini bado alisimama, walitaka pia kumchonganisha na mume wake, nampongeza mume wake alisimama imara, nimempa hapohapo wizara hii, ina 'madudu' mengi," alisema.

Kuhusu Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Stephen Mashauri, Rais alisema alifanya kazi Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) na baadaye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ambako kote alifanya vizuri.

Akimwelezea Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Emmanuel Tutuba, Rais Magufuli alisema alifanya kazi Wizara ya Fedha na Mipango. Alisema Mamlaka ya Mapato (TRA) miaka ya nyuma walipokuwa wakiziweka fedha kwenye akaunti ya muda maalum, alizisimamia kwa maslahi ya taifa.

Alisema Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga, Judica Omari, alifanya kazi sehemu mbalimbali ikiwamo SADC, Wizara ya Fedha na aliteuliwa kuwa Katibu Tawala Msaidizi Njombe na kwamba ni 'mchaga' ambaye anazuia fedha kuibiwa.

Kuhusu Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Leonard Masanya, Rais alisema alikuwa miongoni mwa watu waliokuwa kwenye timu iliyotumwa kwenda Ethiopia kushughulikia mradi wa Stigler's Gorge, ambao alisimamia vizuri mazungumzo upande wa Tanzania.

Rais Magufuli alisema Msajili Mkuu wa Mahakama, Wilbert Chuma, katika majina mengi yaliyokwenda kwake alimwona huyo ndiye chuma kwelikweli.

"Msajili wa Mahakama Kuu, Shamira Sarwat, alichukia mno, wapo wanaomwangalia hivi sasa, wanatamani wasingemwona," alisema. Rais Magufuli aliwataka wote walioapishwa wakatangulize maslahi ya nchi mbele na kuchapa kazi kwa manufaa ya sasa na baadaye.

"Nina uhakika mtapata ushirikiano mzuri kwa makatibu wakuu, mawaziri, majaji na wakuu wa mikoa na kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho kinatekeleza ilani," alisema. Kabla ya kuapisha Brigedia Jenerali Mzee na Kamishna wa Magereza, Masunga, kutokana na kutakiwa kutumikia majeshi mengine, walipewa muda wa kwenda kubadilisha sare za jeshi walizokuwa wamezifaa, ndipo Rais Magufuli alipowavika vyeo vipya na kuwaapisha kushika nyadhifa hizo mpya.

# NMB yaiahidi makubwa serikali

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imesema itahakikisha inaendelea na kuunga mkono juhudi za maendeleo ya serikali ya awamu ya tano ili kuifikia malengo yaliyokusudiwa ya kuwahudumia wananchi.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Idara ya huduma za Serikali wa Benki ya NMB, Vicky Bishubo, alipokuwa akiwasilisha taarifa ya benki hiyo kwenye mkutano wa utoaji taarifa ya mafanikio ya miaka minne ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) uliofanyika jijini Dodoma.

"Benki ya NMB ni mali ya wananchi na serikali hivyo tunafurahi tunapoona kila upande unaendelea kuiunga mkono katika mafanikio yaliyopatikana hivyo tunawaomba mwendelee kutuunga mkono kwa kufungua akaunti na kuweka fedha kwetu," alisema.

Bishubo alisema benki hiyo itahakikisha inaendelea kuunga mkono juhudi za serikali ili kufikia malengo ya kuwahudumia wananchi wake katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema benki hiyo inaendelea kufungua matawi na kuweka mashine za ATM katika maneo mbalimbali ili kuhakikisha wananchi wanafikiwa na huduma za kibenki karibu na maaneo yao.

Alibainisha kuwa uwapo wa benki hiyo katika kila wilaya hapa nchini imesaidia pia kurahisisha maendeleo ya wananchi kwa kupata huduma za kifedha karibu kwenye maeneo yao.

Aliongeza pia benki hiyo imeweka mawakala wengi nchini kwa lengo la kuwasogezea wananchi huduma za kifedha katika maeneo yao.

Aidha, alisema benki hiyo imekuwa ni sehemu ya mafanikio ya Ofisi ya Tamisemi kutokana na kufanyakazi kwa karibu na halmashauri zote nchini.

Kwa upande wake, Waziri Selemani Jafo, alitaja baadhi ya mafanikio ya ofisi hiyo kuwa ni ujenzi wa vituo vya afya 97 zimejengwa na vingine kukarabatiwa na serikali katika kipindi hicho cha miaka minne ya mafanikio.

Jafo alitaja mafanikio mengine kwenye sekta ya elimu kuwa ni ongezeko la ufaulu wa wanafunzi, ujenzi wa vyumba vya madarasa na ukarabati wa majengo ya shule kongwe hapa.

Waziri huyo aliishukuru benki hiyo kwa kuendelea kushirikiana na serikali kwa kutoa misaada mbalimbali kwenye sekta ya afya na elimu nchini.

# Mlipuko magonjwa mifugo waitesa Pwani

**Na Khadija Kalili, PWANI**

MWENYEKITI wa Chama cha Wafugaji Mkoa wa Pwani, John Kawawa Simba, amesema mifugo yao imekumbwa na mlipuko wa magonjwa ya upele na ukurutu ambao unaisumbua, hivyo kutishia ustawi wa mifugo mkoani humo.

Akizungumza na Nipashe, Simba alisema ugonjwa wa mapele ngozi umekuwa ukiathiri ng'ombe kwa kusababisha ngozi kuvimba na kuwa na mapele makubwa ambayo mengine hutengeneza majipu, ng'ombe wanapoteza hamu ya kula na zinakonda sana, hali ambayo inashusha thamani ya mifugo wanapoenda kuuzwa mnadani. Aidha, wakichinjwa ngozi zao hazina ubora unaotakiwa katika kwenye viwanda vya ngozi.

"Hii ni changamoto kubwa ambayo tunaipitia kwa sasa huku kukiwa na uhaba wa maofisa mifugo kwani kwa sasa maofisa hao wanaishia katika ngazi ya kata, huku tatizo lilikiendelea kukua na kuleta hasara kubwa kwa wafugaji hasa wanaoishi vijijini ambako hakuna maofisa mifugo wa kutoa huduma kabisa," alisema Simba.

Kadhalika, anayataja baadhi ya maeneo yenye wafugaji ambayo yamekumbwa na ugonjwa wa mapele ngozi kuwa ni Vigwaza, Chalinze na Bagamoyo mkoani Pwani.

"Mbali ya kuumwa mapele ngozi na ukurutu pia mifugo hii inasumbuliwa na ugonjwa wa homa ya mapafu ambao husababisha homa kali, ng'ombe anashindwa kupumua na hatimaye kufa, nyama ya ng'ombe mwenye ugonjwa wa homa ya mapafu huwa haina ladha kwa mlaji," alisema Simba.

"Hivi sasa ugonjwa wa homa ya mapafu ya ng'ombe umekuwa tishio kubwa kwa sababu watoa huduma ambao ni maofisa mifugo ni wachache na wanaishia kwenye ngazi ya kata huko vijijini ndani hawawezi kufika, hivyo tunaiomba serikali iangalie kwa jicho la tatu ili kunusuru hii mifugo yetu japo tunaishukuru kwa kutupa madawa ya kuogesha mifugo," alisema Simba.

Ofisa Mifugo wa Halmashauri ya Chalinze, Hamza Chingoma, alithibitisha kuwapo kwa tatizo hilo katika maeneo yaliyotajwa na mwenyekiti wa wafugaji, huku akisema wanajitahidi kupambana na magonjwa hayo.

"Hivi sasa maofisa mifugo tulionao wanajitahidi kupambana kwa kutoa chanjo na tiba dhidi ya ugonjwa wa mapafu ya ng'ombe na magonjwa mengine," alisema.

"Nakiri kuwa tunakabiliwa na uhaba wa wataalamu wa mifugo ambapo nao umekuwa ni changamoto kubwa huku akiomba serikali itoe ajira kwa maofisa mifugo kwani walioajiriwa kwa sasa ni wachache ambao hawakidhi haja katika kutoa huduma kwa mifugo," alisema na kuongeza:

"Serikali iajiri maofisa mifugo wengine kwani wanahitajika maana hawa tulio nao ni wachache sana; kwa sasa tunao 24 tu huku kukiwa na vijiji 74 idadi yao haikidhi haja ya kutoa huduma stahiki na miongoni mwao wapo ambao wanastaafu na wanaokaribia kustaafu."

Aidha akizungumza kwa njia ya simu na Nipashe kutoka Makao Makuu ya nchi Jijini Dodoma Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Tanzania, Prof. Hezron Nonga, alisema sababu kuu ni msimu wa hali ya mvua zinazoendelea kunyesha nchini kote kwa sasa.

"Kwa mujibu wa takwimu zetu, maeneo mengi kwa sasa nchini yameathirika na ugonjwa wa mapele ngozi, huku akisema kuwa ugonjwa huu ni wa msimu na ambao unasababishwa na virusi vinavyoitwa lumpy skin disease virus (LSDV) na kusambazwa na wadudu kama inzi, kugusana na mnyama mwenye maambukizi, vyakula, maji na vifaa vya shambani vyenye maambukizi alisema profesa.

Prof. Nonga alisema njia kuu ya kuzuia ugonjwa wa mapele ngozi na homa ya mapafu ya ng'ombe ni chanjo kwani kinga ni bora zaidi kuliko tiba. Suala la chanjo kwa mifugo kwa sasa ni ajenda ya kitaifa ili kuhakikisha kwamba mifugo yote inapata chanjo dhidi ya magonjwa ya kipaumbele yakiwemo magonjwa ya mapele ngozi na homa ya mapafu ya ng'ombe.



Balozi wa Uingereza nchini, Sarah Cooke (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Bia Serengeti (SBL), Mark Ocitti, wakionja whisky aina ya John Walker Blue Label, katika hafla maalum ya 'Whisky Tasting' iliyoratibiwa na SBL, kwenye makazi ya balozi huyo jijini Dar es Salaam juzi, ikilenga kuwapa nafasi wateja na wadau wengine kuonja ladha ya vinywaji vikali vinavyosambazwa na kampuni hiyo, ikiwamo Johnnie Walker, inayotimiza miaka 200 tangu kuanzishwa kwake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mil. 277/- kutetea haki za binadamu

**Na Beatrice Shayo**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), umesaini mkataba wenye thamani ya Dola za Kimarekani 120,000 (sawa na Sh. milioni 277) kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao ikiwamo kutetea haki za binadamu.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Mratibu wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, alisema wamesaini makubaliano na tuzo ndogo na Chama cha Wanasheria Marekani (ABA) kupitia mfuko wake wa HakiElimu kwa ajili ya kutekeleza mradi wa miaka miwili.

Alisema kwa mujibu wa sheria walizowekewa kabla ya kuanza kuzitumia fedha hizo wanatakiwa kutoa taarifa.

Alisema fedha hizo zitaanza kutumia kuanzia Februari 1, mwaka huu na ukomo wake utakuwa ni Julai 31 mwaka 2021.

"Wanufaika wakuu wa mradi huu ni watetezi wa haki za binadamu ikiwamo mashirika yanayotetea haki za binadamu, wanasheria na waandishi wa habari wa habari," alisema Olengurumwa.

Alisema mradi huo umelenga kuongeza utetezi wa uhuru wa kujieleza kama inavyoelezwa na ibara ya 18 ya katiba ya nchi mwaka 1977 na uhuru wa kujumuika, haki na majukumu ya watetezi wa haki za binadamu nchini Tanzania.

"Mradi huu unatarajiwa kutekelezwa kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na utafiti na utunzaji wa taarifa na nyaraka, utetezi kwa njia ya mahakama pamoja na mazungumzo ya wadau na taasisi muhimu za serikali na zisizo za serikali," alisema.

Olengurumwa alisema wanawakaribisha wawekezaji wengine kuwasaidia ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Naye Mkuu wa Idara ya Ulinzi na Usalama kwa Watetezi wa Haki za Binadamu, Deogratias Bwire, alisema bado wana uhitaji mkubwa wa kuwapo kwa majadiliano mbalimbali baina ya tasnia ya habari na ufahamu wa utekelezaji wa sheria mbalimbali za habari zilizowekwa kwa kuwa bado kuna tatizo la uelewa.

# Barabara Mtwara-Newala-Masasi kukamilika 2020/21

SERIKALI imesema ujenzi wa barabara ya Mtwara-Newala-Masasi kwa kiwango cha lami kwenye kilometa 160 zilizobaki pamoja na daraja la Mwiti utaanza katika mwaka wa fedha 2020/21.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota.

Katika swali lake, Chikota alisema ujenzi wa barabara ya Mtwara – Newala – Masasi yenye urefu wa kilometa 210 umeanza kwa kiwango cha lami kutoka Mtwara hadi Mnivata yenye kilometa 50.

"Je, serikali ina mpango gani kwa kilometa 160 zilizobaki?" Alihoji.

Kwandikwa alisema upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara yote ya Mtwara – Nanyamba – Tandahimba – Newala – Masasi yenye kilometa 210 pamoja na daraja la Mwiti ulikamilika mwaka 2015.

"Mpango wa serikali ni kujenga barabara yote kwa kiwango cha lami kwa awamu," alisema.

Alieleza kuwa awamu ya kwanza inahusisha sehemu ya Mtwara – Mnivata yenye urefu wa kilometa 50 ambayo utekelezaji wake hadi kufikia Desemba, 2019 ulikuwa asilimia 76.

"Jumla ya Sh. bilioni 3.40 zimetengwa katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alisema katika bajeti ya mwaka 2019/20 na ujenzi wa barabara umeishia Mnivata na kwamba Mnivata hadi Nanyamba ni kilometa 20.

"Na kwa kuwa mkandarasi yupo pale kwanini bila kuathiri taratibu za manunuzi kwanini mkandarasi aliyepo asijenge kwa kiwango cha lami hadi Nanyamba mjini, lakini barabara Mtwara-Nanyamba-Masasi kuna barabara pacha ambayo ni ya ulinzi inakwenda hadi Michenjele, serikali ina mpango gani wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami?" alihoji.

Akijibu, Kwandikwa alimwomba mbunge kuvuta subira kwa kuwa serikali imedhamiria kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

"Zipo taratibu za manunuzi zinafuatwa mkandarasi kama atakuwa na sifa basi ataomba ili aweze kukamilisha kipande hicho," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema baada ya kukamilisha barabara inayojengwa sasa, watajenga barabara ya hiyo pacha ya kiulinzi.

# Serikali kuendelea kuvutia wawekezaji

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, ameliambia Bunge kuwa serikali itaendelea kuvutia uwekezaji katika maeneo yote yenye rasilimali ikiwamo jasi inayopatikana katika kata za Bendera na Makanya wilayani Same.

Kairuki alitoa kauli hiyo jana Bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Same Mashariki (Chadema), Naghenjwa Kaboyoka.

Katika swali lake, Kaboyoka alisema kata za Bendera na Makanya zina jasi nyingi na jasi inaweza kutoa malighafi kutengenezea 'gypsum boards', mabomba ya maji machafu, saruji, POP na mbolea,

Alihoji serikali ina mpango gani wa kusaidia kupatikana kwa mwekezaji ili aanzishe viwanda hivyo katika maeneo hayo wilayani Same.

Akijibu Waziri Kairuki alisema serikali itaendelea kuvutia uwekezaji katika maeneo yote yenye rasilimali ikiwamo jasi.

Aliupongeza uongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro na Wilaya ya Same kwa kutenga eneo katika Kata ya Makanya kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha saruji na kuingizwa katika Mwongozo wa Uwekezaji wa Mkoa wa Kilimanjaro.

"Hatua za kutafuta wawekezaji zinaendelea," alisema Waziri Kairuki.

Alibainisha kuwa azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kujenga uchumi wa kati unaoongozwa na sekta ya viwanda ifikapo mwaka 2025.

"Viwanda vinavyotumia rasilimali zinazopatikana nchini na kuzalisha bidhaa zinazotumika kwa wingi vimepewa kipaumbele, nchi kwa sasa imeweza kuzalisha baadhi ya bidhaa zinazotosheleza soko la ndani na ziada kuuza nje ya nchi zikiwamo bidhaa zinazotokana na malighafi ya jasi," alisema.

Kairuki alisema lengo la serikali ni kuongeza uzalishaji wa ndani na kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje katika maeneo yote yenye rasilimali zinazoipa Tanzania faida ya ushindani itaendelea kuvutia wawekezaji.

" Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zingine kama vile Kituo cha Uwekezaji Tanzania, Mamlaka ya EPZ, Tume ya Madini na wadau wengine tutaendelea kushirikiana kuzitangaza fursa za uwekezaji za Wilaya ya Same ili kuvutia na kutekeleza uwekezaji katika jasi iliyoko wilayani Same," alisema.

Alizitaka wizara, taasisi za serikali na mamlaka za serikali za mitaa kuendelea kusimamia mikakati ya kuboresha mazingira ya uwekezaji katika maeneo yao ikiwamo kuainisha na kuyapembua kiyakinifu maeneo yote yenye rasilimali.

"Pia kuyatenga na kuyarasimisha kwa ajili ya uwekezaji ili kupunguza migogoro isiyo ya lazima na wawekezaji ili kufikia dhamira ya serikali kufikia uchumi wa kati wa kipato cha kati kufikia mwaka 2025," alisema.



Mabalozi mbalimbali wastaafu wakifuatilia mkutano wa kumi na nane (18) wa Bunge la 11 kikao cha tano (5) kinachoendelea bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Ataka serikali kumalizia ujenzi maboma ya maabara

MBUNGE wa Lushoto (CCM), Shabani Shekilindi, ameitaka serikali kumalizia ujenzi wa maboma ya maabara yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Akiuliza swali bungeni jana, alihoji serikali ina mpango gani kumaliza maboma hayo.

"Wananchi wa Wilaya ya Lushoto wamejitahidi kujenga maboma mengi ya maabara mpaka sasa serikali haijawaunga mkono. Je, serikali ina mpango gani wa kumalizia maboma haya?" Alihoji.

Akijibu, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, alisema maabara 138 zinaendelea kujengwa kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto na nguvu za wananchi.

"Serikali kwa kushirikisha nguvu za wananchi imekamilisha ujenzi wa vyumba vya maabara 13 katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto na katika Mwaka wa Fedha 2019/20," alisema.

Alisisitiza kuwa halmashauri inaendelea na hatua za mwisho za ukamilishaji wa maabara katika shule za sekondari za Mlongwema, Kwemalamba, Lukozi, Ngwelo na Shume kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R).

Katika swali la msingi, Mbunge wa Kondoa Mjini (CCM), Edwin Sannda, alisema maboma mengi ya maabara kwenye shule za sekondari za kata nchini hayajakamilika.

"Hata pale yanapokamilika hakuna vifaa vya maabara, na tunahitaji sana wanasayansi kuelekea uchumi wa viwanda. Je, serikali ina mkakati gani wa kukamalisha maabara haya na ni lini yatakamilika?" Alihoji.

Alihoji ni lini vifaa vitapelekwa katika maabara zilizokamilika.

Waitara alisema serikali kwa kushirikisha nguvu za wananchi na washirika wa maendeleo imekamilisha ujenzi wa maabara 5,801 katika shule za sekondari nchini.

Aidha, alisema serikali inaendelea na ukamilishaji wa vyumba vya maabara kupitia ruzuku ya Serikali Kuu na mapato ya ndani kwa kushirikisha nguvu za wananchi.

"Vilevile, katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Halmashauri ya Mji Kondoa, imeidhinishiwa jumla ya Sh. milioni nane kwa ajili ya ukamilishaji wa maabara katika Shule ya Sekondari Bicha," alisema.

Alieleza kuwa serikali imenunua na kusambaza vifaa vya maabara vyenye thamani ya Sh. bilioni 19.13 katika shule 2,948 za sekondari zilizokamilisha ujenzi wa maabara.

"Serikali kwa kushirikisha na wananchi na wadau wa maendeleo itaendelea kuboresha maabara za masomo ya sayansi ili ufundishaji wa masomo hayo ufanyike kwa vitendo badala ya nadharia," alisema.

## Wadau madini wapewa somo

**Na Allan Isack, SIMANJIRO**

WADAU wa madini ya Tanzanite wa Mji Mdogo wa Mirerani, Simanjiro mkoani Manyara, wametakiwa kuchangamkia fursa ya madini hayo kwa kuwa serikali imeondoa kodi zilizokuwa zikilalamikiwa.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, aliyasema hayo jana wakati akizindua soko na mnada wa madini ndani ya ukuta unaozunguka migodi ya madini ya Tanzanite.

Chaula alisema baada ya wadau wa madini kulalamikia kodi ya asilimia tano ya zuio na asilimia 18 ya ongezeko la thamani, aliwataka wadau kuchangamkie fursa hiyo.

Alisema serikali ina mpango na sekta ya madini ili iwe miungoni mwa sekta zinazochangia kwa wingi pato la taifa.

"Changamkieni fursa hizi za uuzaji na ununuaji wa madini kwa kuwa na soko hapa Mirerani na Orkesumet na soko lingine litafunguliwa hivi karibuni," alisema Chaula.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wa Madini Tanzania (Tamida), Sam Mollel, alishauri tozo hizo kutolewa kuwa kuwa zilikuwa tatizo kubwa kwa wadau wa madini.

Mollel alisema hali hiyo imehamasisha wachimbaji wadogo kuuza madini kwenye masoko ya madini kwa kuwa wana imani kodi zilizoleta usumbufu kwa wadau wa madini zimeondolewa na Rais Jophn Magufuli.

Katibu wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (Marema), Tariq Kibwe, alisema wadau wa madini wanaendelea kupewa elimu ya ulipaji kodi.

Mdau wa Madini ya Tanzanite, Shifonya Solomon alisema ukuta unaozunguka migodi ya madini ya Tanzanite, umekuwa na manufaa kwao.

Dalali wa Madini, Elisha Laizer alisema uwepo wa masoko ya madini ya vito ni nafuu kwao, kwa kuwa watapambana na matatizo mbalimbali yanayowakabili ikiwamo bei ya madini ya Tanzanite.

Salome Mnyawi, muuzaji wa magonga ya Tanzanite alisema, baadhi ya wanawake wa eneo hilo, watachangamkia soko hilo kupitia umoja wao.

# EAC yazindua mfumo wa takwimu fedha

**Na Novatus Makunga, ARUSHA**

JUMUIYA ya Afrika ya Mashariki (EAC), imezindua mwongozo wa takwimu za fedha kwa serikali pamoja na usimamizi wa madeni kwa sekta ya umma na ukusanyaji wa mapato ya kodi.

Akizindua mwongozo huo juzi, Naibu Katibu Mkuu wa EAC, anayeshughulikia miundombinu ya fedha na utawala, Mhandisi Steven Mlote, alisema mwongozo huo, ni muhimu kwa kuwa viwango ni bora kwa takwimu kwa nchi hizo.

Mlote alisema lengo la mwongozo huo, mfumo wa eneo zima la Afrika ya Mashariki na kimataifa katika uandaaji wa takwimu za fedha za serikali (GFS) na takwimu za deni la taifa (PSDS).

Alisema mwongozo huo unaelekeza mikopo ya serikali ya nchi wanachama wa EAC, usizidi asilimia tatu ya pato la taifa (GDP), makusanyo ya kodi yawe zaidi ya asilimia 25 ya GDP na deni la taifa liwe chini ya asilimia 50 ya GDP.

Kwa mujibu wa Mlote, vigezo vinavyofanana na makusanyo na uandaaji wa takwimu za fedha utaondoa mkanganyiko wa kuanzishwa kwa umoja wa sarafu wa Afrika ya Mashariki ifikapo mwaka 2024.

Alisema itifaki ya Umoja wa Sarafu wa Afrika ya Mashariki (EAMU) itakuwa na uratibu imara wa sera ya uchumi.

Kifungu cha 17 cha itifaki ya umoja wa sarafu wa Afrika ya Mashariki kinataka nchi hizo, alisema kinataka kuwa na mfumo wa kimataifa wa kuandaa na kuchanganua takwimu muhimu za umoja wa sarafu.

Alisema mwongozo huo ni sehemu ya matakwa ya itifaki ya umoja wa sarafu wa Afrika ya Mashariki yaliyoagizwa na Baraza la Mawaziri Novemba, 2014.

Licha ya kuzungumza hayo, alisema mpango huo umelenga maofisa wa serikali ambao wana jukumu la kuandaa takwimu za fedha EAC, kwa ajili ya kuweka viwango bora zaidi ya kitakwimu na kusimamia umoja wa forodha.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Adolf Ndunguru, alisema lengo la mwongozo huo ni kuwa na taarifa sahihi ambazo zitawezesha nchi hizo kuwa na sera nzuri.

Alisema mwongozo huo, utadhibiti matendo maovu ya usimamizi wa fedha na uchumi wa nchi na hauta athiri mipango ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

"Uzinduzi huu wa kuwa na takwimu zimeonyeshwa kwenye nchi zote ni muhimu kwa kuwa itasaidia kujenga umoja wa sarafu ulio imara," alisema.

Ndunguru alisema hata katika Umoja wa Ulaya ulianza kwa kuwa na matatizo kutokana kukosekana kwa mwongozo bora, na baadhi ya nchi hizo zilikosa nidhamu ya ukopaji.

Mkurugenzi wa Kituo cha Takwimu cha Shirika la Fedha la Kimtaifa (IMF-AFRITAC), Kanda ya Afrika ya Mashariki, Herve Jolly, alisema mwongozo huo umeandaliwa kwa awamu kwa msaada wa kitaalamu kutoka IMF.

Jolly alitaja awamu hizo kuwa ni pamoja na takwimu zinazoelezea kwa kina sekta ya umma, skimu ya bima kwa jamii, mfumo wa mapato na usimamizi wa deni la taifa, ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi, uandaaji wa mfumo wa sera, mchakato wa uandaaji wa nyaraka za biashara na uandaaji wa mwongozo sahihi wa taarifa za miamala inayoathiri uchumi.

Uzinduzi huo umewashiriki maofisa wa fedha, uchumi na fedha kutoka nchi za Eritrea, Ethiopia, Malawi, Kenya, Rwanda, Tanzania na Uganda.



Mfanyabiashara wa nguo za mitumba, Msonge Gelvas, akipima kiuno cha suruali wakati akisubiri wateja kando ya barabara, jijini Arusha mwishoni mwa wiki. Wananchi wengi wa kipato cha kati na chini hupendelea matumizi ya bidhaa za mitumba kutokana na unafuu wa bei. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Madiwani wapitisha bajeti bil. 55.4/-

**Na Allan Isack, ARUSHA**

WAJUMBE wa Baraza la Madiwani Halmashauri ya Arusha DC wilayani Arumeru, wamepitisha rasimu ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/21.

Mpango huo una makadirio ya mapato na matumizi ya Sh. bilioni 55.4 na ulipitishwa wakati wa mkutano maalum wa Baraza la Madiwani uliofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita.

Akiwasilisha rasimu hiyo kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Mchumi Albert Mahoo, alisema kwa mwaka wa fedha 2020/21, halmashauri hiyo imepanga kukusanya na kutumia Sh. bilioni 55.4, kutokana na ukomo wa bajeti uliotolewa na Hazina.

Alisema mchanganuo wa mpango wa bajeti ya Sh. bilioni 55.4 ni pamoja na Sh. bilioni 4.9 kutumika katika katika matumizi ya kawaida sawa na asilimia 8.86 na Sh. bilioni 8.9 zitatumika kutekeleza miradi ya maendeleo sawa na asilimia 16.8. pia alisema Sh. bilioni 41.6 itakuwa ruzuku ya mishahara ya watumishi sawa na asilimia 75.06.

Katika kutekeleza miradi ya maendeleo, alisema halmashauri hiyo itatumia mapato ya ndani ya Sh. milioni 832.5, Sh. bilioni 3.5 fedha za ruzuku kutoka serikali kuu na Sh. bilioni 4.5 kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo.

Alisema halmashauri hiyo imepanga kushirikiana na wananchi katika utekelezaji wa majukumu ya msingi ili kufikia malengo ya dira ya taifa ya kutoa huduma bora kwa wananchi na kuondoa umaskini.

Vipaumbele vya halmashauri hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/21, ni elimu, kilimo na umwagiliaji, mifugo na uvuvi, afya, ardhi, mipango miji, maliasili, fedha na biashara, rasilimali watu na utawala, Tehama na maeneo mtambuka.

Hata hivyo, wajumbe wa baraza hilo, licha ya kupitisha mpango wa bajeti hiyo, walisema endapo bajeti hiyo itatekelezwa kwa ufanisi, itakuwa na mafanikio makubwa kwa kuwa imepanga kutekeleza miradi inayowagusa wananchi moja kwa moja.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Baraka Simon, alisema mpango huo utatekelezwa kwa ufanisi, lakini aliitaka halmashauri kubuni miradi ya kimkakati ambayo itatekelezeka na kuiletea halmashauri mapato na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa bajeti hiyo.

Diwani wa Viti Maalum, Jasmin Bachu, ameishauri halmashauri kufanya tathmini ya wafanyabiashara ambao si waaminifu wenye vitambulisho vya wajasiriamali kwa kuwa wanaikosesha mapato halmashauri.





# Mkoa wajivunia umeme uhakika kwa viwanda

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

SERIKALI imewataka wawekezaji kuwekeza kwenye viwanda kwa kuwa kuna umeme wa uhakika kwa kipindi chote cha mwaka.

Akizungumza Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Anna Mgwhira, alisema umeme unaozalishwa unatosheleza na kwamba upo wa ziada ikiwamo miundombinu rafiki.

Aidha, amelaani vikali taarifa iliyotolewa na Meneja wa Tanesco Mkoa ya kuwapo kwa baadhi ya watu kuhujumu shirika hilo kwa kuharibu miundombinu na wezi wa nyaya za umeme.

Mkuu huyo wa mkoa aliomba jamii kutoa ushirikiano katika kuwaibua watu hao ili waweze kuchukulia sheria kama inavyotakiwa.

"Nasikitika kuona baadhi ya watu wanalihujumu shirika letu kwa kuiba umeme, wezi wa mafuta ya transfoma pamoja na nyaya za umeme nitoe wito kuwa mtu anayefanya matendo haya ni kuhujumu uchumi hivyo pindi atakapokamatwa ni lazima ashtakiwe kwa kuhujumu uchumi na wananchi tunaomba ushirikiano katika kuwabaini watu hawa," alisema Mgwhira.

Kwa upande wake, Meneja wa Tanesco Mkoa wa Kilimanjaro, Mhandisi Mahawa Mkaka, alisema umeme unaozalishwa katika mkoa huo ni megawati 135, ambapo matumizi kwa mkoa mzima kwa sasa ni megawati 42.

Mhandisi Mkaka alisema kuwa, kwa miundombnu iliyowekezwa na shirika hilo katika mkoa kuna nafasi ya kutosha ya ziada hata kama wawekezaji wa viwanda wakija kuwekeza ndani ya mkoa huo hawatapata changamoto ya kukatika kwa umeme.

Meneja huyo alisema kuwa changamoto nyingine ni ulinzi wa miundombinu ya shirika hilo, ambapo baadhi ya watu wasio waaminifu wanaiharibu ikiwamo kuiba nyaya za umeme na mafuta ya Transfoma huku wengine wakiiba vyuma na wezi wa umeme.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agnes Hokororo, alisema serikali imeendelea kuweka miundombinu rafiki ya kuhakikisha wawekezaji wananufaika kwa muda mfupi mara anapofika mkoani hapo.

"Kila wilaya imetenga maeneo yatakayowasaidia wawekezaji kuwekeza, tunawaomba wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kuja na kuwekeza katika wilaya zetu," alisema.

# Wafanyabiashara walilia kodi kubwa

**Na Mary Mosha, MOSHI**

WAWEKEZAJI wazawa mkoani Kilimanjaro wameiomba serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza kodi zinazowakabili ili kuimarisha uwekezaji na kutoa ajira kwa vijana.

Meneja Msaidizi wa Marenga Milis, Priva John, akizungumza na gazeti hili, alisema kuwa wawekezaji wa ndani wanakabiliwa na mzigo wa kodi hali ambayo inasababisha kukwama kwa wawekezaji wazawa wenye mitaji midogo.

Alisema ikiwa serikali itaona umuhimu wa kupunguza mrundikano wa kodi kwa wawekezaji wazawa, wataweza kuimarisha thamani za bidhaa wanazozalisha na kuwa na bei nafuu kwa wateja wao.

"Tunaiomba serikali ikae na wizara husika pamoja na halmashauri kuangalia namna bora ya kumvutia mwekezaji mzawa ili aweze kumudu gharama za uzalishaji na kusaidia kuwapo kwa bidhaa zenye ubora kwa bei nafuu," alisema.

Kwa upande wao, baadhi ya wafanyabiashara wakubwa Manispaa ya Moshi, Elia Malya, alisema ikiwa serikali inania ya dhati ya kuifanya Tanzania kuwa na nchi ya viwanda na kufikia uchumi wa kati 2025 ni lazima iwatazame wawekezaji wazawa na kuwapunguzia mzigo wa kodi.

Alisema ikiwa watapunguziwa mzigo wa kodi, wataweza kuzalisha kwa wakati na bidhaa zenye ubora ambayo bei zake zitakuwa nzuri pamoja na kuajiri Watanzania wengi.

"Sisi wafanyabiashara tunaonekana siyo wazalendo, lakini siyo kweli bidhaa za kutoka nje ya nchi zinakuwa zinauzwa kwa bei nafuu zaidi kuliko zile zinazozalisha hapa ndani ya nchi...na hiyo ni kutokana na mrundikano wa kodi wanazotozwa wawekezaji wa ndani na kushindwa kuzalisha na kuuza bei nzuri," alisema Edward Mroso.

Mwanaisha Mzava, alisema mbali na bidhaa hizo kuzalishwa kwa gharama kubwa na kushindwa kuuza bei ambayo ni ya kawaida, lakini wanashindwa kulipa wafanyakazi mishahara mikubwa kutokana na faida ndogo wanayozalisha.

Akijibu juu ya mishahara midogo inayotelewa na baadhi ya wawekezaji kwenye viwanda vyao, Ofisa Kazi Mfawidhi Mkoa wa Kilimanjaro, Mwinyimkuu Mturuya, alisema wanaendele kutoa elimu juu ya haki na wajibu wa wafanyakazi pamoja na waajiri.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Vijana, Wanawake na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama (kushoto), akiwa katika ziara ya kukagua majengo ya mradi wa mnada wa kuku uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma, ikiwa ni moja ya miradi iliyofadhiliwa na Ubalozi wa Denmark kupitia mradi wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji (LIC) kwa kushirikana na Baraza la Taifa la Biashara(TNBC). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC ataka wananchi kupunguza mifugo

**Na MaryMosha, MOSHI**

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, amewataka wananchi wanaoishi vijiji vya Mtakuja na Mserikia katika Wilaya ya Moshi kuanza kupunguza idadi ya mifugo yao kwa kuuza ikiwa ni njia mojawapo ya kukabiliana na migogoro ya kugombea malisho kati ya wafugaji na wakulima hasa nyakati za ukame.

Aidha, alisema kuna haja ya jamii hiyo kuanza kufuga kisasa na kupunguza idadi ya makundi makubwa ya mifugo ambayo yamekuwa yakiharibu mashamba ya wakulima na kusababisha migogoro ya mara kwa mara.

Mkuu huyo wa mkoa alitoa agizo hilo juzi, wakati akizungumza na wananchi wa vijiji juu ya njia bora za kumaliza migogoro kati ya makundi hayo mawili.

"Viongozi wa vijiji hivi viwili, nataka muandae mpango mkakati wa kuisaidia jamii ya wafugaji kuwa na shughuli mbadala za kuwaingiza kipato," alisema na kuongeza:

"Naagiza fikirieni kupunguza sehemu ya mifugo yenu na kubakisha idadi ndogo ya mifugo kwa sababu ongezeko la watu limesababisha ardhi kuwa finyu na haitoshi kwa malisho na kilimo."

Mmoja wa wafugaji, Lomayani Alaisi, alisema hawana tatizo na agizo hilo kwa kuwa wanafahamu linalenga kuwahimiza kufuga kisasa na kuepukana na migogoro isiyo ya lazima.

"Binafsi sina tatizo na nitatii agizo la serikali la kutaka kupunguza mifugo na kuanza kufuga mifugo ya kisasa, naijua adha kubwa ninayoipata kipindi cha kiangazi tunapohama na makundi ya mifugo kwa ajili ya kuitafuta malisho katika mikoa ya jirani. Kazi kubwa iko kwa wenzangu kukubaliana na jambo hili ambalo kwao ni gumu," alisema Lomayani.

Awali, Diwani wa Kata ya Mabogini (Chadema), Emmanuel Mzava, akizungumza mbele ya mkuu huyo wa mkoa alisema wameanza utaratibu wa kutenga maeneo ambayo hayajaendelezwa kwa ajili ya malisho.

"Baraza la Maendeleo ya Kata lilikaa na kupitisha azimio la kuunda kamati za kudhibiti makundi ya mifugo yanayotoka mbali na kuingizwa kwenye mashamba ya wakulima, kamati hiyo ipo na imeshaanza kazi. Pia tumetenga maeneo kwa ajili ya malisho hivyo tunaamini migogoro hii itafikia mwisho," alisema Mzava.

Nipashe
# TESA
Jumanne Februari 4, 2020
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 14

## Veta mpya kuondoa vijana vijiweni



Ukurasa 15

## Safari nzuri ufaulishaji wa mkoa unapokwazwa na doa



Ukurasa 19

## DC acharuka kufeli kusikoisha



### RAWAN ALIYEANZIA MIAKA 12...

# Binti anayeweka rekodi kubakisha mmoja, kufikia vilele milima yote mirefu duniani

Ukurasa 16

ELIMU YA KIPOLISI

# TRAFIKI WAKO KAZINI KILA KONA









JIELIMISHE

# Veta mpya sasa kuondoa vijana vijiweni Mkuranga

## •Wataalamu viwanda waja

**NA YASMINE PROTACE,** MKURANGA

VIJANA kukaa vijiweni bila ya kuwa na shughuli maalumu, ni ishara ya hatari, kutokana na ukosefu wa ujuzi ambao ungeweza kuwashughulisha na kujiingizia kipato.

Kumekuwapo na tatizo la baadhi ya vijana kujiingiza katika makundi yasiyofaa, sababu ni hawana kikuu cha kufanya, katika mihangaiko ya kila kukicha.

Lakini wapi vijana hao walisoma vizuri na kumaliza kuvuka hatua ya kimasomo, lakini hali ya kukosa ujuzi wa kufanya, kunawarudisha washinde vijiweni.

Tumekuwa tukiona na kushuhudia baadhi ya vijana ambao hawajafanikiwa kujiunga na elimu ya msingi, sekondari na hata vyuo, wanapochukua mbadala wa vyuo vya maendeleo ya ufundi, maarufu Veta, sasa wamepata ujuzi unaowasaidia ujuzi kuwaongezea kipato.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani, Injinia Mshamu Munde, anasema, wanatarajia kujenga chuo cha kisasa cha Veta kitakachowasaidia wanafunzi.

Anawataja walengwa wakuu, ni wale ambao hawakupata nafasi ya kujiunga na sekondari kidato cha kwanza au wahitimu wa kidato cha nne waliokosa nafasi ya kuendelea na masomo zaidi.

Injinia Munde anasema, wote hao watajiunga katika chuo hicho cha Veta na kupatiwa ujuzi utakaowasaidia kujiongezea kipato, kwani uongozi wa wilaya umegundua hali ya wahitimu wengi wanashinda vijiweni, hawana sifa za kujiajiri na wanaishia katika makundi yasiyofaa.

Mtazamo wa mkurugenzi huyo, ni kwamba kuanzishwa chuo hicho, kutakuwa mkombozi wa vijana kujiajiri hata kujikita katika shughuli za kuwapa kipato wakitumia ujuzi walio nao.

Anasema, chuo hicho kinatarajiwa kujengwa katika Kata ya Shungubweni na imeshapatiwa eneo la mita za mraba 221,000.

"Veta itatusaidia taratibu ambazo zitakazotuwezesha kujengwa kwa chuo, ikiwamo kupatiwa hati baada ya kukamilika kwa taratibu hizo," anasema.

Anafafanua taratibu za ujenzi, zitaanzia kwa kuwatumia wadau wa maendeleo, kazi kuu ya kwanza ikiwa ni kuitafutia ramani itakayosaidia kutoa picha ya kiasi cha fedha kinachotakiwa katika ujenzi wake. Mtazamo uliopo ni kwamba, chuo kitaanza kikiwa ni cha kutwa na kwa kuwachukua wanafunzi wa Mkuranga pekee na baadaye kitakapokuwa na mabweni, watachukuwa watu kutoka maeneo ya mbali nchini.

Injinia Munde anasema, ni chuo kitakachosaidia watoto kutokaa vijiweni wanapokosa nafasi za kujiunga na hatua zaidi ya masomo, mathalan kutoka msingi kwenda sekondari.

Anatoa wito wake kwa wadau wa maendeleo, kuwasaidia ili watimize azma yao ya Mkuranga kuwa na chuo cha kisasa cha Veta, akimuunga mkono Rais Dk. John Magufuli, anayependekeza kutekelezwa umuhimu wa Mkuranga kuwa na chuo chake cha ufundi.

"Nchi haiwezi kufikia uchumi wa viwanda, bila ya kuwa na jamii yenye wafanyakazi wasio na ujuzi," anasema Munde na anaongeza kuwapo Veta, kina maana ya ujuzi zaidi wa kufanya kazi kwa kutumia teknolojia.

Anasema, hadi sasa wilaya ina idadi kubwa ya viwanda na anaamini wakipata elimu sahihi, hasa kupitia Veta, itawaondoa katika sifa ya kuwa vibarua katika utitiri wa viwandani vinavyofunguliwa Mkuranga.

Injinia Munde anasema, hata hivyo Wilaya ya Mkuranga ina vyuo vidogo vya elimu ya ufundi stadi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani, Injinia Mshamu Munde. **PICHA: YASMIN PROTACE**

UCHAMBUZI

**NA SABATO KASIKA**

# Safari nzuri ufaulishaji wa mkoa unapokwazwa na doa



Hali ya darasani, shule ya msingi mkoani Mtwara. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

KATIKA matokeo ya mtihani wa taifa wa kuhitimu elimu ya msingi mwaka jana, mikoa 13 ilitajwa kuwa vinara, kutokana na wanafunzi wote waliofanya mtihani katika mikoa hiyo kuchaguliwa kuingia sekondari.

Mikoa hiyo, iliyotajwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo ni Tabora, Katavi, Njombe, Dodoma, Geita, Kilimanjaro, Morogoro.

Kwa mujibu wa Jafo, mikoa mingine iliyofanikiwa kupeleka wanafunzi wote sekondari ni Ruvuma, Shinyanga, Singida, Mwanza, Kagera na Mtwara.

Hata hivyo, pamoja na kufanikiwa katika hilo, sintofahamu ilijitokeza kwa baadhi ya wanafunzi kutoripoti shuleni, shule zilipofunguliwa tangu Januari 6 mwaka huu.

**KILICHOJIRI**

Mtwara ni miongoni mwa mikoa iliyokumbana na sintofahamu hiyo, kufuatia wanafunzi wa kidato cha kwanza zaidi ya 3,000 kutoripoti shuleni, kwamba asilimia 75 ya wanafunzi hao bado hawajaripoti.

Matarajio ya mkoa ni wanafunzi 20,400 ndiyo waliofaulu mtihani wa darasa la saba na kutakiwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu, lakini inadaiwa wachache tu ndio walioripoti.

Hiyo ni kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa, Gelasius Byakanwa, baada ya kufanya ziara katika Manispaa ya Mtwara Mikindani na kukuta hali hiyo ambayo ilimshangaza na kutoa agizo zito.

Agizo lake, alitaka wazazi wote waliogoma kupeleka watoto shule sheria ichukue mkondo wake na akakumbusha kuwa nia ya serikali ya kutoa elimu bure, ni kuona wanaobahatika kupata fursa za sekondari, wanajinga huko.

Itakumbukwa nchini katika kutimiza hayo, ulianzishwa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) miongo miwili iliyopita, ikilenga katika mistari ya kuboresha huduma, mahitaji na elimu inayotolewa shuleni.

Hadi sasa kuna mfano wa sekondari za kata zilizosambaa nchini kote, kukidhi mahitaji ya kielimu katika ngazi zote, jamii iliko.

Leo hii, yanayotekelezwa, mzizi wake ulianza katika mipango ya awali baada ya uhuru wa nchi na kisha baadaye, ukawepo katika mpango maalum wa kwanza kati ya mwaka 1964-1969, zaidi ikijikita katika elimu ya msingi kuwafikia Watanzania wote.

Katika mipango iliyofuata, ikiwamo wa pili 1969 hadi 1974, ilikuwa na maboresho zaidi hata elimu ya ngazi ya juu, sekondari na vyuo, huku kukipitishwa Azimio la Musoma, kuhusu elimu. Moja ya zao lake, ni kuundwa kwa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA).

> “Utoro wa wanafunzi upo nchi nzima, lakini nimeitaja mikoa hiyo 13 iliyoingiza wanafunzi wote sekondari, ambayo ilitarajiwa kwamba ingeendelea kuwa kioo kwa kuhakikisha wote wanaripoti shuleni.



Wanafunzi wa shule ya sekondari iliyopo wilayani Masasi, mkoa Mtwara.

Kwa kurejea Mtwara, mkoa umefanya vizuri kwa wanafunzi wote wa darasa la saba waliochaguliwa kwenda sekondari kupewa nafasi yao. Kasoro imejitokeza, pale kitendo cha wanafunzi kutoripoti shuleni pasipo taarifa zozote.

Kama wapo wazazi waliofanya makusudi kutowapeleka watoto wao shule, ni bora wabadili msimamo huo haraka ili wasikumbane na mkondo wa sheria kwa kuwanyima haki watoto wao haki ya msingi ya kupata elimu.

Viongozi wa vitongoji, vijiji na mitaa kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, wamshapewa rungu kuhakikisha wazazi wenye mchezo huo wanakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Ni bora wazazi wakajiongeza na kuwapeleka watoto wao shule bila kusukumwa, kwani hakuna kisingizio cha ukosefu wa ada, kutokana na ukweli kwamba elimu inatolewa bure hadi kidato cha nne.

Mkoa kupeleka wanafunzi wote sekondari ni sifa na inaonyesha wanafanya vizuri darasani, cha kujiuliza ni kwamba inakuaje washindwe kuripoti shule? Nini kiko nyuma ya utoro huo?

Kwa ujumla ni kwamba mikoa iliyofanikiwa kupeleka sekondari wanafunzi wote waliohitimu elimu ya msingi mwaka jana, ina tatizo hilo la utoro ila tofauti ni idadi tu ya wanafunzi ambao hawajaripoti shuleni.

Utoro wa wanafunzi upo nchi nzima, lakini nimeitaja mikoa hiyo 13 iliyoingiza wanafunzi wote sekondari, ambayo ilitarajiwa kwamba ingeendelea kuwa kioo kwa kuhakikisha wote wanaripoti shuleni.

Lakini, matokeo yake yamekuwa kinyume na kufanana na mingine ambayo hadi sasa, baadhi ya wanafunzi bado hawajaripoti na inawezekana wapo wazazi waliohamisha watoto wao kujiunga na shule nyingine.

Hata kama wamefanya hivyo, kuna ubaya gani kutoa taarifa, ili uongozi wa shule ujue hilo? vinginevyo watoto wao wanaendelea kuhesabika kwamba ni watoro wakati wakiendelea na masomo, katika shule nyingine!

Kwenye hili suala la utoro wa wanafunzi na hasa wa kike, huwa kuna tuhuma kwamba baadhi ya wazazi hukataa kuwaendeleza kielimu na badala yake wanabaki nyumbani ili waolewe.

Zipo tuhuma kwamba, wengine huwaelekeza wafanye vibaya kwenye mtihani, ili mwisho wa siku wasifaulu kwenda sekondari, lengo likiwa ni hilo la kutaka waolewe ili wazazi wapate mahari.

Kama hizo ni miongoni mwa sababu zilizosababisha baadhi ya wanafunzi waliochaguliwa kidato cha kwanza, kutoripoti shule, ni vyema sheria ichukue mkondo wake dhidi ya wazazi wa aina hiyo.

Lakini wanafunzi wenyewe wanaokumbana na visa vya aina hiyo wanapaswa kujiongeza, kwa kutafuta njia ya kujinasua katika mazingira hayo na hatimaye waendelee na masomo.

Wanaweza kutoka kwao na kwenda kutoa taarifa kwa viongozi wa vitongoji, vijiji au mitaa ili hatua zichukuliwe za kuhakikisha matatizo yanayowakabili yanashughulikiwa, ili hatimaye wapate msingi ya kusoma.

ELIMU

**NA WOINDE SHIZZA, ARUSHA**

RAWAN ALIYEANZIA MIAKA 12...

# Binti anayeweka rekodi kubakisha mmoja, kufikia vilele milima yote mirefu duniani

• 'Ajifua' kupanda mrefu kuliko yote • Anaiingiza Tanzania rekodi ya dunia • Machi; atakwea mlima mrefu duniani

RAWAN Dakak, ni Mtanzania anayeangukia kundi la wasichana, mzaliwa wa mjini hapa, kwa sasa umri wake unatimu miaka 18, akiwa tayari ameshaweka rekodi ya kipekee kupanda milima sita mirefu duniani.

Haishi hapo, anasonga mbali zaidi mwezi ujao, anatarajia kutimiza ndoto ya kupanda mlima mrefu duniani, Everest, wenye kimo cha mita 8,848 kutoka usawa wa bahari, katika eneo la Mahalangur, ambalo ni sehemu ya milima ya Himalaya, inayotenganisha mipaka ya mataifa Nepal na China.

Huwa kuna usemi 'usione vyaelea, ujue vimeundwa.' Msichana, Rawan alianza kupanda mlima nchini akiwa na umri wa miaka 12 tu, baada ya kujiunga na timu ya shule ya upandaji milima, alikopatiwa elimu, ujuzi na taarifa mbalimbali za milima duniani.

Baada ya kupata mafunzo yaliyomwingia kwa tija, msichana huyo alivutiwa sana na mchezo wa kupanda na akajikuta, ushiriki wake unamwekea rekodi ya kupanda milima mirefu kutoka katika mabara yote duniani.




Rawan Dakak, akiwa katika matukio tofauti. Alipoupanda Mlima Kilimanjaro, ikiwa ni sehemu yake ya mazoezi ya kupanda Mlima Everest, mwezi ujao. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**



### ILIKUWAJE?

Msichana Rawan, aliiambia Nipashe kwamba, ni uamuzi wake binafsi uliomsukuma kujitosa katika mchezo huo milimani, anasema alihakikisha haungiliani kitu na kuharibu masomo yake, katika lengo la kupata ufaulu.

Anabainisha kuwa ndoto yake imekuwa ya kweli na mpaka sasa ameshapanda milima sita katika mabara manne akipeperusha bendera mbili katika kila kilele alichofikia; moja ya nchi yake Tanzania na ya pili, amani ya dunia.

Rawan anasema, lengo lake kuu ni kufikisha ujumbe wa kutaka amani duniani, kuhamasisha maendeleo kwa wanawake na vijana wa rika lake, akiwataka wajitahidi kutimiza ndoto zao na kufahamu chochote wanachikiwekea nia, kinawezakana.

Anataja baadhi ya milima aliyokwishapanda ni wa nyumbani Kilimanjaro, wenye urefu wa mita 5,895, mwingine Elbras uliopo nchini Russia barani Ulaya wenye urefu wa mita 5,648.

Mingine anayoitaja ni Aconcagua, uliopo nchini Argentina, Amerika Kusini, wenye urefu mita 6,962; Carstenz Pyramid, uliopo Indonesiam, barani Asia wenye urefu wa mita 4,884; na Vinson Massin, ulio mrefu zaidi bara Antartica jirani na nchini Chile, ukiwa na urefu wa mita 4,892.

> Wazazi wenzangu napenda kuwaambia mtoto akiwa na ndoto yake tusiipuuze bali tumsaidie kufikia anapotaka.

### ALIVYOJIANDAA

Rawan anasema, siri ya mafanikio yake ni kwamba, kila mara alipitaka kupanda milima, alitakiwa kufanya mazoezi kwa saa 20 kila wiki, yanayompa uwezo wa kubeba mzigo wake wenye kilo 35, katika hali ya hewa ya baridi chini ya nyuzi joto sentigredi 30 akinuia kutimiza ndoto ya kuupanda Mlima Everest.

Kijana huyo anasema, ni aina ya mazoezi yanayowavutia wengine kushirikiana na tayari kuna wenye vifaa vya kupanda mlima vyenye uzito wa kilo 30 na wanfanya mazoezi ya kuhimili upandaji mlima. Katika mazoezi hayo, ameshapanda miwili mkoani Arusha, ukiwamo Mlima Meru wenye kimo cha mita 4,562; Ruwenzori nchini Uganda, una mita 5,109; Mlima Kazbegi wenye kima cha mita 5,033, nchini Russia.

Anaeleza imani yake kwamba, atakapofanikwa kuupanda kileleni Mlima Everest wenye kima cha mita 8,848, ataingia katika rekodi kuwa mwanamke wa kwanza mwenye umri mdogo duniani kupanda mlima huo.



Wapanda mlima waliofika kileleni mwa Mlima Everest, ambao ni mrefu zaidi duniani, anakowania kufika Rawan Dakak, mwezi ujao. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Mbali na hilo, anasema atakuwa Mtanzania wa kwanza kupanda mlima huo na kuvunja rekodi ya kupanda milima yote mirefu iliyopo katika mabara saba ya dunia.

"Nafanya mazoezi ya ndani kwa saa 20 kwa wiki, yanayonipa uwezo wa kubeba mzigo wenye kilo 10 hadi 15 na kuvuta mwingine wenye uzito hadi kilo 25," anasimulia na kuendelea:

"Mazoezi mengine ninayoyafanya ni kupanda mlima katika hali ya baridi...mazoezi haya yamenilazimu kupanda mlima Kilimanjaro uliopo Tanzania wenye mita 5,895, mlima wenye baridi kali wa Kazbek."

Anataja milima mingine anayofanyia mazoezi ni yenye kimo cha mita 3,820, ukiwamo Ararat wenye mita 5,137 nchini Uturuki; Mlima Kenya (mita 4,985); na Qurnat wa Lebanon wenye (mita 3,088).

"Hii nimepanda ni kwa ajili ya mazoezi ya kupanda mlima mrefu kuliko yote duniani," anaeleza Rawan.

Historia inaonyesha watu wa kwanza kufika kilele walikuwa Edmund Hillary wa New Zealand na Sherpa Tenzing Norgay wa nchini Nepal, Mei 29, 1953, jambo ambalo kijana wa Kitanzania anaamini utamwingiza katika historia ya kuwa mwanamke kijana na Mtanzania wa kwanza kufika kilele cha Mlima Everest.

Rawan anakiri ni safari ngumu, ila anaamini ataimaliza vyema, akiwa na rai kwa Watanzania kumwombea safari yake ikamilike, atimiza ndoto hiyo ya kitaifa kufikia kilele cha milima saba duniani. Hadi sasa ameshapanda milima sita.

### MAMA YAKE

Huyo anajitambulisha kwa jina la Hala, ni mama mzazi wa Rawan, anayesema alipogundua ndoto ya mtoto wao, waliamua kumuunga mkono kwa kumpa ushirikiano wa kila hatua aliyofanya.

Anasema, mtoto wake alikuwa na malengo (ndoto ) ya kupanda milima yote mikubwa duniani na hadi sasa kufikia mafanikio aliyoyataja milima mitano mikubwa, akithibitisha kauli ya mwanawe, kwamba alianza akiwa na umri wa miaka 12 na hivi sasa anajiandaa kwenda kupanda mlima mrefu zaidi duniani.

"Tuliona mtoto wetu ana ndoto na tukaamua kumsapoti na ndio maana hadi sasa amepanda milima mitano mikubwa Afrika, lengo lake ni kupanda milima yote mikubwa Afrika na sisi lazima tuhakikishe amefanikisha ndoto zake," anasema.

> Hii nimepanda ni kwa ajili ya mazoezi ya kupanda mlima mrefu kuliko yote duniani.

Hala anaongeza; "Wazazi wenzangu napenda kuwaambia mtoto akiwa na ndoto yake tusiipuuze bali tumsaidie kufikia anapotaka."

### KUTOKA TANAPA

Kamishna wa Hifadhi Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (Tanapa) Dk. Allan Kijazi, anapongeza kijana huyo wa kike kwa kuweza kupanda orodha ya milima hiyo, ikiwamo wa nchini, Kilimanjaro, akiwa na umri mdogo.

Ahadi yake katika nafasi ya Tanapa, ni kumpa ushirikiano wa kutosha katika utimizaji wa ndoto yake, huku akibainisha pindi kijana huyo atakaporejea nchini kutoka katika safari yake ya kupanda mlima huo, atakuwa balozi mzuri wa kuutangaza mlima Kilimanjaro duniani.

Dk. Kijazi anasema, kijana huyo wa kike akirudi wataanzisha programu atakayoifanya kupita katika shule mbalimbali nchini, kuwahamasisha wenzake kupanda Mlima Kilimanjaro.

# Maana na aina ya kusoma, faida zake



Wanafunzi wanakijisomea. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

KWA mujibu wa kamusi, dhana kusoma ni namna ya kupata elimu kwa namna mbalimbali kama vile shuleni na vyuoni.

Pia ni namna ya kufahamu yaliyoandikwa kwa kutamka, au kupitisha macho, au kugusa maandishi, mbinu inayotumiwa zaidi na wasioona.

Inaelezwa kuna aina tatu za kusoma: kimyakimya, kwa sauti na kwa burudani.

Usomaji wa kimyakimya, mtu hufumba kinywa na kupitisha macho katika kila mstari kwa haraka. Macho hayo huunganisha neno lililotangulia na lile linalofuata, huku ubongo wake unachambua mambo muhimu yanayojitokeza na anayahifadhi kichwani.

Katika hilo, msomaji ananufaika kwa kupata nafasi ya kupima mwendo wake na kiasi cha uelewa; hujiepusha na kusumbua wengine; anazingatia kanuni za matamshi; na anasoma mengi katika muda mfupi, kulinganisha na anayetamka.

Pili, kusoma kwa sauti ni namna ya kuyaangalia maandishi na kuyatamka kwa sauti inayosikika.

Mambo ya kuzingatia hapo ni kwamba kuna vipengele viwili vinavyounda mchakato wa ufahamu wa kusoma: Uelewa wa msamiati na kile anachokisoma.

Ili kuilelewa anachokisoma, ni lazima msomaji awe na uwezo wa kuelewa msamiati uliotumika katika maandishi na endapo yaliyotumika hayataeleweka, uhafamu hautakuwapo.

Katika ufahamu wa kusoma, msomaji anatakiwa kuzingatia mambo kama kubaini mawazo makuu kwa kujiuliza, kinachoongelewa hapo ni nini? Ni jambo gani analolizungumzia mwandishi? Msomaji akiwa na maswali haya akilini mwake basi itakuwa rahisi kwake kuielewa habari hiyo.

Kingine, ni kuzingatia alama za zilizotumika; kwa kufanya hivyo kunamsaidia kuelewa ujumbe wa habari.

Pia anatakiwa kubaini maana ya maneno na misemo mbalimbali; habari nyingine huwa zina maneno ya kisanii, hivyo ni muhimu msomaji kubaini nafasi yake katika muktadha wa habari hiyo, kumsaidia kuelewa ujumbe wa mwandishi.

Vilevile, msomaji anatakiwa kuwa makini na anachokisoma, kila kipengele inampasa akielewe vizuri.

Kusoma kwa burudani; ni usomaji unaolenga kujiburudisha tuna mara nyingi huangukia zaidi katika magazeti, majarida na vitabu tofauti. Mambo ya kuzingatiwa katika ufahamu wa 'kusoma kwa burudani' ni kwamba kuna wakati mwingine si lazima msomaji awe na vitabu vyote anavyohitaji.

Ingawa lengo la msomaji huwa ni kujiburudisha tu, lakini pia hujiongezea maarifa. Hiyo ni kwa sababu, magazeti, majarida na vitabu, hutumia lugha sanifu kuelezea mambo mbalimbali yanayoihusu jamii.

Hivyo msomaji kutokana na kusoma vitabu na majarida mbalimbali hujiongezea kiwango cha uwelewa wa lugha na mambo mengine ya kijamii yanayojadiliwa humo.

Inaelezwa kuwa jambo zuri msomaji kujijengea tabia ya kujipima, ili aweze kuelewa kiwango cha maarifa aliyopata katika kujisomea. Kujipima huku kunaweza kufanywa kwa kujiwekea utaratibu wa kuweka kumbukumbu ya vitu au makala zilizosomwa na kufanya ufupisho wa kila makala.

JE, WAJUA?

**NA MWANDISHI WETU**

# Tafsiri kamili na nafasi ya mahari





Tukio la ndoa nchini Uganda. Kulia; zawadi ya mahari. **PICHA: MTANDAO**

"SICHUKULII mahari kama malipo yangu, kwa sababu Geoffrey hawezi kunilipa," anasema Angela, raia wa Uingereza mwenye asili ya nchini Ghana, anayeeleza utamaduni maarufu sana katika nchi za Kusini mwa jangwa la Sahara.

"Badala yake napenda dhana iliyopo kwamba, mchumba wangu na familia yake wananichukulia kama mtu wa thamani ninayejiunga na familia yao," anaendelea.

Mahari inatolewa wakati mume wake mtarajiwa anataka kuoa mahali fulani. Mume huyo mtarajiwa, huagizwa na wakwe zake watarajiwa, kuhusu mambo gani anapaswa kuyaandaa kabla ya harusi yao.

Mahitaji ambayo itaelezwa kuleta kabla, huwa ni fedha au zawadi, au vyote viwili. Mara nyingine, mahitaji hayo yanaweza kupelekwa kwa wakati mmoja, lakini mara nyingi mahari hailipwi kwa pamoja

Ni utamaduni ulio maarufu sana Thailand, China na Papua New Guinea.

Lakini, kwa upande wa mwanamke Angela, ni suala tu la kukubali alikotoka na ana maelezo: "Waafrika huona fahari sana na utamaduni wao kutoa na kupokea mahari. Kulikuwa na wakati ambao kuwa Mwafrika halikuwa jambo la kuvutia. Lakini, kwa sasa mambo yamebadilika na wenyeji wanajivunia utamaduni wao wa Kiafrika."

Mume wake, Geoffrey, ambaye ni Mwingereza mwenye asili ya Ghana, anayeelezea utamaduni wa kulipa mahari, kama kutoa shukrani kwa familia ya mke.

"Lakini, iwapo malipo yatakuwa ya juu sana na kuondoa ile ishara ya shukrani, kuna hatarisha mchakato mzima kwa sababu unaondoa maana ya mahari," anasema.

Wiki moja kabla ya ndoa yao, Geoffrey na Angela waliandaa sherehe ya harusi ya kitamaduni nchini Ghana na wakati wa sherehe, kama hiyo mahari hulipwa ama iwe pesa au zawadi, ilikabidhiwa kwa familia ya Angela.

Kundi la wanandoa waliamua kubadilisha sherehe yao na kuifanya kuwa ya kisasa zaidi, wakiitolea ufafanuzi katika kauli: "Ile mahari itakayotolewa baadaye tutapewa sisi wanandoa. Mama yangu amekuwa muwazi na kuanzia mwanzo alikuwa akisema 'wewe siyo wa kuuzwa, hakuna anayeweza kukunua."

Gharama ya mahari inatofautiana na Geoffrey anafafanua: "Haikuwa ghali, hivyo ilikuwa katika kundi la mamia."

Kuna wanandoa waliamua kuangaza mahari yao kwa mtazamo tofauti.

Yupo mwenye asili ya nchini Zimbabwe, anayesema alilazimika kutafuta kazi ya pili, aweze kulipa mahari aliyotakiwa kugharimia kiasi anachoweza anakilipa kwa awamu ambayo ikitimu ni gharama ya ununuzi wa nyumba.

Anasema iwapo angeshindwa kulipa mahari aliyotakiwa kuilipa, hangeweza kukutana na familia ya mke.

Daima kwa jumla, haifahamiki ni lini mahari ilikuwa jambo la lazima barani Afrika, lakini katika sehemu nyingi inaangukia katika sura ya pesa.

Kihistoria, ulipaji mahari unatofautiana, kulingana na nchi na utamaduni wa eneo.

Mwanaharakati Evelyn Schiller kutoka nchini Uganda, anapinga dhana ya utoaji mahari katika mtazamo imebadilika kwa kiasi kipindi anachokitaja cha vizazi vitatu vilivyopita.

"Tazama kwa wakati huu, mahari ilivyo. Inachukuliwa kwa misingi ya pesa na hapo ndipo neno malipo linapotokea. Siyo tena zawadi kwa bibi harusi badala yake imekuwa kama malipo kwa bibi harusi."

2015, mahakama ya juu zaidi ya Uganda ilitoa uamuzi kwamba mahari si kitu cha lazima na inapotolewa, isiwe cha lazima kurejeshewa wakati wa kutalikiana.

Hata hivyo, utoaji wa mahari umekuwa ukiendelezwa kijamii, ukichukuliwa ni njia moja ya kuimarisha uhusiano ndani ya jamii.

"Watu weusi Uingereza, tuna utamaduni wetu kwa sasa," anatamka Tolly T, mtangazaji redio wa nchini Uingereza mwenye asili ya Nigeria, anayehoji utoaji mahari kama unaweza kuzaa matunda kwao:

"Kwa waliozaliwa miaka ya 80 na kuendelea kama sisi, Waingereza weusi au wenye asili ya Nigeria, hata bila kujali chimbuko lako, tumekuwa na utamaduni wetu," anasema na kuongeza:

"Tunaendeleza kile tunachotaka kutoka Afrika na kufanya vivyo hivyo kutoka Uingereza. Kisha tunajiundia utamaduni wetu ambao unaturuhusu kujiuliza maswali na kuutekeleza kama ni msingi kwetu sisi."

***Kwa mujibu wa vyombo vya kimataifa.***

RIPOTI

# Virusi vingi vinatoka kwa wanyamapori

## • Ukimwi, Sars...

KWA miaka zaidi ya nusu karne, maambukizi ya magonjwa yamekuwa yakitoka kwa wanyama mpaka kwa binadamu.

Mwaka 1980, Ukimwi unadaiwa kutokea kwa sokwe mwaka 2004 mpaka 2007, mafua makali ya ndege na nguruwe, yalidaiwa kusababisha shida ya mafua makali mwaka 2009.

Vilevile ilibainika kuwa maambukizi ya Sars ulitokana na popo, huku ugonjwa wa ebola pia ulisababishwa na popo.

Binadamu wamekuwa wakipata magonjwa kutoka kwa wanyama, hasa maambukizi ya magonjwa ya hivi karibuni yanaelezwa kuwa yametokea kwa wanyamapori.

Mabadiliko ya mazingira yanaongeza kasi ya maambukizi aina hiyo kutokea, huku ongezeko la wanaoishi mjini kusafiri katika mataifa mbalimbali wakati ugonjwa huo umeanza, unafanya maambukizi yasambae kwa kasi zaidi.

Wanyama wengi huwa wana bakteria hatari na virusi vinavyosababisha magonjwa. Mzunguko wa virusi unategemea nani anavyo na kwa wakati gani kufikia upande mwingine.

Kwa mfano, asilimia 10 ya watu walifariki kutokana na maambukizi ya ugonjwa wa sars, inadaiwa mwaka 2003 ikilinganisha na mafua makali yaliyokuwa chini ya asilimia 0.1.

Mazingira na mabadiliko ya tabianchi, yanabadilisha tabia ya wanyama, namna wanavyoishi, maeneo yao na vyakula.

Namna maisha ya binadamu yanabadilika. Hivi sasa, asilimia 55 ya idadi ya watu duniani kote wanaishi mjini, wakati miaka 50 iliyopita walikuwa asilimia 35.

Mara nyingi wanyama pori huwa wanaofika mijini, kwa sababu hunapatikana vyakula vingi na kufanya mzunguko wa upatikanaji wa magonjwa uwe rahisi.

Nani hatarini?

Magonjwa mapya yanayojitokeza mara nyingi, ni hatari zaidi na yanapewa uangalizi wa karibu kimataifa.

Watu ambao wana mifumo dhaifu kwa kutokuwa na afya nzuri, ndio anatajwa kuwa hatarini, pia akitajwa mtu ambaye hana virutubisho vya mlo kamili, anaishi katika maeneo ambayo kuna hewa chafu na mazingira machafu.

Maambukizi mapya yanaweza kusambaa katika miji mikubwa ambayo ina mkusanyiko mkubwa wa watu, ambao wanavuta hewa kwa pamoja na wako kwa katika mazingira yanayofanana.

Baadhi ya utamaduni, watu huwa wanakula chakula ambacho vinahusiana na wanyamapori kwa karibu.

Ili kujikinga, jamii na serikali zinajaribu kukabiliana na maambukizi mapya ya magonjwa, kama ilivyo kwa corona hivi sasa nchini China.

Kadri mazingira yanavyobadilika, ndio magonjwa mapya yanaibuka, hivyo kuweka mazingira ni jambo muhimu, linaloweza kusaidia kupunguza mlipuko wa magonjwa na kusambaa kwake.

Pia, kubadili namna watu wanahusiana na wanyama katika mazingira yao ni jambo muhimu kuzingatiwa.

**Kwa mujibu wa taarifa za mtandao**



Ilivyokuwa mgonjwa wa virusi vya Sars akihudumiwa wodini nchini China. **PICHA: MTANDAO**

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI, ALIYEKUWA RUFIJI

# DC acharuka kufeli kusikoisha

• Aaanzisha operesheni Rufiji • Aaahidi 'kufa' na wazazi wasababishi• Wanaoishi na bibi shina la mimba • Wazazi kuhamia shamba nako tabu inayojitegemea



Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Juma Njuwayo (aliyesimama), akiongea kwenye mkutano na wananchi, walimu na wanafunzi katika Shule ya Msingi Umwe. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

WILAYA ya Rufiji mkoani Pwani, ina vijiji 38 na vitongoji 178, vyenye wakazi 130,000, kati yao asilimia 85 wanajishughulisha na kilimo.

Katika elimu wilaya hiyo bado inaelezwa kusuasua katika mwamko, hali ya utoro bado inendelea kuwa kikwazo cha ufaulu.

Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Juma Njuwayo, analazimika kufanya ziara katika kata za wilaya hiyo kuongea na wananchi, walimu na wanafunzi, kukemea vitendo vya utoro na kuweka mikakati ya ufaulu.

"Nimechoka, siwezi kuwa Mkuu wa Wilaya wa kumi za mwisho za ufaulu katika mitihani ya kitaifa. Tumekuwa tunavumiliana sana mnaniharibia kazi, siwezi kuendelea kukaa kimya," anasema Njuwayo.

Mkuu huyo wa Wilaya anabainisha, katika matokeo ya darasa la saba mwaka 2016, ufaulu ulikuwa asilimia 49, na mwaka jana ufaulu ulifikia asilimia 80 na Halmashauri hiyo ya Rufiji kuwa ya 112 kati ya halmashauri 186 ikilinganishwa na mwaka 2018, ilikuwa ya 179.

### AWAFUATA WALIKO

Njuwayo anasema, kutokana na takwimu hizo imemlazimu kuongea na wazazi, walimu na wanafunzi kuweka mikakati ya pamoja ili kuongeza hali ya ufaulu katika halmashauri hiyo.

Akiongea katika kata za Umwe, Ikwiriri, Mgomba, Mkongo, Ngorongo, Mwaseni na Kipugura anasema wilaya hiyo ina utoro na mimba zinazochangia ufaulu duni kwa wanafunzi.

"Naanza kuwaburuza mahakamani wazazi wa watoto watoro, haiwezekani tangu shule imefunguliwa mtoto hajafika shule halafu mzazi umekaa kimya hutoi taarifa shuleni wala husemi kama kuna tatizo ili walimu wajue," anasema.

Mkuu huyo wa Wilaya anasema, utoro kwa wanafunzi umekuwa kitu cha kawaida, huku wazazi wakielezwa kuwa chanzo kwa kushindwa kuwadhibiti watoto wao.

Njuwayo anasema, amepata taarifa ya baadhi ya wanafunzi kuaga nyumbani kwamba wanaenda shule, lakini wanaishia ufukweni na wengine maporini wakifanya vitendo vya uvutaji mihadarati.

Kuna taarifa kutoka katika vyombo vya usalama kuwa wapo watoto kuanzia darasa la pili hawaendi shule, wanaaga nyumbani, lakini hawafiki shule, huku wazazi wao wakiomba msaada kwa polisi kwa madai wameshindwa kuwadhibiti watoto wao.

"Huu utoro wa wanafunzi ndio unaochangia hasa kuwa na ufaulu hafifu, kama hakuna ushirikiano kati ya wazazi na walimu, hakuna mabadiliko yatakayopatikana kwa mujibu wa takwimu za kisayansi ni asilimia 30 tu ya mchango wa mwalimu, ili mwanafunzi afaulu.

"Asilimia 70 zilizobaki ni kwa mzazi na mtoto. Sasa kwa hali hii tusipochukua hatua kwa wazazi wazembe tutaendelea kuwa wa mwisho kwenye ufaulu?" Anahoj.

Pia, anasema kinachochangia ufaulu duni ni baadhi ya wazazi wamekuwa wakiwaamuru watoto wao wafanye vibaya kwenye Mtihani wa Taifa, ili wasiendelee na elimu ya sekondari.

### WAZAZI WAPOTOSHAJI

Njuwayo anasema, wazazi hao kwenye baadhi ya maeneo wanadaiwa kusema kuwa mtoto kufaulu na kuendelea na masomo ya sekondari ni moja ya chanzo cha umaskini kwenye familia.

Kauli hiyo mahususi anaielekeza kutolewa na wazazi wenye maisha duni, wanaodai vifaa na mahitaji ya sekondari ni vingi, hivyo watakuwa wanamalizia fedha zao huko na kushindwa kufanya mambo mengine.

Mbali ya mkakati wa kuwafikishia mahakamani wazazi ambao watoto wao ni watoro, mkuu huyo wa wilaya ameagiza kuwapo kwa makambi ya wanafunzi wenye mitihani ya kitaifa kwa shule za msingi na sekondari.

Anasema, endapo mwalimu mkuu na Mkuu wa Shule hawatatekeleza agizo hilo la kuweka kambi miezi mitatu kabla ya mtihani, atawavua vyeo vyao, pamoja na Ofisa Mtendaji wa kata husika.

Njuwayo anawataka wazazi kuanza kuwa na uhusiano mazuri na walimu, kwa kufuatilia maendeleo ya watoto wao, ili panapogundulika kuwapo tatizo litafutiwe ufumbuzi mapema.

"Wazazi fuatilieni watoto wenu, wakifanya vizuri hawa matokeo yake mtayaona baadaye. Tushirikiane tukomeshe mimba za wanafunzi ni aibu mtoto kumzaa mtoto mwenzie. Hii inachangia umaskini kwenye jamii zetu na watoto wenu wakiwa wasomi hapa Rufiji maendeleo yatakuwapo," anasisitiza.

Njuwayo anasema, takwimu za mwaka 2019 zinaonyesha wanafunzi 19 walikatisha masomo kwa kupata mimba wakiwa masomoni, kati yao wa shule za msingi saba na sekondari 12.

Aidha, kwa mwaka huu wanafunzi watatu waliotakiwa kujiunga na Shule ya Sekondari Mkongo, wameshindwa kufika shule kutokana na kupata mimba.

### MAOFISA ELIMU

Ofisa Elimu Msingi wa Wilaya ya Rufiji, Edward Buganga, anasema kumekuwapo mitihani ya kila mara kwa darasa la nne na la saba, lakini utoro umeendelea kuwa kikwazo cha ufaulu.

Buganga anasema, wapo watoto wa darasa la sita wanaopata mimba na kukatisha masomo, jambo ambalo ni kichocheo cha umaskini kwenye jamii.

Anatoa wito kwa wazazi kuwadhibiti watoto wao kuhudhuria kwenye vibanda vya video kuwa nao karibu na kufuatilia maendeleo yao kwani kwa kufanya hivyo itawainua watoto wa Rufiji kielimu na kuleta mabadiliko ya maendeleo.

Inaelezwa utoro uliokithiri na mimba za ututoni, vinachangiwa na watoto wengi kuachwa na wazazi wao wakijilea na kujitafutia chakula.

> Takwimu za mwaka 2019 zinaonyesha wanafunzi 19 walikatisha masomo kwa kupata mimba wakiwa masomoni, kati yao wa shule za msingi saba na sekondari 12.

Ofisa Elimu Sayansikimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Juliana Masanja, anasema idadi kubwa ya wanafunzi watoro na wanaopata mimba shule, ni wanaochwa na wazazi wao wakilelewa na bibi.

Aidha, chanzo kingine cha utoro ni ambao wazazi wao wanajishughulisha na kilimo, wazazi wanalazimika kukaa mashambani na kuwaacha watoto wakijilea wenyewe bila ya mwongozo wa wazazi.

"Baadhi ya wazazi wa Wilaya ya Rufiji, wamekuwa na tabia ya kuwaacha watoto na bibi zao, wengine wanaachwa wakijilea wenyewe mtoto anawalea watoto wengine hivyo wanaku huru kufanya wanachotaka, kuzurura kutoenda shule lakini wengine wanajiingiza kwenye vitendo vya ngono mapema" anasema Juliana.

Juliana anabainisha, kwa miaka miwili mfululizo, wanafunzi 18 walipata mimba na kushindwa kuendelea na masomo ya elimu ya msingi.

Anasema, kutokana na hali hiyo kitengo chake kimekuwa kikikutana na kamati za shule, kujadili namna ya kitatua changamoto hiyo, lakini kutoa elimu kwa wanafunzi walioko shuleni juu ya elimu ya madhara ya mimba za utotoni.

Mmoja wa wazazi, Nunu Ngayonga, mkazi wa Ikwiriri, anasema utoro na mimba za utotoni unachangiwa na wazazi wengi kukaa mjini na mashambani na kuwaacha watoto wakijilea wenyewe.



WADAU SABATO KASIKA

# Sauti za wadau

Mwaka 2010, serikali ilijiwekea miaka mitano kwamba kufikia 2015 sekondari zote za kata ziwe na maabara, lakini hadi sasa baadhi ya shule hazina. Wadau wanasemajе kuhusu hilo?



**AKAROLY GODFREY (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

MIMI nadhani miaka mitano, ambayo serikali ilijiwekea haikuwa sahihi kabisa, kwa sababu ilikuwa haijakamilisha mambo mengi yakiwamo madarasa, madawati na vifaa vingine vya shule.

Labda ingeamua kuelekeza zaidi nguvu kwenye majengo ya maabara na maabara zenyewe, lakini kufanya vyote kwa pamoja isingekuwa rahisi kuvikamilisha ndani ya miaka mitano, hasa kutokana na ukweli kwamba serikali yenyewe ina mzigo mkubwa wa majukumu kwa ajili ya maendeleo ya nchi na watu wake.

Kwa hiyo, ipo haja kuwashirikisha wananchi na wadau wa elimu katika kufanikisha jambo hili, kwa ajili ya kupata maabara bora na za kisasa kuliko zile za shule kongwe, ambazo nazo zimebaki kuwa za kawaida kutokana na maabara zake kuchakaa.

Binafsi ningeshauri kwamba uwepo ushirikishwaji wa wananchi katika jambo hili, ambalo linalenga kuinua kiwango cha elimu nchini na ikumbukwe kuwa masomo ya sayansi ndiyo yanayochangia kupata madaktari, wahandisi na wengine wa fani mbalimbali ndiyo maana huwa kuna maabara ambazo wanafunzi hujifunza kwa vitendo.

Kinachotakiwa ni kuweka kile kinachohitajika na tena kikiwa na ubora unaotakiwa, ili wanafunzi waweze kunufaika na elimu kwa vitendo.

Mkakati huo wa serikali wa kutaka kila shule kuwa na maabara ni mzuri na upewe msukumo ili kuhakikisha tatizo la baadhi ya shule kutokuwa na maabara libaki kuwa historia.



**ANDREW MURUGO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

BINAFSI sioni ubaya wowote kusikia serikali ikiahidi kufanya jambo fulani kwani ninatambua kuwa inafanya kazi kwa malengo.

Hata mimi niliwahi kumsikia naibu waziri wakati huo akiahidi kwamba ifikapo mwaka 2015 sekondari zote za kata zitakuwa na maabara.

Kwa maana hiyo ni kwamba ilikuwa imejiwekea mkakati kuhakikisha shule hizo zinakuwa na maabara ingawa ukosefu wa maabara kwenye shule hizo bado upo.

Wazazi, walezi na wadau wengine wa elimu washirikishwe katika jambo hili, kwani ndoto za Watanzania ni kuwa na wataalamu wa fani mbalimbali.

Ili kupata wataalamu hao, ni lazima kila shule kuwa na maabara kwani huko ndiko kwenye kitovu cha kuwapata. Nikumbushe kuwa nguvu za serikali pekee hazitoshi, bali nasi tunatakiwa kushiriki kwa hali na mali, katika kufanikisha upatikanaji wa maabara kila shule.

Lakini tukikaa pembeni na kusubiri kwamba serikali iliahidi bila kuona uwezekano wa sisi weenyewe kuchangia chochote, mwisho wa siku tutabaki kulalamika bila kutambua kuwa tuna wajibu wa kuzisaidia na kuziboresha shule zetu, ambazo kimsingi ni za umma na umma wenyewe ndiyo sisi Watanzania.

Tunaposikia matokeo mabovu ya wanafunzi katika mitihani na hasa kwenye masomo ya sayansi, tujue kuwa nasi tunachangia ubovu huo kwa kushindwa kuchangia uwepo wa maabara katika sekondari za kata tulizojenga kwa nguvu zetu wenyewe.



**ASHA NASORO (MKAZI WA MVUHA MKOANI MOROGORO)**

SEKONDARI kuwa na maabara ni mchakato unaohitaji kufuata hatua zote na hatimaye kufanikisha kila sekondari ya kata kuwa na maabara.

Maabara inahitaji kuwa na wataalamu wake, bila hao hata kama shule itakuwa na kila kitu, bado litakuwapo tu la wanafunzi kushindwa kujifunza kwa vitendo.

Hivyo kuwa maabara ni hatua, kuwa na majengo yake ni hatua nyingine, lakini kikubwa zaidi ni kuwa na wataalamu.

Ninatamani kila shule kuwa na maabara, lakini ni muhimu serikali ihakikishe inapata wataalamu wa kutosha na pia upatikanaji wa maabara uwe sambamba na kuwapo kwa umeme na kuwapa walimu mshahara mzuri, ili wasiendelee kukimbilia kwenye shule binafsi.

Suala la uwekaji wa maabara lisiofanywe bora liende tu kwa lengo la kuwaridhisha wananchi kuwa imetimiza ahadi kama ilivyoahidi, bali kinachotakiwa ni kufanya jambo la uhakika kwa manufaa ya watoto wa Kitanzania, ambao wanaandaliwa kwa ajili ya kuwa wataalamu na viongozi wa baadaye.

Lakini niipongeze serikali kwa juhudi mbalimbali ambazo inafanya katika kuinua kiwango cha elimu nchini ikiwamo kutoa elimu bure ili kuhakikisha watoto wote wa Kitanzania, maskini na matajiri wanapara elimu na hakuna tena anayebaki nyumbani kwa kisingizio cha kutokuwa na ada.



**KIDAWA ABDUL (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

TANGU mwanzo mie niliamini kwamba hiyo ilikuwa ni lugha ya kisiasa, kutokana na ukweli kwamba hadi sasa suala la ukosefu wa maabara kwa shule za umma bado ni tatizo, ambalo halijapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Wanafunzi wataendelea kushindwa sana katika masomo ya sayansi, kwa sababu hawayasomi kwa vitendo.

Hivyo wito wangu kwa serikali ni kwamba ichukue hatua za makusudi, katika jambo hili la msingi, kwani ilishafanya makosa miaka ya nyuma kwa kujenga shule nyingi, ambazo hazina kitu, ilikuwa ni bora ingejenga shule chache zilizokamilika kwa kila kitu kuliko hizi za sasa, ambazo zinaonekana kuwa kero kwa wanafunzi na wazazi pia.

Serikali ina vyanzo vingi vya kupata fedha, ingetumia vyanzo hivyo kupata fedha haraka zitumike kujenga na kununua maabara kwa ajili ya sekondari za kata.

Kwa sasa ukiamua kuzifuatilia shule hizi, utagundua kuwa baadhi hazina maabara, lakini hazina majengo yake. Sasa kwa mazingira kama hayo wanafunzi wanaweza kujifunza kwa vitendo?

Ikumbukwe kuwa wanafunzi wanapenda masomo ya sayansi, lakini wanashindwa ni namna gani wanaweza kuyajifunza kwa vitendo.

Utaratibu wa kuwa na maabara kila shule uharakishwe kwani serikali ndiyo iliahidi hilo mbele ya umma.



**FATUMA KUSAGA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KIPINDI hicho cha miaka mitano haikuwa mingi na ni kweli baadhi ya sekondari za kata bado hazina maabara.

Unaweza kukuta shule ina majengo ya maabara, lakini hakuna kitu, au ina maabara, lakini majengo hakuna ama ina vyote hivyo, lakini hakuna mtaalamu wa maabara.

Hivyo siamini kama ahadi hiyo ingetimia. Ila ninachojua ni kwamba serikali huwa ina utaratibu wake wa kushughulikia mambo, ikiwamo wa kuchangisha fedha au kuomba msaada kwa ajili ya maendeleo na mambo mengine ya msingi.

Kwa ujumla ni kwamba mimi kama Mtanzania sina uhakika na kuhusu kutimizwa kwa ahadi hiyo, cha msingi ni kusubiri iendelee kuleta maendeleo na pia ninatambua kuwa nchi bila wasomi wa taaluma mbalimbali inaweza kukwama.

Lakini pia ninaamini kwamba kuna mipango ya muda mrefu na mfupi ya kuboresha elimu. Kama Watanzania, tuendelee kuwatia moyo viongozi wa serikali kwa kazi kubwa ya kuleta maendeleo, ambayo wamekuwa wakiifanya.

Hebu tuwe tayari kushiriki katika jambo hili la kusaidia shule zote za sekondari za kata kuwa na maabara.

Hapa nina maana kwamba iwapo tutahitajika kuchangia kwa hali na mali, basi tuwe tayari kufanya hivyo, kwa sababu lengo ni kusaidia maendeleo ya elimu ya watoto wetu.





# Mil. 230/- kuboresha barabara Mbarali

**Na Nebart Msokwa, MBARALI**

WAKALA wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, imetenga zaidi Sh. milioni 230 kwa ajili ya uboreshaji wa barabara katika Mji wa Rujewa ndani ya miaka miwili ili kuwarahisishia wananchi usafiri na usafirishaji.

Hayo yalisemwa na Meneja wa Tarura Wilaya ya Mbarali, Mhandisi Abdul Mfundili, wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi ya Mkoa wa Mbeya ambayo ilikuwa inakagua miradi mbalimbali.

Mfundili alisema katika mwaka wa fedha 2018/2019 walitengewa Sh. milioni 200 kwa ajili ya kuboresha barabara ya Rujewa mjini yenye urefu wa kilomita 0.6 na mfereji wa maji wenye urefu wa mita 233.

Alisema walipata mkandarasi ambaye alitekeleza mradi huo kwa Sh. milioni 165.9 na aliikamilisha kazi hiyo lakini wakamlipa Sh. milioni 150.6 na kwamba barabara hiyo kwa sasa ipo kwenye matazamio na muda huo ukiisha mkandarasi huyo atalipwa fedha zote.

Alisema katika mwaka wa fedha 2019/2020 alisema wametengewa Sh. milioni 32 ambazo zitatumika kuboresha kipande kingine cha barabara na tayari wame kwa ajili ya kulima barabara yenye urefu wa kilomita 1.1.

Alisema barabara hiyo tayari mkandarasi amepatikana na amelima na kumwaga vifusi kwa gharama ya Sh. milioni 17.05 na kwamba bado mkandarasi huyo hajalipwa malipo yoyote.

"Lengo ni kuboresha miundombinu hii ili kuwarahisishia wananchi usafiri na usafirishaji, na miradi yote inatekelezwa kwa fedha kutoka katika mfuko wa fedha za barabara ambao upo chini ya Serikali Kuu," alisema Mhandisi Mfundili.

Alisema barabara hiyo ambayo inaendelea kuboreshwa inaelekea katika Hospitali ya Wilaya ili kurahisisha huduma za afya na kwamba baada ya kukamilisha wataanza barabara zingine.

# Serikali yamaliza mgogoro wa mpaka

**Na Nebart Msokwa, CHUNYA**

KAMATI ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, imetatua mgogoro wa vijiji vitatu vilivyokuwa vinagombea kitongoji cha wafugaji na kuhatarisha amani pamoja na kukwamisha shughuli za maendeleo.

Vijiji vilivyokuwa na mgogoro huo ni Mbugani katika Kata ya Mbugani, Chalangwa Chalangwa na Sangambi Kata ya Sangambi ambavyo vilikuwa vinagombea kitongoji cha Simba Leaf kwa zaidi ya miaka sita.

Vijiji hivyo kila kimoja kilikuwa kinadai kuwa kitongoji hicho ambacho kinakaliwa na wafugaji kiko upande wake na kila kimoja kikitaka kukusanya mapato ikiwamo michango kwa ajili ya ujenzi wa shule.

Akitoa taarifa ya ramani ya vijiji hivyo, Ofisa Ardhi wa Wilaya ya Chunya, David Wilson, alisema wakati wanafuatilia walibaini kuwa mpaka rasmi uko kwenye jiwe namba GM 22 ambalo ndilo linatenganisha vijiji vyote vitatu.

Alisema kitongoji cha Simba Leaf kilionekana kuwa ndani ya kijiji cha Sangambi na hivyo akashauri Kamati ya Ulinzi na Usalama kutumia ramani hiyo kufanya uamuzi.

Wilson alisema ramani iliyotumika kwenye utatuzi wa mgogoro huo ni ile ambayo iliboreshwa kwa mara ya mwisho mwaka 2006, hivyo akavitahadharisha vijiji hivyo kutoendeleza mgogoro huo.

"Alama zote tulizokuwa tunazifuatilia zinaishia kwenye hili jiwe na kwa kufuata jiwe hili, kitongoji hiki cha Simba Leaf kinatakiwa kiwajibike Sangambi badala ya Chalangwa kama ilivyokuwa awali," alisema Wilson.

Baada ya maelezo ya ofisa huyo, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, na wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, walifanya ziara mwishoni mwa wiki na kufanya mkutano wa hadhara ambao uliwaunganisha wananchi wa vijiji vote vitatu.

Mahundi alisema baada ya mgogoro huo kudumu kwa muda mrefu bila kupatiwa ufumbuzi, waliwaagiza maofisa ardhi kubainisha mipaka ya vijiji vyote vitatu kwa kutumia mfumo wa GPS na ndipo ikabainika kuwa Kitongoji kilichokuwa kinagombaniwa kipo ndani ya Kijiji cha Sangambi.

"Kuanzia sasa tunahesabu kuwa mgogoro huu umekwisha na bahati nzuri viongozi wa vijiji vyote wapo hapa na nawaagiza kuwa mabalozi wa kuwaelimisha wananchi juu ya kauli hizi za serikali badala ya wao kuwa vinara wa kuchochea," alisema Mahundi.

Alisema uamuzi walioutoa ni kwa mujibu wa ramani na si mipaka ya kutungwa, hivyo akawataka wananchi wa vijiji vyote vitatu kuheshimu mipaka hiyo.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Chalangwa, Thadeo Mwagane, alisema hakuridhishwa na uamuzi wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa madai kuwa kitongoji hicho kiko ndani ya kijiji chake kwa muda mrefu.

Alisema hata mwaka 2015 wakati wa uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani kitongoji hicho kilikuwa kinawajibika kwa kijiji chake tofauti na uamuzi uliotolewa.



Mkuu wa Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, Mhandisi Maryprisca Mahundi (mbele), akiwaongoza wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya hiyo, jana, kukagua mipaka ya vijiji vitatu vya Mbugani, Chalangwa na Sangambi ambavyo vilikuwa vinagombea na Kitongoji cha Simba Leaf, kwa miaka sita. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mbeya kujenga sekondari vipaji maalumu

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya, inakusudia kujenga shule maalumu ya sekondari ambayo itakuwa inapokea wanafunzi waliofaulu kutoka kwenye shule za msingi za mchepuo wa Kiingereza zinazomilikiwa na halmashauri hiyo.

Meya wa Jiji hilo, Mchungaji David Mwashilindi, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani ambalo pia lilihudhuriwa na madiwani wa Manispaa ya Iringa ambao walikuwa ziarani kujifunza uendeshaji wa shule za mchepuo wa Kiingereza.

Mwashilindi alisema jiji hilo linamiliki shule mbili za msingi ambazo ni za mchepuo wa Kiingereza na linaendelea na ujenzi wa shule ya tatu ambayo inajengwa katika eneo la uwanja wa ndege wa zamani.

Alizitaja shule ambazo tayari zinafanya kazi kuwa ni Mkapa na Azimio ambazo alisema zinafanya vizuri kitaaluma na akakanusha taarifa zilizokuwa zinazagaa kuwa baadhi ya wazazi wameanza kuwahamisha watoto wao kwenye shule hizo kwa sababu ya kushuka kitaaluma.

Mwashilindi alisema wadhibiti ubora wa elimu wameshathibitisha kuwa shule hizo ni bora, hivyo wataendelea kuimarisha usimamizi wa taaluma ili wazazi wasijutie fedha wanazotoa.

"Lengo letu kwa baadaye ni kuanzisha shule ya sekondari ambayo itakuwa inapokea wanafunzi wetu wanaofaulu kutoka kwenye shule zetu hizi ili kuwa na mwendelezo mzuri, wenzetu wa Iringa lazima tuwaambie ili wasiishie kuziona hizi tulizonazo bali wajuwe na maono tuliyonayo," alisema Mwashilindi.

Alisema shule mpya ambayo inaendelea kujengwa kwa sasa inajengwa na Jeshi la Kujenga taifa (JKT) kikosi cha Itende jijini hapa na kwamba mpaka kufikia Machi, mwaka huu, itakuwa imefikia hatua nzuri.

Baadhi ya madiwani walishauri halmashauri hiyo kutopuuza taarifa za taaluma kushuka katika shule hizo na badala yake wazichunguze taarifa hizo na wakibaini kuwa kuna ukweli, waboreshe kabla hawajafungua shule mpya.

Mmoja wa madiwani hao, Adamu Simbaya kutoka kata ya Mbalizi Road, alisema hata yeye amezisikia taarifa hizo kuwa baadhi ya wazazi wanawahamisha watoto wao hivyo akataka uchunguzi ufanyike. Alisema wakati wanapoendelea kuboresha shule hizo wanatakiwa waepuke kupuuza taarifa za aina yoyote na badala yake wazichunguze kwa ajili ya kupata ukweli na kuutumia kufanya mabadiliko.

"Sisi ndio wa mfano kwenye uendeshaji wa shule hizi na hivyo lazima tuwe makini na taarifa tunazopata, mimi mwenyewe nimepata taarifa kuwa kuna wazazi wanawahamisha watoto wao kwenye shule zetu hasa Azimio kwa sababu ya kushuka kwa elimu," alisema Simbaya.

Hata hivyo, Diwani wa Sisimba, Geofrey Kajigili, alisema wazazi kuwahamisha watoto wao kwenye shule yoyote ni kitu cha kawaida kwa maelezo kuwa kuhamisha watoto kuna sababu nyingi ikiwemo wao wenyewe wazazi kuhamia kwenye miji mingine.

Alisema Shule ya Msingi Azimio bado haijamaliza hata miaka miwili tangu ilipofunguliwa na hivyo ni mapema kuanza kuipima kiwango cha elimu kama kimepanda ama kimeshuka.





# Diwani apiga mkwara wazazi wanafunzi watoro

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

DIWANI wa Chamino jijini Dodoma, Jumanne Ngede, amesema kuwa wazazi na walezi wa watoto wanaosoma shule za msingi na sekondari, ambao ni watoro wataburuzwa mahakamani ili kuwa fundisho kwa wengine wenye tabia kama hiyo.

Ngede, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na wajumbe wa kamati ya bodi ya Shule ya Msingi ya Chinangali kwenye kikao cha kutathmini changamoto mbalimbali zinazokabili shule zilizopo kwenye kata hiyo.

Ngede, alisema hatua ya kuwaburuza mahakamani wazazi na walezi ina lengo la kuziona shule hizo zilizopo kwenye kata hiyo zinafanya vizuri kwenye taaluma na watoto wanaosoma wanafanya vizuri pindi wanapohitimu elimu.

Alisema serikali imewapunguzia makali na mzigo mkubwa kwa upande wa elimu, hivyo hakuna sababu kwa wazazi na walezi kuwafumbia macho watoto wao ambao wamekuwa na tabia ya utoro na wao kushindwa kutoa ushirikiano kwa walimu husika na kamati zilizochaguliwa kwenye shule zao.

"Ili kufika katika ushindani wa kufanya vizuri kitaaluma kwenye wilaya yetu, ni vema wazazi, walezi, walimu na kamati ya bodi ya shule iliyochaguliwa wakawa kitu kimoja ambacho kitakachowezesha kukomesha tabia hii," alisema.

Ofisa Elimu Kata ya Chamwino, Sponsa Mkusa, alisema pamoja na serikali kuwapunguzia baadhi ya mahitaji ya wanayohitaji kwa wanafunzi, bado wana wajibu wa kuhakikisha wanachangia elimu hiyo ikiwamo katika eneo la chakula na mahitaji mengineyo.

Mkusa alisema kuna baadhi ya mahitaji hayahusiani na serikali kama vile ununuzi wa madaftali, chakula na sare ya shule, hivyo ni lazima wazazi na walezi wahusike katika kuhakikisha watoto hao wanasoma vizuri.

# Mradi TGNP wasaidia kuibua vitendo vingi vya ukatili kijinsia

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MRATIBU wa mradi wa kutokomeza ukatili wa kijinsia, unaoratibiwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Zaibabu Mmari, amesema elimu inayotolewa hivi sasa nchini kuhusu masuala hayo, imesaidia kuibua vitendo hivyo tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Mratibu huyo kutoka TGNP Mtandao, alisema hivi sasa jamii imeamka na kuonyesha hali ya kupinga kwa kuviripoti katika vyombo vya dola vitendo hivyo.

Aliyasema hayo jijini Dodoma wakati wa kupata taarifa ya vitendo vya ukatili kutoka kwenye asasi za kiraia zilizopata fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Alisema kuwa lengo la mradi huo ni kuhamasisha watu kuacha vitendo vya ukatili wa kijinsia ambavyo vina madhara makubwa ikiwamo vifo kama hatua za kisheria hazitachukuliwa kwa watu wanaofanya vitendo hivyo.

Alisema taarifa zinaonyesha kwamba hali ya ukatili nchini bado ni mbaya, ingawa kuna baadhi ya mikoa vitendo hivyo vimepungua kutokana na jamii kuelewa kuwa mambo ambayo wanayafanya ni ukatili wa kijinsia.

Mmari aliongeza kuwa utafiti unaonyesha kuwa watu wanaofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia ni wa karibu ikiwamo baba, mama, kaka, dada mjomba na shangazi, hivyo hawawezi kuona kama ni ukatili wanadhani kuwa ni mambo ya kawaida tu.

Alisema baada ya elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto kutolewa mikoa ya Rukwa na Mara vitendo hivyo vimeanza kupungua hasa ukeketaji.

Alisema mradi huo wa kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto unafanywa katika mikoa 16 nchini, ambapo mikoa 13, ipo Tanzania Bara na mikoa mitatu ipo Zanzibar kwenye wilaya zaidi ya 30.

Consolata Chikoti, kutoka kituo cha msaada wa sheria kwa wanawake na watoto, alisema wanajishughulisha na utoaji wa msaada wa kisheria kwa waathirika wa masuala ya ukatili wa kijinsia kwa kuwa wengi hawajui sheria zinazowalinda.

"Serikali hivi sasa inatambua kuwa vitendo vyote vya kikatili nchini ni kosa la jinai hivyo sisi kama wadau wa sheria kazi yetu, kutengeneza mazingira salama kwa waliofanyiwa vitendo hivyo ili waweze kupata haki zao," alisema.

Pia alisema kituo hicho kimeshawasaidia watu wengi waliofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na hatua mbalimbali zimeshachukuliwa kwa wahusika ikiwamo ya kupelekwa mahakamani na wengine kuhukumiwa.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo (katikati), akimkabidhi taarifa ya mafanikio ya miaka minne ya wizara hiyo Mkuu wa Idara ya Huduma za Serikali NMB, Vicky Bishubo (kulia), baada ya kuwasilishwa mwishoni mwa wiki jijini Dodoma. Kushoto ni Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mwita Waitara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC atoa siku saba ujenzi wa machinjio kukamilika

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, ametoa siku saba kwa uongozi wa Jiji la Dodoma kuhakikisha unamaliza ujenzi wa machinjio ya nyama ya mnada wa Msalato yaliozuiwa kutokana na kutokuwa na mfumo wa majisafi na taka.

Machinjio hayo yalifungwa Januari 28, mwaka huu na Bodi ya Nyama, baada ya kukagua na kubaini machinjio ndogo inayotumika haina mfumo wa majitaka na safi, mlango pamoja na uzio kwa ajili ya usafi na usalama wa nyama ambazo zinachinjwa.

Katambi alisema jiji linapaswa kuhakikisha machinjio hayo yanakamilika ili wafanyabiashara wa nyama waendelee na biashara hiyo.

Alisema maamuzi ya Bodi ya Nyama ilifanya uamuzi sahihi licha ya kuwataka kupita ofisi ya mkuu wa mkoa na wilaya kuomba kibali kabla ya kufikia maamuzi ya kufunga.

"Bodi inapaswa kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa au wilaya kushauriana nini kifanyike, kwa sababu unapofunga machinjio unaathiri watu wengi... huu mnada upo toka enzi unapoufungia uwe umejiandaa vizuri ili usiwarudishe nyuma watu wanaotegemea kufanya biashara hiyo ili kuendesha maisha yao," alisema Katambi.

Aliongeza: "Hakuna haja ya kuweka vikwazo katika machinjio ndogo mbadala ambayo imetolewa wakati wanasubiri machinjio kubwa ikamilike inapaswa kuwaelimisha nini kifanyike." Katambi.


Alisema baada ya kuisha jiji iliomba kuongezewa muda wa kuendelea kutumia machinjio ndogo, lakini cha kushangaza Bodi ya Nyama inawazuia.

Awali, ofisa kutoka bodi hiyo, Godfrey Sosthenes, alisema wamekuwa wakifanya ukaguzi katika machinjio na kujiridhisha kuwa eneo hilo linastahiki kufungiwa kutokana na kukosa vigezo.

Alisema wamefungia machinjio hiyo mbadala kutokana na kutokuwa na mfumo wa majisafi na taka, mlango na uzio jambo ambalo si sahihi kisheria.

"Mara nyingi tumekuta mbwa ndani ya machinjio haya kitu ambacho si salama kwa afya ya jamii ndio maana tumefunga machinjio haya," alisema Sosthenes.

Alisema waliamua kufunga machinjio hayo kwa kuzingatia sheria namba 17 ya nyama na magonjwa ambayo inasema lazima watu wazingatie usafi na usalama wa raia katika wanyama wanaowachinja.



# Zanzibar yaandaa maadhimisho wiki ya sheria mara ya kwanza

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KWA mara ya kwanza Zanzibar inatarajiwa kuadhimisha Wiki ya Msaada wa Kisheria ambayo itakwenda sambamba na Siku ya Sheria ili kuimarisha ustawi wa jamii kupitia upatikanaji wa msaada wa kisheria.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Waziri wa Katiba na Sheria Zanzibar, Khamis Juma Mwalimu, alisema maadhimisho hayo yanatarajiwa kufanyika Febuari 7, mwaka huu, na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

Waziri huyo alisema jamii inakabiliwa na changamoto kubwa ya vitendo vya udhalilishaji kiasi ambacho kinaathiri ustawi wa jamii.

Alisema upatikanaji wa haki hasa kwa watu wasiokuwa na uwezo utawezesha kuviangamiza vitendo hivyo na kuwa na ustawi mzuri wa jamii.

Mwalimu alisema katika kuelekea kwenye kilele cha maadhimisho hayo, wizara yake imeandaa shughuli mbalimbali ikiwamo utoaji wa elimu kwa wananchi na kutembelea wafungwa walioko magerezani ili kutoa msaada wa kisheria.

Aidha, alisema katika maadhimisho hayo kutakuwa na uzinduzi wa mfumo wa usajili wa watoa huduma za msaada wa kisheria kwa njia ya kielektroniki na uzinduzi wa sheria ya msaada wa kisheria kwa lugha nyepesi ya Kiswahili.

"Niwaombe kushirikiana nasi katika kuhakikisha wananchi wetu wanapata taarifa sahihi juu ya upatikanaji wa msaada wa kisheria katika nchi yetu," alisema.

Waziri huyo alisema kuna baadhi ya wananchi wanyonge haki zao zinapotea kwa sababu ya unyonge wao, hivyo utoaji wa elimu utasaidia kupata haki zao.

Kuanzishwa kwa idara ya msaada wa kisheria, alisema ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi na utawala bora kuona wananchi wanapata ufumbuzi wa matatizo yanayohusu sheria.

Alisema changamoto iliyokuwa ikiwakabili wananchi kwa muda mrefu ni tatizo la msaada wa kisheria katika vyombo vya sheria ikiwamo Mahakama.

Alibainisha kuwa wananchi wanakabiliwa na kesi ambazo ufumbuzi wake ni mwepesi wa kupata msaada wa kisheria, lakini hakuna taasisi au jumuiya yenye uwezo wa kufanya kazi hiyo.

"Tumeunda idara ya huduma za msaada wa kisheria kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kupata ufumbuzi wa mashauri yao ikiwamo wafungwa walioko magerezani na watuhumiwa wengine," alisema.

Aidha, alisema katika Wiki ya Huduma za Msaada wa Kisheria, wananchi wanatakiwa wajitokeze kwa wingi kupata huduma za kisheria kwa kutaja shida na changamoto mbalimbali zinazowakabili ikiwamo kesi.

"Hii ni fursa adhimu sana ambapo wananchi wanatakiwa kuitumia kwa ajili ya kupata msaada wa kisheria katika masuala mbalimbali ikiwamo madai na mashauri yaliyoko mahakamani," alisema.



Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Raya Issa Msellem, akizungumza na waandishi wa habari Chukwani Zanzibar jana, kuhusu kuanza kwa Mkutano wa 17 wa Baraza la Wawakilishi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Maswali 112 kuulizwa BLW

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKUTANO wa 17 Baraza la Wawakilishi Zanzibar unatarajiwa kuanza Februari kesho na utakuwa na maswali 112.

Katibu wa Baraza hilo, Raya Issa Msellem, alisema jana kuwa katika mkutano huo itasomwa kwa mara ya pili na kujadiliwa miswada ya sheria ambayo iliwasilishwa katika kikao kilichopita.

Alisema miswada hiyo ni pamoja na wa sheria ya kufuta sheria ya mawakili sura ya 28 na sheria ya wakuu wa viapo sura ya 29 na kutunga sheria ya mawakili na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Raya alisema muswada mwengine ni wa sheria ya kuweka masharti yanayohusiana na haki na huduma za ustawi wa wazee na kuanzisha mpango wa pensheni jamii, usimamizi wake na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Aidha, alisema katika mkutano huo kutawasilishwa ripoti za kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2019/20.

Pia alisema kutawasilishwa taarifa ya dawa za kulevya kwa mwaka 2018 na mwelekeo wa mpango wa taifa.

Kwa zaidi ya wiki mbili, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao ni wajumbe wa kamati za baraza walikuwa katika ziara kwenye taasisi mbalimbali Unguja na Pemba pamoja na Tanzania Bara kuona utendaji wa shughuli za kazi.

Raya alisema katika kikao hicho Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, anatarajiwa kuwasilisha mwelekeo wa mpango wa taifa kwa mwaka 2020-2021 mbele ya Baraza la Wawakilishi.

Mpango huo utatoa mwelekeo wa bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2020-2021 na kutaja vipaumbele vya serikali vinavyotarajiwa kutekelezwa.

# Upanuzi wa uwanja kukuza uchumi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KUKAMILIKA kwa ujenzi wa jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (Terminal III) utasaidia ukuaji wa mapato ya nchi.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohammed Ramia Abdiwawa, alipofanya ziada ya kukagua jengo hilo ambalo ujenzi wake unaendelea.

Alisema lengo la serikali ni kuona shughuli za maendeleo zinaimarika na kupata mafanikio katika sekta mbalimbali.

Alisema wakati wa bajeti iliyopita, walitangaza kipaumbele kikubwa ni uwanja huo kumalizika kwa wakati ambapo matarajio ni mwaka huu.

Balozi Ramia alisema katika uwanja huo, wametenga Sh. bilioni 61 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la abiria makandarasi kutoka kampuni ya BCEJ wameahidi kazi hiyo kukamilika Juni, mwaka huu.

Aidha, alisema lengo la ziara hiyo ni kuona maendeleo ya uwanja huo. Awali kazi ilikuwa inadorora lakini kwa sasa inaendelea vizuri na vifaa vipo vya kutosha kwa ajili ya ujenzi huo.

Kutokana na kasi hiyo, Balozi Ramia alisema ameridhishwa na shughuli za ujenzi katika uwanja huo na kuwataka wakandarasi kukamilisha kwa wakati ili lengo lilokusudiwa liweze kufikiwa.

Naye Waziri wa Mawasiliano na Usafirishaji, Dk. Sira Ubwa Mamboya, alisema wizara inaendelea kuchukua juhudi mbalimbali za kuhakikisha ujenzi huo unakamilika na kuleta mafanikio.

Pia alisema kwa sasa changamoto iliyoko katika ujenzi huo ni mvua ambayo imekuwa ikinyesha bila mpango na kuathiri mtiririko wa kazi.

Meneja anayesimamia uwanja huo, Yassir Dikosta, alisema kazi ilipoanza ilikuwa na changamoto mbalimbali ambapo kwa sasa wamejipanga na mkandarasi kufanya kazi hiyo saa 24 ili kuona kazi hiyo inakamilika kwa wakati.

# 77 mbaroni tuhuma za uhamiaji haramu

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WAHAMIAJI haramu 77 kutoka katika mataifa mbalimbali wanashikiliwa na Idara ya Uhamiaji mkoani Mbeya kwa kosa la kuingia na kufanya kazi nchini.

Mkuu wa Idara ya Uhamiaji wa Mkoa wa Mbeya, Naibu Kamishna wa Jeshi la Uhamiaji, Shaaban Hatibu, alisema wahamiaji hao walikamatwa wakati wa operesheni maalumu iliyofanyika wiki nzima.

Alisema operesheni hiyo ilifanyika kwenye mashamba makubwa ya wawekezaji, migodini, vituo vya mabasi, kwenye taasisi mbalimbali pamoja na kwenye makazi ya wananchi hasa katika Wilaya za Chunya na Mbeya.

Alisema baadhi ya wahamiaji hao walikutwa wakiwa hawana vibali na wengine wanavyo, lakini walikuwa wanavitumia vibaya ambapo hakufafanua namna walivyokuwa wanavitumia vibali vyao kwa madai kuwa kwa sasa ni siri.

Alisema kati ya wahamiaji hao, 52 ni Wamalawi, Waethiopia 10, Wamarekani wawili, Wahindi wawili, Mchina mmoja, Mkenya mmoja, Msomali mmoja, Mzambia mmoja na mmoja kutoka nchi ya Ireland.

"Hawa tutawachukulia hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kurejeshwa nchini mwao, wengine tutawafikisha mahakamani na wengine tutawatoza faini kwa mujibu wa sheria," alisema Hatibu.

Alisema kwa mujibu wa sheria, watuhumiwa wanaostahili kulipa faini watatakiwa kulipa Dola za kimarekani 600 kila mmoja.

Alieleza kuwa katika operesheni hiyo, Watanzania sita pia walikamatwa kutokana na kuwasaidia wahamiaji hao kuingia nchini na wengine walikuwa wamewaajiri.

Aliwataka Watanzania kuepuka kuwasaidia wahamiaji hao kuingia nchini kwa maelezo kuwa vitendo hivyo vinahatarisha usalama wa taifa kutokana uwapo wa baadhi ya magonjwa ya mlipuko kwenye mataifa hayo ambayo yanaweza yakasambaa nchini. Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alimwagiza Mkurugenzi wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya kutuma wataalamu kwenda kupima afya za wahamiaji hao kabla ya kuwachanganya na mahabusu wengine ili kuepuka kusambaa kwa magonjwa.

Ntinika alisema nchi inachukua tahadhari ya mlipuko wa virusi hatari vya corona ambavyo vimeua watu nchini China na mataifa mengine ya Bara la Asia.

"Nimeshawasiliana na Mkurugenzi wa Hospitali yetu ya Kanda, Dk. Godlove Mbwanji, ameshaniambia tayari wataalamu wanakuja hapa, hakikisheni wote wanapimwa kwa sasa kuna magonjwa ya hatari ambayo kama taifa lazima tuchukuwe tahadhari," alisema Ntinika.

Aidha, aliwataka wahamiaji hao wakisharejeshwa kwenye mataifa yao wasithubutu tena kuingia nchini bila kufuata taratibu za kisheria ikiwamo kuwa na vibali.

# Sukari guru kuzalisha nishati pombe ya kupikia vyakula Dar

**Na Gaudensia Mngumi**

KAZI za kibunifu zinazofanywa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali likiwamo Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO), zinaanzisha mpango wa kutumia sukari guru kuzalisha nishati ya kupikia nyumbani.

Mradi huo unatarajiwa kuanzia Dar es Salaam ili kupunguza matumizi makubwa ya mkaa na kuni, unaoteketeza maelfu ya hekari za misitu nchini.

Hayo yalibainika mwishoni mwa wiki iliyopita jijini Dar es Salaam wakati Ofisi za Umoja wa Mataifa (UN), Mtandao wa Ubunifu wa UN (UNIN) na Kituo cha Ubunifu cha Mpango wa Chakula wa Duniani (WFP), ulipoandaa usiku wa ubunifu wa mashirika ya UN nchini na kuonyesha kazi mbalimbali na jinsi ubunifu ulivyo mwarobaini wa kumaliza changamoto za jamii.

Victor Akim, kutoka UNIDO, akielezea ubunifu wa kuhamasisha kutumia sukari guru kutengeneza nishati mbadala ya kupikia nyumbani alisema mradi utatumia guru (molasesi) kutengeneza pombe ('bioethanol') na kwamba majaribio yanaanzia Tabata na Ilala kwa kusambaza majiko 110,000 kwa kaya za eneo hilo kwa majaribio.

"Ubunifu na teknolojia hii unalenga kushirikiana na sekta binafsi wazalishaji wa sukari kutumia molasesi kutengeneza bioethanol -nishati mbadala. Lakini siyo sukari guru pekee tunalenga pia kutumia mabibo ya korosho na mabaki ya katani" anaeleza Akim alipowasilisha wazo la ubunifu kutoka UNIDO.

Kaimu Mratibu, Mkazi wa UN na Mwakilishi wa WFP nchini, Michael Dunford, akizungumza kwenye usiku wa ubunifu alisema:

"Mazoea ya kutekeleza majukumu kwa njia zilizozoeleka hautatusaidia kufikisha kwenye malengo ya maendeleo endelevu (SDG) yatupasa kuwa wabunifu, kufikiria ufumbuzi wa changamoto za siku zijazo na kutoogopa kujaribu mambo mapya."

Dunford alihimiza utamaduni na kujenga mazingira wezeshi ya kuleta ubunifu na kufanya mambo mapya akisema ni muhimu katika kuibua njia mpya za utendaji katika UN. Ili kufanikisha azma hiyo mashirika mengi ya UN yameunda timu za kuhamasisha ubunifu kidunia na katika mataifa wanapofanyia kazi.

Alisema kwa UN Tanzania harakati za ubunifu zinaendeshwa na Kituo cha Ubunifu cha WFP na Mtandao wa Ubunifu wa UN -UNIN na kwamba kupitia safari ya ubunifu maofisa 30 kutoka mashirika 11 ya UN wamejifunza na kutumia njia mbalimbali za ubunifu zilizoainisha kikamilifu njia bora za kutatua matatizo kama vile, kuibua mbinu za kufanya mawasiliano yenye ufanisi zaidi na wadau na wahisani wa UN. Je, tutafanya nini ili kupata nishati endelevu kwa ajili ya watu wanaoishi katika kambi za wakimbizi?



Magari yakipita kwa taabu katika eneo la Kizuiani Kitunda, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, kutokana na barabara kuharibiwa vibaya na mvua zinazoendelea kunyesha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mafundi wanaochelewesha kituo afya waandaliwa dawa

**Na Gurian Adolf, KALAMBO**

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Josephat Kandege, amewaagiza watendaji wa serikali waliopo Kata ya Samazi wilayani Kalambo mkoani Rukwa, kuwachukulia hatua za kisheria baadhi ya mafundi wanaodaiwa kukwamisha ujenzi wa kituo cha afya Samazi.

Mafundi hao wanadaiwa kugoma kufanya kazi kwa madai kuwa fedha wanazolipwa kutokana na kazi hiyo kuwa ni ndogo.

Agizo hilo alilitoa mwishoni mwa wiki alipokuwa katika ziara ya kikazi na kutembelea eneo ambalo ujenzi wa kituo hicho unafanyika na kupewa taarifa kuwa kuna baadhi ya mafundi wamekuwa kikwazo cha maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho cha afya kwa kugoma kufanya kazi kwa madai kuwa fedha wanazopata kutokana na malipo ya kazi hiyo ni kidogo.

Kandege ambaye ni Mbunge wa Kalambo, alisema kuwa wananchi wa jimbo hilo wameshakubaliana kuwa yeyote atakayekwamisha ujenzi wa kituo hicho ni lazima achukuliwe hatua, ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Alisema kuwa ni vizuri kila mwananchi akashiriki kikamilifu katika ujenzi huo wa kituo cha afya kwani kitatatua changamoto zinazo wakabiri za kutembea umbali mrefu kwa ajili ya kutafuta huduma za afya.

Kwa upande wake mhandisi wa halmashauri hiyo, Daud Sebiga, alisema kuwa ujenzi wa kituo hicho unatarajiwa kukamilika ndani ya siku 90.

Alisema kuwa mpaka sasa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo imeshapokea fedha kiasi cha Sh. milioni 400 kutoka serikali kuu ambazo zitatumika kukamilisha ujenzi ndani ya siku 90 ya majengo matatu ambayo yatatumika katika kituo hicho cha afya.

Naye Juma Kibongwe, Diwani wa Kata ya Samazi aliishukuru serikali kwa niaba ya wananchi wa kata hiyo kwa kutoa fedha hizo, na kueleza kwamba ujenzi wa kituo hicho cha afya utakapokamilika utawaondolea kero wanazokutana nazo wanapokuwa wagonjwa.

Ujenzi wa Kituo cha Afya Samazi ulianza tangu Juni 2019, baada ya serikali kutoa shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi huo, lakini umekuwa ukisuasua kutokana na kuibuka kwa mvutano wa eneo gani kijengwe kituo hicho.

Hivi sasa kuna changamoto ya baadhi ya mafundi kususia kazi kwa madai kuwa fedha wanazolipwa baada ya kufanya kazi za ujenzi kuwa ni ndogo, hali inayokwamisha kasi ya ujenzi huo.

**HABARI KIMATAIFA**

## China yaituhumu Marekani kuhusu virusi corona

**BEIJING,** China

CHINA imeituhumu Marekani kueneza taharuki kuhusu virusi vya corona badala ya kutoa msaada wa kukabiliana na ugonjwa huo ambao tayari umesababisha vifo vya watu 362.

Wizara ya Mambo ya Nje ya China imesema Marekani haijatoa msaada wowote wa manufaa zaidi ya kusambaza hofu ikiwa ni pamoja na kuwapiga marufuku wasafiri wa Kichina kuitembelea nchi hiyo.

Mwishoni mwa wiki iliyopita Marekani ilitangaza dharura ya kiafya pamoja na marufuku ya muda ya kuingia nchini humo kwa raia wa kigeni waliokuwa China kwa lengo la kudhibiti kusambaa kwa mlipuko wa virusi hivyo.

Hadi sasa watu 17,000 wameambukizwa virusi vya corona na tayari vimesambaa kwenye mataifa 24 licha ya serikali nyingi kuweka marufuku ya kuingia kwa watu wanaotoka China.

Wakati huohuo, mawaziri wa afya wa nchi zenye uwezo mkubwa wa viwanda duniani liitwalo G7 wanatarajia kukutana kujadiliana kuhusu virusi vipya vya corona.

Mkutano huo utafanyika kwa njia ya mawasiliano ya simu kwa mujibu wa Wizara ya Afya ya Italia.

Hadi Jumapili idadi ya vifo kutokana na virusi hivyo nchini China ilikuwa ni 361. **DW**

## Kagame, Museveni kubadilishana wafungwa

**LUANDA,** Angola

NCHI za Rwanda na Uganda zimekubaliana kubalishana wafungwa ikiwa ni mojawapo ya njia ya kuimarisha tena uhusiano kati ya nchi hizo mbili jirani.

Hatua hiyo ilifikiwa baada ya mkutano kati ya Rais wa Uganda, Yoweri Museveni na Rais wa Rwanda, Paul Kagame, uliofanyika juzi Luanda, nchini Angola, na kushuhudiwa pia na mwenyeji wao Joao Lourenco, na Felix Tshisekedi wa DRC.

Hata hivyo, haijafahamika ni lini wafungwa hao kutoka nchi hizo mbili wataachiliwa huru, huku wakikubaliana pia kuachana na vitendo vinavyoweza kurudisha nyuma juhudi za kupata amani ya kudumu.

Makubaliano ya kuondoa uhasama kati ya Rwanda na Uganda yaliyosainiwa na marais wa nchi hizo mbili, Agosti 2019, jijini Luanda nchini Angola yalileta afueni na furaha kubwa kwa raia wa nchi hizo, hususani wafanyabiashara.

Uganda imekuwa ikiishtumu Rwanda kwa kutumia raia wake kuhatarisha usalama wake, huku Rwanda nayo ikiishtumu Uganda kwa kuwatesa na kuwazuia raia wake, suala ambalo lilisababisha Kigali kufunga mpaka wake wa Katuna. **RFI**

# Nzige Somalia wasababisha kutangazwa hali ya dharura

**MOGADISHU,** Somalia

SOMALIA imetangaza hali ya dharura kutokana na kuenea kwa kundi kubwa la nzige katika eneo la Afrika Mashariki.

Waziri wa Kilimo nchini humo, Said Hussein Lid alisema kuwa wadudu hao wameonekana kuwa tishio kwa kuwa tayari wameshambulia mimea mingi ya chakula na kufanya hali ya usalama wa cha chakula Somalia kuwa hatarini.

Alisema kuna hofu kuwa hali hiyo inaweza kushindwa kudhibitiwa kabla ya muda wa mavuno mwezi Aprili.

Umoja wa Mataifa (UN) umesema kuwa uvamizi wa nzige wengi haujawahi kutokea katika nchi za Somalia na Ethiopia kwa miaka 25.

Nalo Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), limesema kuwa nchi jirani ya Kenya, haijawahi kukutana na shambulizi la nzige kiasi hicho kwa kipindi cha miaka 70 iliyopita.

**FAO iliwahi kutoa wito wa kutolewa kwa msaada ili kukabiliana na athari za nzige kama vile ukosefu wa chakula, utapiamlo na kuathirika kwa mfumo wa maisha ya kila siku.**

Ingawa Somalia imekuwa nchi ya kwanza kutangaza kuwa na hali ya dharura lakini haiwezi kutumia dawa ya kunyunyizia kwa kutumia ndege ili kuua wadudu hao.

UN imetoa wito wa usaidizi wa kimataifa kukabiliana na nzige wengi waliovamia maeneo ya Afrika Mashariki.

FAO iliwahi kutoa wito wa kutolewa kwa msaada ili kukabiliana na athari za nzige kama vile ukosefu wa chakula, utapiamlo na kuathirika kwa mfumo wa maisha ya kila siku.

Vilevile liliwahi kueleza kuwa nchi za Ethiopia, Kenya na Somalia ziko katika wakati mgumu kukabiliana na makundi ya nzige.

Shirika hilo linahofia kwamba idadi ya nzige hao huenda ikaongezeka mara 500 zaidi ifikapo Juni mwaka huu.

Nzige hao wamesambaa kuanzia Yemen hadi maeneo mengine ya Bahari ya Shamu. Kiwango kikubwa cha mvua mwishoni mwa 2019 kilitengeneza mazingira mazuri yanayochangia uwepo wa wadudu wao.

Mbali na nzige hao kuongezeka maeneo ya Afrika Mashariki, pia wamejitokeza katika nchi za India, Iran na Pakistan, ambao huenda wakabadilika na kuanza kusambaa ifikapo msimu wa mvua.

Nzige wanaweza kusafiri umbali wa kilomita 150 (maili 93) kwa siku na kila nzige mkubwa anaweza kula chakula kingi kwa siku.

Mwezi uliopita kundi la nzige lililazimisha ndege ya abiria nchini Ethiopia kubadili safari yake. Wadudu hao waliingia kwenye injini, kioo na sehemu ya mbele ya ndege, na kulazimika kutua katika Uwanja wa Ndege wa Addis Ababa. **BBC**



Wananchi wa Malawi wakishangilia baada ya jana Mahakama ya kikatiba nchini humo kutengua matokeo ya urais yaliyomuweka madarakani Mutharika. **PICHA: MTANDAO**

## Raia wapewa silaha kupambana wanamgambo

**OUAGADOUGOU,** Burkina Faso

MAOFISA nchini Burkina Faso wamewapatia wananchi silaha kama dawa ya kukabiliana na ongezeko la mashambulio ya wanamgambo wa Kiislamu yanayoongezeka.

Serikali ya Burkina Faso inakabiliwa na shinikizo la kuchukua hatua kujaribu kudhibiti wanamgambo.

Katika kipindi cha Januari watu wapata 60 waliuawa katika mashambulio manne tofauti kaskazini mwa nchi hiyo.

Hivi karibuni wabunge nchini humo walipiga kura kwa kauli moja kuunga mkono kuwapatia raia silaha, hatua ambayo walisema itasaidia kupambana na makundi yenye silaha. Inatarajiwa kusainiwa kuwa sheria.

Mashambulio ya wanamgambo wenye uhusiano na makundi ya al-Qaeda na Islamic State yameongezeka kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita na kusababisha zaidi ya watu milioni moja kuyakimbia makazi yao.

Wakosoaji wamehoji ikiwa raia wakipewa silaha itasababisha vifo vingi lakini serikali inasisitiza kuwa watu watakaojitolea kuwa na silaha ni muhimu kwani watasaidia kumaliza kusambaa kwa ghasia.

Sheria inasema kuwa uwezo wa jeshi wa kupambana na wanamgambo hautoshi kutokana na idadi yao kuwa ndogo na kuna ukosefu wa mafunzo yanayofaa.

Waziri wa Mawasiliano, Remi Dandjinou alisema: “Kwa sababu ya tishio linaloendelea, watu wameelezea utashi wao wa kushiriki kikamilifu katika kuilinda nchi yao,” ilisema. Alisema huo siyo ushahidi wa udhaifu wa jeshi na kwamba watakaojitolea kupewa silaha kama kikosi cha kujilinda cha Ufaransa kilichokuwapo wakati wa uvamizi wa Ujerumani wakati wa vita kuu ya Pili ya Dunia.

Lakini kuna hofu kwamba hatua mpya kuchoche zaidi mzozo wa kikabila na kuchochea uhasama baina jamii za wawindaji na wakulima.

“Inaweza kuchochea uhasama wa kijamii na kusababisha ukiukaji mkubwa haki za binadamu, ambao unaweza kuwasukuma zaidi watu kuingia mikononi mwa makundi ya Jihad,” alisema Dandjinou.

Serikali ya Burkina Faso awali ilikana madai ya kuenea kwa ukiukaji wa haki za binadamu.

Alisema raia yoyote mwenye umri wa miaka 18 na zaidi anaweza kukubaliwa kupewa mafunzo na hakuna umri wa ukomo. Lakini kupewa mafunzo haiwezi kuwa ni sehemu ya kundi lolote la kisiasa. **BBC**

# Serikali yaendeleza msimamo uraia pacha

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa suala la uraia pacha ni la kikatiba na kwamba mchakato wa kubadili katiba bado unaendelea.

Hayo yalielezwa na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje ya Nchi na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro, alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Restuta Mbogo.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema sheria ya uraia inakata uraia pacha na kuhoji serikali lini itaruhusu uraia huo.

"Serikali mwaka 2014 ilitoa uraia kwa wageni waliokuwa wanaishi kama wakimbizi 150,000 nchini Tanzania, je, serikali haioni kutoruhusu uraia pacha kunawanyima fursa Watanzania wanaoishi nje ya nchi kuja kuwekeza?" Alihoji.

Akijibu, Dk. Ndumbaro alisema pale katiba itakapobadilika na kuruhusu uraia pacha ndipo watabadili Sheria ya Uraia Namba 6 ya Mwaka 1995 ili kuongeza kipengele cha kuruhusu uraia pacha.

Alieleza kuwa Watanzania wanaoishi nje ya nchi, wanaendelea kufurahia fursa zilizotolewa nchini ikiwamo haki ya kuwekeza na haki nyingine.

Katika swali la msingi, Mbogo alisema Watanzania wengi wanaoishi nje ya nchi wamejikuta ni raia wa nchi wanazoishi kwa sababu mbalimbali ikiwamo kazi lakini si kwamba hawaipendi Tanzania.

"Je, serikali ina mpango gani wa kuwatambua Watanzania waliochukua uraia wa nchi nyingine ili kukuza uchumi wa nchi na kusaidia ndugu zao?" Alihoji.

Akijibu, Dk. Ndumbaro alisema idara ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi wanakadiriwa kuwa zaidi ya milioni moja na wanamiliki akaunti kwenye taasisi mbalimbali za kifedha na ni wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii.

Alieleza kuwa pia wanamiliki nyumba 169 ambazo zimeuzwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) zenye thamani ya Sh. bilioni 5.5 hadi kufikia Februari , mwaka 2019.

Naibu waziri huyo alisema serikali imeendelea kusimamia masuala ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi bila kubagua ikiwamo waliochukua uraia wa nchi nyingine ili kuhakikisha mahitaji yao yanashughulikiwa.

"Wizara imeweka mikakati ya kuwatambua na kuhakikisha diaspora wanashiriki katika kukuza uchumi na mikakati yao ni pamoja na kuhimiza kujisajili kwenye balozi zetu na maeneo ya wakilishi, kuratibu makongamano ya diaspora ndani na nje ya nchi," alisema.

Aidha, alisema Watanzania hao wameleta mafanikio makubwa kwa ndugu zao na Taifa kwa ujumla kwa kuchangia sekta ya afya, ambapo serikali imekuwa ikipokea wataalamu wa afya wa magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza.

"Novemba 2019 tulipokea vitabu vya afya vya Sh. milioni 30," alisema.




Mwenyekiti wa Chama cha Wahasibu Tanzania (TAA), Peter Mwambuja, akizungumza na wanahabari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu Wiki ya Uhasibu, itakayoadhimishwa Machi 9 hadi 14, mwaka huu. Kulia ni Makamu Mwenyekiti wa TAA, Odemari Rushita na Mkurugenzi wa Miradi na Mipango, Ezekiel Stephen. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waziri Kamwelwe aifunda MAB

**Na Bahati Mollel,** TAA

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isaack Kamwelwe, ameiasa Bodi ya Ushauri ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (MAB), kutanguliza utaifa na uzalendo mbele katika majukumu yake.

Kauli hiyo aliitoa mwishoni mwa wiki katika halfa ya uzinduzi wa bodi hiyo jijini Dar es Salaam.

"Napenda kutumia nafasi hii kuwaasa kwamba nafasi hizi mlizopewa ni kwa ajili ya kulitumikia Taifa letu kwa weledi, uaminifu na uadilifu mkubwa huku mkitanguliza maslahi mapana ya taifa na uzalendo mbele," alisema Waziri Kamwelwe.

Pia Waziri Kamwelwe aliitaka bodi hiyo kuhakikisha inashirikiana na menejimenti ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), na taasisi za serikali hususan Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) katika ujenzi wa viwanja lengo ya kuviongeza ili ndege za Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) na mashirika mengine yaweze kupanua wigo wa safari.

Kadhalika, alisema ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege ukaimarishwe, ingawa bado kuna changamoto ya kukosekana kwa uzio wa ndani na nje ya viwanja vya ndege, na kuwa suala la ugonjwa wa homa ya virusi vya corona ulioanzia China lipewe kipaumbele kwa kuzingatiwa maslahi mapana ya taifa yazingatiwe.

"Hili la ugonjwa wa corona liangaliwe kwa ukaribu zaidi ili viwanja vya ndege visiwe ndio njia ya kuingiza ugonjwa huu, pia usalama wa watendaji kazi uangaliwe," alisema na kuongeza:

Bodi hiyo inaundwa na Mwenyekiti Dk. Masatu Chiguma na wajumbe ni Mhandisi Ven Kayamba, Dk. Paschal Mugabe, Mhandisi Daniel Kiunsi, Mhandisi Christopher Mukoma na Alex Haraba.

Mkurugenzi Mkuu wa TAA, Mhandisi Mshauri, Julius Ndyamukama, alisema Mamlaka hiyo imekuwa ikikua tangu kuanzishwa kwake hadi sasa, na kutolea mfano wa mapato kuongezeka kutoka shilingi bilioni 6.3 hadi kufikia bilioni 105.2 kwa mwaka, ambalo ni sawa na ongezeko la asilimia 1,570.

Naye Mwenyekiti wa MAB, Dk. Masatu Chiguma, alimuahidi Waziri kuwa atafanya kazi kwa kushirikiana na TAA, ili kufanikisha malengo yaliyowekwa.

# Sakata la Mwamposa hatimaye latua rasmi bungeni

INATOKA UK. 2

pamoja na kanuni za Bunge ili kuipa nguvu na kuungwa mkono na wabunge.

Akijenga hoja hiyo upya alisema: "Kwa kutumia kanuni ya 47 pamoja na ile ya 48, naomba nitaisoma kuhusu jambo la dharura na nitaomba kuanza na suala lililotokea kule mkoani Kilimanjaro," alisema.

Mbatia ambaye ni mtaalamu wa majanga nchini, alisema suala la mkusanyiko ambalo limesababisha vifo vya watu 20, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ibara ya 19, fasili ya tatu inasema hifadhi ya haki zilizotajwa katika ibara hii inakuwa chini ya taratibu zilizowekwa na sheria mbazo ni muhimu katika jamii ya kidemokrasia kwa ajili ya usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii na umoja wa kitaifa.

Alisisitiza kuwa amelazimika kurejea Katiba kwa sababu majanga ambayo yanatokea pamoja na matakwa ya sheria na ukizingatia majanga hayo kwa asilimia 96 yanasababishwa na binadamu ni vyema wakaliwekea utaratibu mzuri wa kuleta umoja, kwa kuwa mauaji ya namna hiyo yanaweza yakatokea kama yalivyotokea kwa Kibwetere.

"Kwa kuwa madhehebu ya dini hapa nchini sasa uratibu wake katika kuhudumia au kutoa huduma zake limekuwa ni suala very sensitive (jambo nyeti) ni vyema sisi kama taifa au wabunge tukaisimamia serikali vizuri na tukaweka utaratibu mzuri wa kuleta umoja, kwa sababu mauaji ya namna hii yanaweza yakatokea kama yalivyotokea ya Kibwetere. Sasa naomba kutoa hoja."

Kutokana na uhitaji huo wa wabunge kutaka mjadala, Spika Ndugai alisema hoja hiyo ya Mbatia ni hoja ya msingi sana, lakini hawawezi kuendelea nayo kwa sababu haikuungwa mkono.

**Kwa kutumia kanuni ya 47 pamoja na ile ya 48, naomba nitaisoma kuhusu jambo la dharura na nitaomba kuanza na suala lililotokea kule mkoani Kilimanjaro.**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**ANAHITAJIKA MUUGUZI**
Anahitajika muuguzi msaidizi au Nurse Assistant kwa anayehitaji **Apige: SImu Namba: 0786 641903 au 0716 172929**

**MKOPO WA HARAKA NA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL)** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumaliza tenda etc. Kwa maelezo zaidi piga: **0758 112 332. Karibu EFL**


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**


### KUPOTEA KWA CHETI



115613402

**Joyce Alphonce Lyimo** anatangaza kupotea kwa cheti Ualimu Daraja A chenye namba usajili **CUK 0203** kilichotolewa na Chuo cha Ualimu Kibamba 2013 katika Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chcochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/OST/RB/103741/2020**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MELCHADES CHARLES LWAMLEMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA MARK 11** yenye na za usajili **T 557 DEK** Chassis No. **GX1106047587,** Engine **No.1G2801287.** yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **DODO/DOD/RB/98046/2020.**

215613802

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMISSION CAUSE NO. 5 2020**

**In the matter of the Estate of the late Kedmon Ezekiel Msonjela of Chilolo, kikombo Area within Dodoma Region And**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY REHEMA OBERD MSONJELA.**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 Probate Rules Gn 369 of 163)**

All persons claiming to ha e any interest in the Estate of the above nambed deceased are hereby cites to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above nambed petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **7th Day of February 2010.**
**Date at Dodoma 8th Day of Jan 2020**
**Prented for fillings this 30th Jan 2020**

RESIDENT MAGISTRATE

215614202

### KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**SAIDI HASSANI MATOLA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya Toyota IST yenye namba ya usajili **T870 DSQ** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi
Polisi Taarifa
**DAR/OST/RB/79821/2020**

115613902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;22/2020**

**Ombi la JUMA RAMADHANI SAID Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu RAMADHANI SAID MATEMELELA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 03/02/2020.

Tarehe 03/2/2020
Sahihi ya Hakimu
MOROGORO

115614102

### KUPOTEA KWA CHETI



115613302

**Michael Mathias Mushi** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye chenye index namba **NS 3078/0035** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Tanzania mwaka 2013 katika Shule ya Sekondari Oria.. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chcochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KW/BI/i/VOL68/2020**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;22/2020**

**Ombi la JUMA RAMADHANI SAID Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu RAMADHANI SAID MATEMELELA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 03/02/2020.

Tarehe 03/2/2020
Sahihi ya Hakimu
MOROGORO

115614102



***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***



**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# GUARDIOLA: LIVERPOOL HAIZUILIKI UBINGWA EPL



**MANCHESTER,** England

HATIMAYE Pep Guardiola amekiri Liverpool haizuiliki tena katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya England baada ya Manchester City ikiwa na wachezaji 10 uwanjani kukubali kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Tottenham Jumapili.

Mabingwa watetezi, City sasa wamepitwa pointi 22 na 'Wekundu' hao baada ya mabao ya Steven Bergwijn na Son Heung-min kuwapa ushindi Spurs.

Penalti ya Ilkay Gundogan katika kipindi cha kwanza iliokolewa na golikipa Hugo Lloris na Oleksandr Zinchenko alitolewa nje kabla ya Bergwijn kufunga bao la kwanza kwenye uwanja huo wa Tottenham Hotspur.

Guardiola anaona kwamba hakuna matumaini ya kikosi chake kutetea ubingwa wa ligi hiyo baada ya kubakiwa na mechi 13 kabla ya ligi hiyo kumalizika, huku sasa akili yake akiielekeza kwenye mbio za Ligi ya Mabingwa Ulaya, Kombe la FA na lile la EFL.

Bosi huyo wa City, ambaye alikaa na wachezaji wake zaidi ya dakika 50 kwenye vyumba vya kubadilishia nguo baada ya kipigo hicho alisema: "Wako mbali sana na sisi kwa hiyo hatuwezi kuwazuia. Wana pointi nyingi, tumepoteza pointi nyingi leo.

"Malengo yetu ni kushinda mashindano yaliyobaki na kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa msimu ujao."

# Rakitic: Sikutendewa haki na Valverde Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

IVAN Rakitic amebainisha kwamba alifikiria kuondoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Barcelona, Januari mwaka huu kutokana na kutotendewa haki na benchi la ufundi.

Rakitic alikuwa akihusishwa na mpango wa kwenda kwa miamba wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Juventus na Inter Milan kabla ya dirisha la usajili kufungwa, huku Manchester United pia ikiripotiwa kumtaka.

Pia ikaripotiwa kwamba, Rakitic alipewa ofa ya kujiunga na Paris Saint-Germain katika dili ambalo lingemhusisha Neymar kurudi pale Camp Nou mwanzoni mwa msimu.

Baada ya ushindi wa Jumapili wa 2-1 dhidi ya Levante, mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia, Rakitic alibainisha hali ilivyokuwa.

"Nilifikiria kuhusu kuondoka wakati wa dirisha la Januari," alisema Rakitic, ambaye alicheza mchezo wote, akiwaambia waandishi wa habari.

"Nilikuwa sitendewi haki na benchi la ufundi la kocha wa zamani Ernesto Valverde.

"Ulikuwa wakati mbaya, lakini sasa yamepita. Naweza kusema kwa uwazi kabisa kulikuwa na mambo ambayo sikuyapenda."

Ansu Fati alifunga mara mbili kuiwezesha Barca kupata ushindi huo na sasa imepitwa pointi tatu na vinara Real Madrid baada ya mechi 22.

Rakitic amecheza mechi 16 za LaLiga msimu huu na jumla ya mechi 24 kwenye mashindano yote.





# *Ronaldo atakata rekodi Juventus*

**RIN,** Italia

CRISTIANO Ronaldo alifunga penalti mbili na kufikisha idadi ya mabao 10 katika mechi sita zilizopita wakati Juventus ikiifunga Fiorentina mabao 3-0.

Wenyeji hao awali walipewa penalti baada ya mpira wa kunawa kipindi cha kwanza na Ronaldo akaifunga.

Rodrigo Bentancur alifanyiwa madhambi ndani ya eneo la hatari na Ronaldo akafunga tena, kabla ya Matthijs de Ligt kufunga bao la tatu dakika za majeruhi.

Ronaldo sasa amefunga katika mechi tisa mfululizo za Serie A kwa Juventus, akiwa mchezaji wa kwanza kufanya hivyo tangu David Trezeguet Desemba mwaka 2005.

Pia amefunga mabao 50 katika mechi 70 tangu alipojiunga na miamba hao wa Italia mwaka 2018.

Ushindi huo umezidi kuimarisha Juventus kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 54 baada ya mechi 22, huku wakiwa wamewapita pointi sita Inter Milan.

## HABARI MICHEZO

# Solskjaer atetea ubutu wa Martial

**MANCHESTER,** England


KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amemtetea mshambuliaji wake Anthony Martial kwa kutokufunga.

Martial hayupo kwenye kiwango kizuri baada ya kufunga bao moja tu katika mechi sita zilizopita kwenye mashindano yote akifunga dhidi ya timu ya daraja la pili ya Tranmere Rovers kwenye mchezo wa FA mwezi uliopita.


Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, alishindwa kufunga kwenye mchezo wa United wa Jumamosi uliomalizika kwa sare ya bila kufungana dhidi ya Wolves, lakini Solskjaer alimtetea mchezaji huyo wa Ufaransa.

"Ametupa kila kitu. Nafikiri alianza katika mechi nane zilizopita mwezi uliopita, na pengine akikimbia kwa asilimia 20 zaidi ya aliyofanya wakati nilipokuja hapa," alisema Solskjaer. "Nina uhakika atafunga tu, kwa sababu ni kawaida kwake kufanya hivyo na nina imani kubwa juu yake."

Martial amefunga mabao nane ya Ligi Kuu katika mechi 19, na mabao 12 kwenye mashindano yote msimu huu.




# ARTETA ALALAMIKIA UWANJA WA BURNLEY



**LONDON,** England

MIKEL Arteta ameelezea hali ya Uwanja wa Turf Moor kama changamoto kwa Arsenal kupata ushindi wakati wakitoka sare ya bila kufungana dhidi ya Burnley.

Baada ya kupata nafasi mbili kwenye mchezo huo wa Jumapili kupitia kwa Alexandre Lacazette na Pierre-Emerick Aubameyang, Arsenal walipata wakati mgumu kwa muda mrefu na kushindwa kutengeneza nafasi za kufunga.

Arteta alikubali kwamba kikosi chake hakikuwa kwenye kiwango cha kuvutia, lakini alitumia muda huo kulalamikia uwanja huo.

"Hali ilikuwa ngumu," alisema raia huyo wa Hispania akiwaambia waandishi wa habari. "Nyasi zilikuwa ndefu, hawakuweka maji yoyote na hiyo haiwezi kuisaidia timu kucheza mpira."

Alipoulizwa kama hali hiyo ilitarajiwa na Arsenal, Arteta alijibu huku akitabasabu: "Hakika kabisa. Sikuweka maji kwenye uwanja wa mazoezi jana (juzi), hivyo nilitarajia hili.

"Hiyo inakufanya ushindwe kucheza vizuri. Lakini ndio mpira. Wao Burnley walifanya vizuri."

# *Conte akunwa na kiwango cha Eriksen*

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte alisisitiza alifurahishwa na kiwango cha Christian Eriksen licha ya kumtoa uwanjani mapema kipindi cha pili wakati Inter Milan ikishinda 2-0 dhidi ya Udinese.

Baada ya kuwasili kutoka Tottenham, Eriksen alitokea benchi katikati ya wiki iliyopita kwenye mchezo wa Kombe la Coppa Italia dhidi ya Fiorentina, akichukua nafasi ya Alexis Sanchez.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark alipewa nafasi ya kuanza kwenye mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Jumapili, akigusa mpira mara 51 na akicheza kwa kiwango cha asilimia 78 cha pasi katika dakika 58 alizocheza.

Matokeo yalikuwa ni 0-0 wakati akitolewa nje, lakini Inter walipata pointi zote tatu shukrani kwa mabao mawili ya Romelu Lukaku, ambapo sasa amefikisha mabao 16 kwenye Serie A.

Conte, ambaye alishuhudia timu yake ikitoka sare katika mechi tatu mfululizo alisema aliridhishwa na kiwango cha Eriksen kwa kipindi alichokuwa dimbani mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27.

"Nafikiri hiyo ni nzuri zaidi kwa mtu aliyefika ndani ya siku tano zilizopita, na hatutakiwi kusahau kwamba tulimuwaisha kumchezesha kwa sababu hatukuwa na viungo, na Eriksen alionyesha kiwango kizuri," alisema Conte akiiambia Sky Sport Italia.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# FATI APENDEZA VIATU VYA SUAREZ BARCA

●●● Sasa vyaonekana kuwapwaya Griezmann na Dembele, aweka rekodi LaLiga kwa...

**BARCELONA,** Hispania

ANTOINE Griezmann alisema anaweza kulifanya hilo. Kocha Quique Setien akadhani Ousmane Dembele anaweza kulifanya hilo. Lakini ni Ansu Fati aliyekabidhiwa kuziba nafasi ya Luis Suarez Barcelona?

**Wakati huu Suarez akiwa hatarajiwi kurudi hadi msimu utakapomalizika, Barca ilitarajiwa kusajili namba tisa katika dirisha dogo la usajili. Na ukweli kwamba hawakufanya hivyo ni kitu ambacho bodi ya klabu hiyo inapaswa kuelezea, lakini wakati mwingine, ushindi wa Jumapili dhidi ya Levante kila kitu ni kuhusu Ansu Fati.**

Setien alimsifu Fati baada ya kinda huyo kuisaidia Barcelona kushinda 2-1 dhidi ya Levante kwenye mechi ya LaLiga Jumapili baada ya kutupia mabao yote mawili.

Fati, 17, alifunga mara mbili katika kipindi cha kwanza wakati Barca ikipunguza wigo wa pointi na kuwakaribia wapinzani wao, Real Madrid kwa alama tatu.

Anakuwa mchezaji kinda zaidi katika historia ya LaLiga kwenye karne ya 21 kufunga mabao mawili, ambapo anavunja rekodi iliyokuwa ikishikiliwa na Juanmi Jimenez.

Fati ameshafunga mabao matano msimu huu na Setien amemsifu kwa kupiga hatua Barcelona, ambayo inajiandaa kuzoea maisha bila majeruhi Suarez hadi mwishoni mwa msimu huu wa 2019-20.

"Nadhani kuwa Ansu ni kijana aliyechomoza, kwamba wote tunajua ana uwezo mkubwa," Kocha Mkuu, Setien aliuambia mkutano wa wanahabari.

"Unapaswa kuelewa kwamba unatakiwa kumpa amani ya akili na kujiamini kutoa alicho nacho ndani.

"Mbali na mabao yake mawili, ninachomsifu ni kazi aliyoifanya katika ulinzi. Alijituma sana. Alitupa suluhisho."

Fati alifunga katika dakika ya 30 na 31 na Barcelona ilikaribia kushinda licha bao la dakika za mwisho za wageni hao kupitia kwa Ruben Rochina.

Setien aliridhika na kiwango cha kikosi chake, ingawa alitarajia kujiimarisha zaidi.

"Ni mwenye furaha na mambo mengi, lakini si kwa kila kitu. Tumepiga mashuti mengi," alisema.

"Tulikuwa na kipindi kizuri cha kwanza, nadhani tulipaswa kufunga mabao zaidi. Tulipoteza udhibiti kidogo katika kipindi cha pili na kuruhusu sana kwetu. Lakini ilikuwa ni kazi nzuri kwa timu."

Barcelona itashuka dimbani ugenini keshokutwa, Alhamisi kucheza mechi ya robo fainali ya Kombe la Mfalme ['Copa del Rey'] dhidi ya Athletic Bilbao.

## ZISIKUPITE

### ABRAHAM AMLILIA CAVANI

STRAIKA wa Chelsea na England, Tammy Abraham amekatishwa tamaa na klabu hiyo kushindwa kumsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain na Uruguay, Edinson Cavani, 32. ***(Mirror)***

### LIVER YAJITOSA KWA SANCHO

LIVERPOOL ipo tayari kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Muingereza Jadon Sancho, 19, katika majira ya joto. ***(Express)***

### ALIA KUMKOSA GIROUD

KOCHA wa Lazio, Simone Inzaghi, amesema kumwongeza mshambuliaji wa Chelsea, Mfaransa Olivier Giroud, 33, katika kikosi chake katika dirisha la Januri, "kungewaongezea nafasi zaidi" ya kutwaa kombe, hiyo ikiwa ni baada ya dili hilo kushindwa kuiva. ***(Gazzetta)***

### BECKHAM KUMFUATA CAVANI

MMILIKI wa Klabu inayoshiriki Ligi Kuu Marekani (MLS), Inter Miami, David Beckham, anataka kuongeza juhudi za kumsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain na Uruguay, Edinson Cavani, 32, wakati mkataba wake utakapomalizika majira ya joto. ***(L'Equipe)***

### WILLIAN KUICHOMOLEA BARCA

WINGA wa Brazil, Willian, 31, angependelea zaidi kusaini mkataba mpya na Chelsea kuliko kujiunga na mabingwa wa Hispania, Barcelona. ***(ESPN)***

### LAMPARD ATAKA KIPA MPYA

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard anataka kipa mpya kuelekea usajili wa majira ya joto kufuatia kiwango kibovu kinachoonyeshwa kwa sasa na Kipa Mhispania Kepa Arrizabalaga, 25. ***(Express)***

### OZIL CHUPUCHUPU ARSENAL

KIUNGO Mjerumani Mesut Ozil, 31, alipewa ofa ya kuondoka Arsenal dakika za mwisho kabla ya dirisha la usajili kufungwa ambapo kocha Mikel Arteta alikuwa tayari kuthibitisha. ***(Mirror)***

### CAVANI AMUIBUA CEREZO

RAIS wa Atletico Madrid, Enrique Cerezo amesema klabu hiyo "haipo hapa kwa ajili ya kuibiwa" kauli hiyo ikiwa ni kwa ajili ya kujibu kitendo cha kushindwa kumsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain na Uruguay, Edinson Cavani, 32, katika dirisha dogo la usajili la Januari. ***(ESPN)***

### LLORENTE AKATALIWA BARCA

BARCELONA ilikataa ofa ya kumsajili mshambuliaji wa Napoli, Mhispania Fernando Llorente, 34. ***(AS)***

### SOUMARE AZITEGA UTD, LIVER

KIUNGO wa Lille, Boubakary Soumare, 20, alikataa ofa nono ya kutua Newcastle Januari kwa matumaini ya kujiunga na Liverpool ama Manchester United katika dirisha la majira ya joto. ***(Le10sport - in French)***

### HODGSON AIONYA BODI PALACE

KOCHA Roy Hodgson ameionya Bodi ya Crystal Palace kwamba inakabiliwa na vita ya kukiboresha kikosi chao katika majira ya joto. ***(Standard)***

HABARI MICHEZO

## Dula Mbabe, Kamata ulingoni

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA Abdallah Pazi 'Dulla Mbabe' anatarajia kupanda ulingoni Februari 8, mwaka huu, kupambana na mpinzani wake Paulo Kamata, kwenye pambano la 'kuvunja ukimya' litakalofanyika jijini Dar es Salaam.

Mabondia hao watakutana katika pambano hilo baada ya kutambiana kwa muda mrefu, kila mmoja 'akijimwambafai' kuwa yeye ni zaidi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana asubuhi baada ya mazoezi, kocha wa bondia huyo, Omary Dame alisema anaendelea kumfua bondia wake kuelekea katika pambano hilo linalotarajiwa kuwa gumu kwa kila upande.

"Bondia wangu anaendelea vizuri kuelekea katika pambano hilo naomba mashabiki wetu wajitokeze kwa wingi siku hiyo kumshangilia," alisema.

Naye Dula Mbabe alisema yuko vizuri kukutana na mpinzani wake huyo, na kumtaka aanze kukaa sawasawa.

Alisema hana shaka na pambano hilo kutokana na uzoefu mkubwa aliokuwa nao.

"Naomba mashabiki wangu waje kwa wingi kuona kichapo nitakachompa mpinzani wangu," alisema Dula.

## Mtibwa kujiuliza kwa Ruvu Shooting

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kufanya vibaya katika mechi yake iliyopita, Mtibwa Sugar imepania kujiuliza kwa kuibuka na ushindi itakaposhuka dimbani kesho kuikaribisha Ruvu Shooting katika mchezo mwingine wa Ligi Kuu utakaopigwa Uwanja wa Mabatini mkoani Pwani.

Akizungumza baada ya mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Zuberi Katwila alisema anashukuru hana mchezaji yeyote ambaye ni majeruhi, na anatarajia mchezo huo utakuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa.

"Mchezo huo utakuwa mgumu na wenye ushindani kutokana na ukweli kwamba Kocha wa Ruvu Shooting, Salum Mayanga, anaifahamu vizuri timu yetu," alisema Katwila.

Hata hivyo, Katwila alikiri kikosi chake kuonyesha 'kupepesuka' baada ya kutofanya vizuri kwenye michezo ya iliyopita dhidi ya KMC na Yanga baada ya kutoka kutwaa Kombe la Mapinduzi, lakini anaamini kama wachezaji wakifuata maelekezo aliyowapa, wanaweza kupata matokeo.

"Mwenendo wa timu yangu hauridhishi baada ya kutwaa ubingwa wa Kombe la Mapinduzi, lakini naahidi kuendelea kujipanga kwa ajili ya mzunguko ujao, hivyo tunaomba mashabiki wetu waendelee kutusapoti wasikatishwe tamaa na matokeo yaliyopita," alisema.

# AZAM FC HAKUNA KULALA HADI KIELEWEKE - KOCHA

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya timu yao kuwa na mwenendo wa kusuasua, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche, amesema bado hawajakata tamaa ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

**Azam FC juzi ililazimisha sare ya bao 1-1 ugenini Iringa dhidi ya Mbeya City na kufikisha pointi 37 baada ya kushuka dimbani mara 18, ikizidiwa pointi 10 na vinara wa ligi hiyo, Simba ya jijini Dar es Salaam.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Cheche alisema ni mapema kujiondoa katika kinyang'anyiro cha kuwania taji hilo kwa sababu bado mechi zilizobakia ili kumaliza msimu ni nyingi na katika soka lolote linaweza kutokea.

Cheche alisema mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ni ngumu na zenye ushindani, lakini kikosi chake kitaendelea kupambana kuhakikisha wanatimiza malengo waliyojiwekea.

"Ni mapema kukata tamaa, ingawa tuna tofauti kubwa na anayeongoza ligi, lakini bado nafasi tunayo ya kupambana, tuna mechi nyingi zimebakia, tuna mechi dhidi yao (Simba), hivyo tutaendelea kujiimarisha, malengo yetu ya kutwaa ubingwa bado yako pale pale," alisema Cheche.

Kocha huyo aliongeza kuwa mchezo wao dhidi ya Mbeya City ulikuwa mgumu na mazingira mabaya ya uwanja yalichangia kuufanya mchezo huo kuwa na changamoto nyingi.

"Mechi ilikuwa ngumu na yenye ushindani, ila hali ya uwanja na mvua haikuwa rafiki, mpira ulikuwa hauchezeki, angalau kipindi cha pili vijana walicheza vizuri, mazingira yalikuwa ni magumu, ila tunapenda kuwaambia mashabiki wetu wasikate tamaa bado mbio za ubingwa ziko wazi," Cheche aliongeza.

Alisema kikosi chake kilitarajia kurejea jijini jana jioni ili kuendelea na maandalizi ya kuivaa Tanzania Prisons Februari 5, mwaka huu kabla ya siku tatu baadaye kuvaana na KMC FC katika mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

UMETISHA...



Winga wa Yanga, Bernard Morrison (mgongoni), akimpongeza mshambuliaji wa timu hiyo, David Molinga baada ya kuifungia Yanga bao pekee wakati ikishinda 1-0 dhidi ya Mtibwa Sugar katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Taifa juzi. **PICHA : JUMANNE JUMA**

## *Simba Queens, Yanga Princess dimbani*

**Na Mwandishi Wetu**

LIGI Kuu ya Wanawake Tanzania inatarajiwa kuendelea leo katika viwanja sita tofauti nchini ambapo Simba Queens itakuwa ugenini kuwakabili Tanzanite Queens jijini Arusha, huku TSC ikiwakaribisha Yanga Princess kwenye Uwanja wa Gwambina, Mwanza.

Ligi hiyo ilisimama kwa muda ili kupisha timu za Taifa za Wanawake (U -17 na U-20) zilizokuwa zinapeperusha bendera ya nchi katika mashindano ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia.

Kocha wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi' aliliambia gazeti hili jana kikosi chake kilifika salama Arusha na wachezaji wako katika hali nzuri kwa ajili ya kusubiri mchezo huo wa leo.

Mgosi alisema malengo ya Simba Queens ni kutwaa ubingwa wa ligi hiyo kwa mara ya kwanza, hivyo wamejipanga kucheza soka la kiwango cha juu.

"Ligi ni ngumu, lakini sisi kwetu tumesema kila mechi ni sawa na fainali, tumejipanga kupambana mwanzo mwisho, sina majeruhi na namuomba Mungu kesho wachezaji wote waamke salama," alisema nyota huyo wa zamani wa Simba na Taifa Stars.

Naye Kocha wa Yanga Princess, Edna Lema, amesema wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya mechi hiyo na wanaufahamu ugumu wa kucheza na TSC.

"Timu za Mwanza zinajipanga, lakini na sisi tumejipanga, kama watatulia na kufuata maelekezo vizuri, naamini safari yetu ya kufuata pointi tatu itamalizika vizuri," Lema alisema.

# Michezo

Jumanne Februari 4, 2020

Nipashe



**Conte akunwa na kiwango cha Eriksen** UKURASA 29

**MTU KATI...**



Mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi akiwekwa 'mtu kati' na mabeki wa Levante kwenye mechi ya LaLiga iliyopigwa katika Uwanja wa Camp Nou juzi na wenyeji hao kushinda 2-1, shukrani kwa kinda Ansu Fati aliyetupia yote mawili. **HABARI UK. 30**

# Simba yataka ubingwa na rekodi ya pointi 100

## ●●● Kusaka ya 50 kwa Polisi Tanzania leo, Matola akiri kazi ipo, Maafande kutumia wembe wa Yanga...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI ikiendelea kukosa huduma za mawinga wake wapya Luis Miquisone na Shiza Kichuya, Simba itashuka katika Uwanja wa Uhuru leo ikiwa na lengo la kuvuna pointi tatu dhidi ya 'Maafande' wa Jeshi la Polisi Tanzania ili kufikisha pointi 50 kuelekea 100 walizolenga kuzifikia msimu huu.

> **Hadi sasa Simba ina pointi 47 ikiwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara, na mechi hiyo ya leo ni ya kukamilisha mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo yenye timu 20.**

Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara alimwambia mwandishi wetu kuwa lengo la klabu hiyo ni kuandika rekodi mpya kwa kuwa timu ya kwanza kufikisha pointi 100.

"Simba ni timu ya rekodi, tunataka ubingwa na ponti 100, kesho [leo] tunataka kufikia nusu ya lengo, hakuna timu iliyowahi kufikisha pointi 100," Manara alisema.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu, Simba watashuka uwanjani katika mechi hiyo wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Coastal Union, wakati Polisi Tanzania iliwafunga JKT Tanzania bao 1-0, kwenye mchezo ambao ulimalizika siku ya pili kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha jijini Dar es Salaam.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema mechi hiyo itakuwa ngumu licha ya kwamba wachezaji wengi walioko katika kikosi cha Polisi Tanzania anawafahamu na wamepitia katika 'mikono yake'.

Matola alisema mara nyingi makocha wanapata changamoto wanapokutana na timu zao za zamani na kwa kuzingatia hilo, amewaandaa Simba kupambana kwa dakika zote za mechi hiyo ya kiporo.

"Ligi ni ngumu na hakuna mechi ndogo, tumejiandaa kupambana kama tulivyopambana katika michezo iliyopita, lengo letu ni kuendelea kushinda na kujiimarisha pale juu katika msimamo, walioko chini yetu wanapambana kutufikia, sisi tunatakiwa tuongeze mbio," Matola alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, aliliambia gazeti hili kuwa anajua Simba ni moja ya timu ngumu, lakini vijana wake wamejiandaa kuwakabili na hawana wasiwasi wowote kuelekea mchezo huo.

Malale alisema ushindi walioupata dhidi ya JKT Tanzania umewasaidia kuongeza nguvu na wanaamini wanaweza 'kuwasimamisha' Simba katika mchezo huo.

"Sisi tumekuja kusaka pointi, tutapambana na kucheza kwa utulivu, unapokuwa ugenini halafu unacheza na Simba ni lazima uingie na mbinu mpya, usicheze kama unavyocheza kila siku, tutaingia tofauti, malengo yetu ni kupata ushindi," alisema Hamsini.

Makamu Mwenyekiti wa Polisi Tanzania, Robert Munisi, alisema kikosi chake kimekuja kuendeleza operesheni 'chukua pointi' kama kilivyofanya kilipokutana na Yanga mapema mwanzo wa msimu.

"Tunaijua Simba, tunajua nguvu zao ziko wapi na tunajua upungufu wao ulipo, tumewasoma, kikubwa tuwaombee uzima vijana wetu waje kutekeleza kile tulichodhamiria," Munisi alisema.

Alimtaja golikipa wao mpya Peter Manyika ameshapata ITC na anaweza kucheza katika mchezo huo wa leo endapo benchi la ufundi litaamua kumtumia.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Ishamhyo ni kati ya JKT Tanzania dhidi ya Coastal Union kutoka jijini Tanga.


# Samatta awaangukia wanaomharibia Aston Villa

**Na Mwandishi Wetu**

NAHODHA wa timu ya Taifa (Taifa Stars) na mshambuliaji mpya wa Aston Villa, Mbwana Samatta amewataka mashabiki wake kuacha tabia ya kuandika maneno makali au lugha isiyofaa katika akaunti za wachezaji au klabu hiyo kwa sababu hali hiyo inamkera.

Baada ya Samatta kusajiliwa na Aston Villa inayoshiriki Ligi Kuu England, mashabiki wake na hasa Watanzania wamekuwa wakiandika ujumbe katika akaunti za nahodha huyo na klabu yake mpya nyingine zikiwa nzuri na baadhi zikionekana kama za 'kichochezi' zinazoweza kumvurugia.

Baadhi ya Watanzania, wamekuwa wakiandika ujumbe katika mtandao wa Aston Villa, wakimshutumu nahodha wa klabu hiyo, Muingereza Jack Grealish kwa madai ya kwamba amekuwa mchoyo wa kumlisha pasi Samatta.



Akizungumza na gazeti hili, Samatta ambaye juzi alifungua akaunti ya mabao katika Ligi Kuu England walipocheza dhidi ya AFC Bournemouth, alisema hali hiyo haimfurahishi na anawaomba mashabiki wake kuacha mara moja.

Samatta alisema anafahamu mapenzi ambayo mashabiki wake wanampa na wanavyomtakia mafanikio, lakini kuendelea kuandika maneno ya kashfa au matusi, hakuleti picha nzuri na uamuzi huo haupendi.

"Mashabiki wa soka Tanzania nafahamu kuwa mnanipenda kijana wenu na mnapenda nifanye vizuri katika timu yangu mpya, lakini nawaomba muache kutoa maneno ya kashfa au yenye mlengo mbaya katika akaunti za timu au wachezaji, binafsi sifurahiswi," Samatta alisema.

Mashabiki ambao wanaandika zaidi kwa lugha ya kiswahili wamekuwa pia wakiandika maneno yasiyostahili kwa wachezaji wa Aston Villa jambo ambalo Samatta anaona halitasaidia katika kumjenga kwenye safari yake ya mafanikio nchini England.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >